**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA TISA**

**Kikao cha Tatu – Tarehe 1 Novemba, 2007**

*(Mkutano Ulianza Saa 3.00 Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 28

**Majibu ya Maswali Bungeni**

**MHE. JUMA HASSAN KILLIMBAH** aliuliza:-

Kwa kuwa baadhi ya majibu ya Serikali kwa maswali ya Waheshimiwa Bungeni, mara nyingi yamekuwa hayamridhishi muuliza swali na hata wananchi anaowawakilisha Bungeni hasa pale Serikali ilipotoa majibu kama Mheshimiwa Mbunge avute subira, Mheshimiwa Mbunge ashirikiane na Halmashauri yake na au hali ya Serikali itakapokuwa nzuri na kadhalika.

(a) Je, Serikali inaweza kutueleza ni taratibu gani zinazostahili kuchukuliwa hasa pale ambapo majibu ya maswali yamepitiliza muda wa utekelezaji na vile vile kutofanikiwa kwa juhudi na nyingine za kupata ufumbuzi kutoka kwenye Halmashauri?

(b) Je, kwa nini Serikali isitoe majibu yenye ukomo ili muuliza swali awe na majibu ya kuwapa wapiga kura wake badala ya kuambiwa avute subira isiyo na mwisho?

(c) Je, Serikali iko tayari kuwa na utaratibu wa kufuatilia majibu ya Mawaziri na kuhimiza utekelezaji wa ahadi za Serikali?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, MAAFA NA KAMPENI DHIDI YA UKIMWI (MHE. DR. LUCAS SIYAME)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juma Hassan Killlimbah, Mbunge wa Iramba Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, maswali ya Waheshimiwa Wabunge, yanapatiwa majibu kamilifu kutoka Serikali kwa mujibu wa Kanuni za Bunge hili Tukufu. Majibu ya Serikali kwa kuzingatia Kanuni ya 37 A (1), (2) na (3) yamekuwa yakionyesha hatua zilizochukuliwa, zinazochukuliwa au zitakazochukuliwa na Serikali katika utekelezaji wa jambo lenyewe. Mara nyingi utekelezaji wa jambo lolote unahitaji raslimali za aina mbalimbali ili kuweza kulifanikisha.

Rasilimali hizo zinahitaji kuunganishwa na hilo ni jukumu la viongozi wote wa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa ambazo sisi Waheshimiwa Wabunge, ni sehemu ya uongozi huo. Kwa kuzingatia nafasi zetu ndani ya Halmashauri za Serikali za Mitaa, inapotokea ahadi ya jambo fulani haijatekelezwa au imechukua muda mrefu, kwa kweli ni jukumu letu sote kuwabana watendaji husika kwenye mabaraza na au kupitia Kamati zinazohusika za Halmashauri zetu ili kuhakikisha utekelezaji wake.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, mipango ya Serikali inazingatia sana fedha zinazotengwa kwenye Bajeti. Mipango inayotekelezwa huainishwa na kuwekewa malengo yanayozingatia uwezo wa fedha na upatikanaji wa rasilimali zingine wakiwemo watalaam, vifaa na vitendea kazi na muda muafaka.

Dhana hiyo ndiyo inayotumiwa na kuzingatiwa na Serikali wakati inapotoa majibu ya masuala mbalimbali. Serikali yetu kama zilivyo nyingine duniani imekuwa makini na sikivu sana katika kushughulikia masuala yanawagusa wananchi na kuathiri shughuli zao. Yanapojitokeza masuala ya aina hii na ambayo hayatabiriki, mara nyingi huathiri mwenendo mzima wa utekelezaji wa malengo ya Bajeti na hivyo kusababisha baadhi ya shughuli kutokamilishwa na pengine kuahirishwa. *(Makofi)* Inapotamkwa kwamba tuvute subira nadhani ni ishara njema kuwa nia ya Serikali kutekeleza jambo husika bado ipo.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa kufuatilia majibu ya Serikali hususan ahadi zinazotolewa na Mawaziri upo na unaratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu. Taarifa ya utekelezaji wa ahadi hizo za Serikali imekuwa ikitolewa mara mbili kwa mwaka na kusambazwa kwa wadau wote ikiwemo Ofisi ya Bunge na Waheshimiwa Wabunge.

**MHE. JUMA HASSAN KILLIMBAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa utekelezaji wa ahadi, au maswali yanayoulizwa na ilani labda ya chama ambacho kinatawala na kwa kuwa mara nyingi labda panapotokea kuwepo kutokutekeleza zile ahadi zinaleta usumbufu hasa kwa sisi Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu tulipokuwa tunaomba kura tuliomba kupitia Ilani ya Chama.

Je, Serikali ipo tayari sasa ikaainisha yale majibu yake yanayotolewa na maswali yanayoulizwa na Wabunge, majibu yake na ahadi ambazo hazijatekelezwa ili inapofika

mwisho wa mwaka kwa kila mwaka ili sisi Wabunge tukawaeleze sawa sawa wananchi kwamba ahadi hizi hazijatimia kwa sababu ambazo Serikali imezitaja?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, MAAFA NA KAMPENI DHIDI YA UKIMWI (MHE. DR. LUCAS SIYAME):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Serikali iliyopo madarakani hutekeleza Ilani yake na ndiyo sababu mara mbili kwa mwaka Serikali hutoa maelezo ya shughuli ambazo imekamilisha ili ifikapo mwisho wa kipindi chake iweze kuelezea ni kwa kiwango gani imetekeleza. Kwa hiyo, tunaamini kwamba nia ya Serikali ni kuhakikisha inatekeleza Ilani ya Uchaguzi.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa katika swali la msingi, moja ya majibu yaliyotolewa ni kwamba Mheshimiwa Mbunge, ashirikiane na Halmashauri yake na kwa kuwa neno hili linaweza kutafsiriwa kwamba Mbunge amejiandikia swali bila kushirikiana na Halmashauri, jambo ambalo linaweza kutafsiriwa kwamba Mbunge hashirikiani na Halmashauri yake.

Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kutueleza kwamba kauli hiyo, siyo kauli nzuri ya kumwambia Mheshimiwa Waziri ndani ya Ukumbi wa Bunge, wakati Mbunge anapoandika, anaandika kwa niaba ya Halmashauri yake na wapiga kura wake?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, MAAFA NA KAMPENI DHIDI YA UKIMWI (MHE. DR. LUCAS SIYAME):** Mheshimiwa Naibu Spika, bado nasisitiza kwamba jibu lililotolewa katika swali la msingi bado ni sahihi kwani bado naamini kabisa kwamba Mbunge bado ni Diwani wa Halmashauri. Kwa hiyo, kila kitu anachotenda sharti ashirikiane na Halmashauri yake.

Na. 29

**Maswali ya Bunge Kutojibiwa kwa Wakati**

**MHE. ZUBEIR A. MAULID (K.n.y. MHE. MOHAMMED R. ABDALLAH** aliuliza:-

Kwa kuwa Mbunge anapouliza swali kwenda Wizara husika wakati mwingine swali hilo linachukua muda mrefu kujibiwa na pengine hata kupita miezi sita au zaidi na wakati mwingine swali hilo linakuwa limepitwa na wakati kwa maana halina mantiki tena kwa wakati huo?

(a) Je, ni sababu zipi zinazofanya majibu ya maswali hayo kuchelewa sana?

(b) Pamoja na maswali mengi kutoka kwa Wabunge. Je, Serikali haioni kuwa hakuna sababu za msingi kwa maswali kutojibiwa kwa muda mfupi?

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, MAAFA NA KAMPENI DHIDI YA UKIMWI (MHE. DR. LUCAS SIYAME)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohammed Rished Abdallah, Mbunge wa Pangani lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumuarifu Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako tukufu, kwamba maswali ya Bunge yamewekewa utaratibu wa kuzingatia kwenye kanuni ya 33 ya Kanuni za Kudumu za Bunge (Toleo la 2004).

Kwa mujibu wa kanuni ilitotajwa, kuchelewa sana kwa maswali ya Mbunge mmoja kujibiwa kunatokana na nia nzuri ya Serikali kutaka kutekeleza utaratibu uliowekwa unaotoa fursa sawa bila upendeleo wa aina yeyote na unaojali manufaa ya Wabunge wote kama wawakilishi wa makundi mbalimbali.

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wote Serikali imekuwa ikizingatia na kutekeleza wajibu wake katika eneo linalohusu maswali kama yanavyopangwa na Ofisi ya Spika kwenye *order paper*. Ni vyema niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kuwa utaratibu wetu kupitia kanuni ni mzuri sana na unalenga kutoa nafasi kwa Wabunge wote kuuliza maswali Serikali.

Kwa mfano, haitaeleweka miongoni mwa wananchi na hata sisi wenyewe Wabunge endapo itasikika mara nyingi Mbunge mmoja tu au baadhi tu wakiuliza maswali Bungeni wakati fursa hiyo ni ya Wabunge wote. Aidha, muda tuliopanga kwa ajili ya maswali unaonekana ni mfupi ukilinganishwa na muda unaotumika kwa shughuli nyingine za Bunge.

Hata hivyo, mtazamo huu siyo sahihi kwani ukizingatia mgawanyo wa muda kwa shughuli zote zinazopaswa kutekelezwa na Bunge utaona kuwa kwa wastani muda wa maswali uliotengwa kwenye mikutano ya kawaida na mikutano ya Bajeti unatosha.

Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali pia inaona hakuna sababu za msingi kwa maswali ya Wabunge kutojibiwa kwa muda mfupi lakini utaratibu uliopo unaofaa uendelee kuzingatiwa ili kuwanufaisha Wabunge wote.

**MHE. ZUBEIR A. MAULID:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa katika swali la msingi la Mheshimiwa Mbunge alichozingatia zaidi ilikuwa ni swali kuletwa halafu likapitwa na wakati kabla halijajibiwa. Je, Serikali inasemaje kuhusiana na maswali kuyaangalia ili yaje yajibiwe kabla hajapitwa na wakati? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, MAAFA NA KAMPENI DHIDI YA UKIMWI (MHE. DR. LUCAS SIYAME):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli maswali yanatakiwa kujibiwa kabla hayajapitwa na wakati. Lakini kama nilivyokwishasema kwenye jibu la msingi kwamba kuna mambo mawili ya msingi kwanza ni kuhakikisha kwamba kila Mbunge, anapewa nafasi ya kuuliza maswali na ya pili ni kuhakikisha kwamba majibu yanayotolewa ni sahihi. Hivyo basi, nia ya Serikali ni

kutoa majibu kwa wakati muafaka lakini yale maswali yaliyofanyiwa utafiti na kujibiwa kwa kina na pia kwamba hapewi mtu mmoja kuuliza mara nyingi kuliko wengine.

Na. 30

**Ubovu wa Barabara Dar es Salaam**

**MHE. FATMA A. FEREJI (K.n.y. MHE. MHE. FATMA ABDALLAH TAMIM)** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi hulipa kodi mbalimbali kwa lengo la kupata huduma bora kama barabara, elimu na kadhalika. Je, kwa nini barabara nyingi Dar es Salaam hasa za Mjini zimekatwakatwa na kuchelewa kutengenezwa hivyo kuwa mashimo yanayosababisha ajali?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mehshimiwa Fatma Abdallah Tamim, Mbunge kutoka Baraza la Wawakilishi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ubovu wa barabara za Dar es Salaam hususani za maeneo ya Mjini unatokana na barabara hizo kutokarabatiwa kwa muda mrefu. Barabara hizo ambazo zilifanyiwa matengenezo makubwa mnamo mwaka 1992 – 1995 kwa msaada wa Serikali ya Japan kupitia shirika lake la msaada la *JICA* na zilipewa muda wa uhai *(Life Span)* wa miaka mitano hadi kumi ambazo tayari muda huo umepita. Tangu wakati huo barabara hizo hazijaweza kufanyiwa matengenezo makubwa *(Major Repair)* kutokana na ufinyu wa Bajeti, bali ukarabati mdogo mdogo ulikuwa unaendelea kama kawaida.

Kutokana na barabara hizo kutokarabatiwa kwa muda mrefu Serikali iko kwenye mchakato wa mpango kabambe wa usafiri – Dar es Salaam (*Transportation Master Plan)* ambapo ipo kwenye maandalizi ya hatua ya pili. Mpango huu unafadhiliwa na Shirika la Misaada la Japan – Jica chini ya Serikali ya Japan. Utekelezaji wa mpango huu ukitekelezwa utasaidia sana suala la usafiri na uboreshwaji wa mtandao wa barabara na miundombinu mbalimbali katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ubovu wa barabara hizo unaotokana na miundombinu iliyo chini ya ardhi ambayo marekebisho yake ya mara kwa mara huhitaji kukatwa kwa barabara hizo. Aidha, hivi karibuni Serikali kupitia mamlaka ya maji safi na maji taka (*DAWASA*) ilitekeleza mradi mkubwa wa kurekebisha mfumo wa maji taka hivyo kulazimu sehemu kubwa ya barabara za mjini katika Jiji la Dar es Salaam kukatwa.

Ni kweli pia kwamba hatua ya kurudishia lami katika maeneo yaliyokatwa hazikuchukuliwa mara moja kwa sababu mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka walihitaji

muda wa kutosha wa kuunganisha mabomba mapya kwenye majengo yaliyokuwa kwenye eneo la mradi kwenda kwenye mifereji mikuu.

Hata hivyo baadhi ya barabara zilizokatwa wakati wa mradi huo zimekwisha rejeshwa katika hali yake ya awali. Kwa mfano katika Manispaa ya Temeke Barabara ya Chang'ombe, Sterio, Sungwi, Everath, Mbozi na Taifa zimekwisha kamilishwa. Katika Manispaa ya Kinondoni barabara zilizokamilika ni Kajenge, Tunisia, Ali Maua, Chole, Chemchem, Kiyungi, Barabara zingine ni Namanga, Makanya na Kawawa. Katika Manispaa ya Ilala barabara zilizokamilika ni za maeneo ya Kariokoo, Jangwani, Gerezani, Kivukoni, Mchikichini, Upanga na eneo la katikati ya Jiji (Mchafukoge na Kisutu).

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya barabara ambazo hazijarudishwa katika hali yake ya kawaida ni pamoja na ile ya Cocacola (Mwenge), Makanya - Sinza, Malezi Bora (Mikocheni), Mama Land *(Mabibo External)* na Malanga Mwananyala. Serikali inaendelea kuwasiliana na kampuni husika ili ziweze kumaliza sehemu ambazo zimebakia. *(Makofi)*

**MHE. MWINCHOUM A. MSOMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tatizo hili pia linaikumba barabara ya Uhuru ambayo ni barabara inayotumika kupita viongozi wetu wa kitaifa wanaokuja katika nchi yetu. Je, Serikali ina gani mpango madhubuti wa kuweza kuboresha barabara hiyo ya Uhuru? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Uhuru kama zilivyokuwa barabara nyingine ambazo zimekwisha kamilishwa na zimekwishatengenezwa.

Sisi kama Serikali tunawasiliana na kampuni ile ambayo ilikuwa inafanya ukarabati katika mifereji ya maji machafu ili pia barabara hii iweze kutengenezwa.

Sasa hivi kama nilivyosema Mkoa wa Dar es Salaam una mpango kabambe wa kuhakikisha kwamba barabara zote hizi zinakarabatiwa, ikiwemo barabara ya Uhuru ambayo ni barabara kubwa na wote tunafahamu. Viongozi wote wanapita barabara hiyo. Itakarabatiwa na Serikali kama nilivyoahidi kwenye swali langu la msingi.

Na. 31

**Rasilimali Muda**

**MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA** aliuliza:-

Kwa kuwa muda ni rasilimali muhimu kaitka kuleta maendeleo ya nchi yetu:-

(a) Je, ni nani mwenye dhamana ya kudhibiti matumizi ya rasilimali hiyo na kuwaeleza wananchi manufaa ya matumizi mazuri ya muda kama ilivyo kama nchi nyingi hasa zilizoendelea?

(b) Je, ni hatua gani za kisheria huchulikuliwa kwa viongozi au wananchi wanaotumia vibaya rasilimali muda?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Devota Likokola, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Devota Likokola kwamba muda ni rasilimali muhimu katika kuleta na kusukuma maendeleo ya nchi yetu na kwamba matumizi mabaya ya muda na tabia ya kutokuzingatia muda katika utendaji ni ukiukwaji mkubwa wa misingi ya utawala Bora.

Katika utumishi wa umma, kuna miongozo mbalimbali kama vile nyaraka za utumishi, kanuni za kudumu za utumishi, kanuni za maadili n.k. kanuni hizi zinawaongoza watumishi namna ya kutumia vizuri muda.

Miongozo hiyo pia inaelezea:-

- Muda wa kuanza kazi;
- Muda wa Kumaliza kazi;
- Siku za mapumziko kwa wiki;
- Siku za mapumziko kwa ajili ya Sikukuu;
- Muda wa kwenda likizo kwa mwaka; na
- Adhabu zinazotolewa kwa watoro kazini, wavivu, walevi na kadhalika.

Kwa hiyo, mfanyakazi anapaswa kuzingatia maelekezo yaliyoko kwenye miongozo hiyo. Mtumishi yeyote asiyezingatia yaliyoainishwa kwenye miongozo hiyo huchukuliwa hatua za kinidhamu. Aidha, katika kujenga tabia ya matumizi mazuri ya muda Serikali imeanzisha utaratibu wa kuwa na mikataba ya huduma kwa mteja *(Client Service Charter).*

Mheshimiwa Naibu Spika, mikataba hii huainisha:-

- Aina ya huduma itolewayo na taasisi husika;
- Utaratibu wa utoaji huduma; na
- Muda unaotumika kutoa huduma hiyo.

Pia katika utaratibu huo huo watumishi hupimwa utendaji wao wa kazi kutokana na tija *(Result Oriented Performance).*

Mheshimiwa Naibu Spika, watumishi wa umma wanatakiwa kuwa waaminifu na kutumia muda wa kazi kutekeleza wajibu wao. Aidha, hawaruhusiwi kutumia muda wa kazi kwa shughuli zao binafsi au kwa mapumziko isipokuwa kama wamepewa idhini ya kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika jibu la sehemu (a) Kiongozi au mtumishi au mwananchi anayetumia vibaya rasilimali muda ni kwamba anakiuka misingi ya utawala bora kwa sababu ya kupata ujira ambao hakuufanyia kazi.

Huu ni wizi, hivyo mamlaka zinazohusika kwa maana ya mwajiri anatakiwa kumchukulia hatua za kinidhamu kama vile:-

- Kupewa onyo/karipio;
- Kusimamishwa au kufukuzwa kazi; na
- Kushushwa cheo au kutopandishwa cheo na hata kushtakiwa mahakamani.

**MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa maelezo ambayo Mheshimiwa Waziri ameyatoa yanalenga sana watu ambao ni watumishi wa umma. Tunafahamu ya kwamba Serikali yetu ina watu wengi sana na wananchi wengi sana wapo katika sekta binafsi. Je, ni hatua gani zinatumika katika watu ambao hawako katika ajira na sekta ya umma? (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Naibu Spika, watumishi wa Sekta ambazo siyo za umma huwa wanazingatia mikataba ambayo wamewekeana na waajiri wao.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wengi wanafahamu kwamba baadhi ya wafanyakazi wa Serikali ni wazembe na wanapiga *story* saa za kazi. Je, Waziri unaweza kutuambia na kwa kuwa na mwenyewe amekiri kwamba sheria zipo, anaweza kutuambia ni wafanyakazi wangapi wamedhibitiwa kutokana na kutumia muda wao vibaya? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Hilo ni kazi lakini Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora jaribu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Naibu Spika, itakumbukwa kwamba ni juzi tu siku ya Jumanne tulijadili Muswada wa kurekebisha sheria ya Utumishi wa Umma.

Pamoja na mambo mengine yaliyozingatiwa ni haya ambayo anayasemea Mheshimiwa Mbunge. Kwa hakika siyo rahisi kupata takwimu ambazo anazihitaji kwa sasa. Isipokuwa tutamtafutia baadaye wakati tukirejea maofisini.

Na. 32

**Sheria Zinazotekelezwa na Pande za Muungano**

**MHE. VUAI ABDALLAH KHAMISI** aliuliza:-

Kwa kuwa, kumekuwa na Sheria mbalimbai za Nchi ambazo zinatekelezwa katika upande wa pili wa muungano – Tanzania Zanzibar lakini hadi sasa utekelezaji wake hauonekani huko Tanzania Zanzibar :-

(a) Je, ni kwa nini kumekuwa na hali ya aina hiyo?

(b) Je, ni lini tume ya Nyuklia (*Atomic Energy Commission*) inayotakiwa kufanya kazi zake Zanzibar kupitia Sheria Na. 7 ya mwaka 2003 itaanza rasmi kufanya kazi?

(c) Je, ni kwa sababu gani Tume ya Nyuklia haina tawi lake Tanzania licha ya kutakiwa kisheria kufanya kazi zake huko Tanzania Zanzibar?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulijibu swali la Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamisi, Mbunge wa Magogoni, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Sheria zinazotungwa na Bunge zinatumika Zanzibar kwa kuzingatia masharti ya Ibara ya 64 (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Ibara ya 132 ya Katiba ya Zanzibar. Ibara ya 64 (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatamka kwamba:-

“Sheria yoyote iliyotungwa na Bunge kuhusu jambo lolote haitatumika Tanzania Zanzibar ila kwa mujibu wa masharti yafuatayo:-

(i) Sheria hiyo iwe imetamka wazi kwamba itatumika Tanzania Bara na vilevile Tanzania Zanzibar au iwe inabadilisha, kurekebisha au kufuta Sheria inayotumika Tanzania Zanzibar, au

(ii) Sheria hiyo iwe inabadilisha, kurekebisha au kufuta Sheria iliyokuwa inatumika tangu zamani Tanzania Bara ambayo inatumika pia Tanzania Zanzibar kwa mujibu wa Mapatano ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ya mwaka 1964 au kwa mujibu wa Sheria yoyote ambayo ilitamka wazi kwamba itatumika Tanzania Bara na vilevile Tanzania Zanzibar, au

(iii) Sheria hiyo iwe inahusu mambo ya Muungano na kila inapotajwa Tanzania katika Sheria yoyote ifahamike kuwa Sheria hiyo itatumika katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa ufafanuzi uliotolewa na masharti ya ibara hii".

Aidha, Ibara ya 132 (2) ya Katiba ya Zanzibar inaelekeza kwamba nanukuu:-

"(2) Sheria kama hiyo lazima ipelekwe mbele ya Baraza la Wawakilishi na Waziri anayehusika".

Kutokana na utaratibu huu wa Kikatiba, Sheria za Muungano wa Tanzania ni lazima kufuata taratibu hizi za kikatiba ili ziweze kutumika pande zote za Muungano.

(b) Kwa hivi sasa Tume ya Tume ya Nyukilia *(Atomic Energy Commission)* haifanyi kazi zake Zanzibar kupitia sheria namba 7 ya mwaka 2003 mpaka pale Waziri mhusika atakapowasilisha sheria hii katika Baraza la Wawakilishi.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, sababu zilizofanya tume ya Nyukilia kutokuwa na tawi lake Tanzania Zanzibar ni la Kisheria na Kikatiba. Pindi zitakapokamilika Tume itafanya kazi zake pande zote mbili za Muungano. *(Makofi)*

**MHE. VUAI ABDALLAH KHAMISI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Waziri, ningeomba sana kuzingatia pande mbili za Muungano basi sheria hii lini zitafanya haraka sana kuanza ili kuzingatia pande mbili za Muungano?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika jibu la msingi ni kwamba sheria hii inapaswa kwanza kupelekwa katika Baraza la Wawakilishi ipitishwe ndipo iweze kufanya kazi pande zote mbili. Tukiwa katika Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano, kwa maeneo ambayo yana utata kama huu jukumu letu ni kuhakikisha kwamba suala hili linafikishwa katika vikao vya Kamati ya Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi, ili hatimaye liweze ufumbuzi na sheria hii itumike pande zote.

**NAIBU SPIKA:** Sasa ningependa nimtambulishe kwa kipekee tu Mheshimiwa Spika wa Bunge la Afrika Mashariki Abdi Rahim Abdi. *Can you please raise up*. Amefuatana na msaidizi wake Ndugu Paul Masami. Nitamtangaza rasmi kwa sababu swali linalofuata ni la Afrika Mashariki. Kwa hiyo, muone Spika wake yuko. (*Kicheko*)

Na. 33

**Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki**

**MHE. MHONGA SAIDI RUHWANYA** aliuliza:-

Kwa kuwa Bunge la Afrika Mashariki limeshindwa kufanya kazi kwa kipindi cha zaidi ya nusu mwaka kutokana na kutoapishwa kwa Wabunge wa Kenya, pamoja na kwamba Ibara ya 50 ya Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki inazungumzia chaguzi za Wabunge wa Bunge hilo.

Je, kwa nini Jumuiya isiweke taratibu zitakazofuatwa na nchi zote wanachama na taratibu za uchaguzi ziendane na Ibara ya 50 ya Mkataba ili kuepusha usumbufu uliotokea.

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Kuchelewa kuapishwa kwa Waheshimiwa Wabunge wa Afrika Mashariki kulitokana na kesi ya madai Namba 1 ya mwaka 2006 iliyowasilishwa katika Mahakama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika kesi hiyo Prof. Peter Anyang' Nyongo na wenzake 10 walifungua kesi wakipinga uchaguzi wa Wabunge wa Afrika Mashariki nchini Kenya kwamba haukufuata taratibu. Mahakama ya Afrika Mashariki iliamua kuwa hapakuwa na uchaguzi wa Wabunge wa Afrika Mashariki nchini Kenya kuwa urudiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo furaha kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa uchaguzi nchini Kenya ulifanyika upya kwa kuzingatia matakwa ya Kifungu cha 50 cha Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kama mahakama ilivyoagiza.

Baada ya Wabunge kutoka Kenya kupatikana, Wabunge wote wa Bunge la Afrika Mashariki waliapishwa mwezi Juni, 2007 na kuwezesha kazi za Bunge la Jumuiya kuendelea kwa mtiririko wa kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika Kifungu cha 50 (1) umetoa mamlaka makubwa kwa mabunge ya nchi wanachama kuangalia jinsi ya kuwapata wawakilishi wao katika Jumuiya kulingana na muundo na mazingira ya kisiasa kwa kila nchi. Utaratibu huu unatoa fursa kwa kila Bunge la nchi

husika kuweka taratibu za kawachagua Wabunge wa Afrika Mashariki kwa kuzingatia mazingira ya kisiasa ya kila nchi. Aidha, nchi wanachama zimeanza kuangalia uwezekano wa kuwa na utaratibu unaofanana wa kuchagua Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki.

**MHE. MHONGA SAIDI RUHWANYA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi niulize swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa muda ni mali na Bunge hilo halikufanya kazi kwa muda wote huo hivyo Jumuiya ilikosa utekelezaji wa maamuzi fulani. Je, ni hasara kiasi gani ilipatikana kwa Jumuiya na ni mambo gani muhimu yalikosa maamuzi au utekelezaji kwa kipindi hicho?

**NAIBU SPIKA:** Nilifikiri ungeongeza kwamba je, itakuwa hata miaka mitano itaishia wapi? *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli muda ni rasilimali na kitendo cha kuelewa kuapishwa kwa njia moja au nyingine yako mambo yaliyochelewa kufanyiwa maamuzi, lakini kwa kutumia taratibu na mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na kutumia Baraza la Mawaziri la Afrika Mashariki shughuli zote za Jumuiya ziliendelea na baada ya Bunge kuwa limeenza sasa mambo yanaendelea kama kawaida.

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba kuongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kuhusu lini Bunge hili linaisha baada ya kuapishwa mwezi Juni. Muda wa Bunge lile unaanza tarehe ile waliyoapishwa mpaka miaka mitano baadaye. Kwa hiyo, miezi sita iliyopotea huko nyuma kabla ya Bunge halijaanza limechukuliwa katika mfumo huo.

La pili, niseme tu kwamba Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya mambo ambayo yalicheleweshwa katika kushughulikiwa wakati ambapo Bunge halikukaa ni kupitishwa Miswada mbalimbali ambayo napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba sasa hivi Bunge hilo la Afrika Mashariki limekaa na limepitisha Miswada mbalimbali mojawapo ukiwa masuala ya Usafiri na Mazingira katika Ziwa Victoria.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa kunijibu mie Naibu Spika. Tunaendelea Waheshimiwa kwa sababu Bunge lipo, na Spika wake nimemtangaza. Kwa hiyo tungoje lifanye kazi vizuri kadri inavyostahili. Tunaenda Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Na. 34

## Uhamishaji wa Askari/Maafisa wa JWTZ

**MHE. MARTHA M. MLATA** aliuliza:-

Kwa kuwa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) lina utaratibu wa kuwahamisha askari/afisa kutoka kikosi kimoja kwenda kingine:-

(a) Je, utaratibu huo ni wa kisheria na askari/afisa hao anatakiwa akae katika kikosi kwa muda gani?

(b) Je, ni askari/afisa wangapi hadi hii leo wamekaa katika kikosi kimoja kwa zaidi ya miaka mitano?

(c) Je, ni sababu zipi zinazofanya askari/afisa hao kukaa muda mrefu katika kikosi kimoja?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Martha Mlata, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Majeshi ya Ulinzi *(DFC)* ambayo ipo kisheria, imetoa mamlaka kwa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi kuunda vikosi na kuhamisha wanajeshi kutoka sehemu moja kwenda nyingine. Hata hivyo, katika utaratibu huo, hakuna muda maalumu uliowekwa kwa wanajeshi kukaa kwenye kikosi kimoja.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa utaratibu wa kuwahamisha mafisa na askari kila baada ya miaka mitano haumo ndani ya sheria na kanuni za jeshi la Ulinzi, ni dhahiri kwamba idadi anayoitaka Mheshimiwa Mbunge itakuwa vigumu kupatikana. Uhamisho kwa wanajeshi hutolewa pale tu yanapotokea mahitaji. Mfano mzuri ni kwa askari na maafisa walioko katika baadhi ya vikosi vya ufundi na taaluma mbalimbali kwa kawaida hukaa katika vikosi hivyo hadi watakapostaafu. Hii ni kutokana na hali ya majukumu yao ya kazi.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyokwisha jibu katika kipengele (b) hapo juu kwamba hakuna utaratibu ndani ya sheria unaoelezea muda wa askari kukaa katika kituo kimoja. Askari anapomaliza mafunzo yake ya awali ya kijeshi hupangiwa kikosi cha kufanyia kazi ambako atakwenda kupatiwa taaluma husika ndani ya kikosi alichopangiwa.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba hakuna muda maalum wa kuwahamisha wanajeshi hao. Sasa mimi napenda kuuliza wanajeshi waliopo katika kambi za mipaka ya nchi yetu. Je, haoni kwamba kwa kuwaacha wanajeshi hawa

wakakaa kwa muda mrefu katika mipaka ya nchi yetu wanaweza wakajihusisha na vitendo vya uhalifu hata kuachia mianya ya kuweza kuingiza maharamia ndani ya nchi yetu?

Swali la pili. Je, kuna utaratibu gani hasa kwa wanawake wanajeshi wanapoolewa kupatiwa uhamisho? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika mpaka yetu ya Tanzania hatuna kambi za jeshi isipokuwa tuna *detouch* viteule. Wanajeshi wanaopelekwa katika viteule hukaa kwa muda wa miezi mitatu mpaka sita ili baadaye tuwabadilishe na kuwapeleka wanajeshi wengine kwa tahadhari hizo ambazo Mheshimiwa Mbunge amezieleza.

Pili, Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba ndani ya jeshi hatuna askari wa kike, hatuna askari wa kiume. Ndani ya jeshi tuna askari na afisa. Ni askari na afisa kwa maana hiyo, askari anapoolewa upo utaratibu wa kisheria unafanywa ili kumwezesha kuweza kuishi na familia yake. Lakini inapotokea askari yule akawa ni mtaalam katika kikosi fulani nikitoa mfano kikosi cha ndege kama yeye ni rubani, na ameolewa katika Mkoa ambao hauna kikosi cha ndege, askari yule atalazimika kubakia katika kikosi kile na utaratibu unaotakiwa ufanywe ni yeye mwenyewe kumwezesha mumewe kumfuata katika kikosi kile. *(Kicheko/Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Haya, kwa kuzingatia jenda, Mheshimiwa Faida Bakar.

**MHE. FAIDA M. BAKAR:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa mara nyingi kunajitokeza tabia ya ucheleweshaji wa malipo kwa askari wetu wanaohamishwa kutoka sehemu moja kwenda nyingine. Je, Serikali haioni kuwa huko ni kuwapunguzia ari ya kufanya kazi askari wetu?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kesi ambazo amezielezea zipo, lakini siyo nyingi na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kupitia Makao Makuu ya Jeshi tunajitahidi sasa kuondokana na matatizo hayo ili kumpunguzia askari huyo ambaye anahamishwa matatizo.

Na. 35

**Utafiti wa Magonjwa hatari**

**MHE. FATMA MUSSA MAGHIMBI** aliuliza:-

Kwa kuwa maradhi yaliyowahi kuangamiza maisha ya Watanzania wengi na hivi sasa yamepotea, mfano *Black Water Fever, Smallpox, Ebola* na kadhalika:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa kuna haja ya kuanzisha kitengo maalum cha kufanya utafiti wa magonjwa hayo na kujiweka tayari endapo yatatokea tena ili tusipoteze maisha ya watu wengi kama ilivyotokea kwa Homa ya Bonde la Ufa?

(b) Je, Serikali imewahi kufanya utafiti wa magonjwa hayo ili kujua yanatokana na nini na hujitokeza baada ya miaka mingapi?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Mussa Maghimbi, Mbunge wa Chake Chake, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua na kuthamini umuhimu wa utafiti na uchunguzi wa magonjwa ya binadamu. Hii ndiyo sababu ya kuanzishwa kwa Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu *(National Institute for Medical Research)* mwaka 1979. Taasisi hii hufanya utafiti na uchunguzi wa magonjwa mbalimbali na matokeo yake huisaidia Serikali kuandaa mikakati mbalimbali ya utekelezaji. Lengo ni kuhakikisha upatikanaji wa huduma za afya zilizo bora na endelevu.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kitaalam, *black water fever* ni dalili ya malaria kali ambayo huambatana na kuathirika kwa mishipa ya damu na figo na hivyo kusababisha kukojoa mkojo mweusi. Hata hivyo, kutokana na kuwepo kwa tiba na dawa bora za malaria hapa nchini na kuongezeka kiwango cha uelewa wa jamii kuhusu ugonjwa huu, dalili hii ya mkojo mweusi *(black water)* kwa sasa haijitokezi kabisa kwa wagonjwa wa malaria.

Ugonjwa wa ndui *(Small pox)* uliwahi kuwepo nchini na baadaye kutokomezwa kabisa. Hata hivyo, bado Wizara yangu inaendelea kufuatilia kwa karibu matukio yote yanayoashiria kuwepo kwa ndui kupitia mpango wa chanjo ya watoto. Mpaka sasa sampuli zote zilizofanyiwa uchunguzi wa ndui hazionyeshi kuwepo kwa vimelea vya ugonjwa huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu haijawahi kupata tukio lolote la ugonjwa wa Ebola. Hata hivyo, kwa kuwa ugonjwa huu umekuwa tishio katika nchi za jirani, Wizara yangu kupitia Kitengo cha Maafa *(Emergency Preparedness and Response Unit)* imepeleka wataalam katika mikoa yote ya mipakani yaani Kigoma, Rukwa, Mara, Mwanza na Arusha ili kutoa elimu kwa umma kuhusu ugonjwa huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Taasisi ya utafiti wa magonjwa inaendelea na utafiti wa mafua makali na mafua ya ndege kwa kushirikiana na Hospitali ya Taifa Muhimbili. Hospitali ya Manispaa ya Mwananyamala na Hospitali ya Haydom – Mbulu. *(Makofi)*

Aidha, Wizara imeanzisha maabara mpya ya virolojia ili kuipa taasisi uwezo wa kufanya uchunguzi wa magonjwa mengine yanayosababishwa na virusi hapa nchini.

**MHE. FATMA MUSSA MAGHIMBI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika. Kwa kuwa magonjwa yaliyotajwa ni magonjwa maangamizi. Je, Wizara imeshatayarisha chanjo ya magonjwa kama ebola ambayo hamna dalili na magonjwa ya Bonde la Ufa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara mpaka sasa hivi haijaandaa chanjo yoyote kwa magonjwa aliyoyataja lakini kama nilivyosema katika jibu langu la msingi Wizara inafuatilia kwa karibu magonjwa yote haya ambayo wanasema ni angamizi ili kuhakikisha kwamba yanadhibitiwa na kuchukuliwa tahadhari iwapo yatajitokeza.

Na. 36

**Samaki watokao Afrika Kusini**

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH** aliuliza:-

Kwa kuwa kuna samaki aina ya vibua wanatoka Afrika Kusini na kuingizwa hapa nchini na kwa kuwa inasemekana kuwa samaki hao huhifadhiwa kwa kutumia dawa ya kuhifadhia maiti ili wasiharibike haraka na hivyo kusababisha athari za kiafya kwa watumiaji kwa kusababisha magonjwa kama ya kansa na kadhalika.

(a) Je, Serikali inalifahamu hilo?

(b) Kama inalifahamu. Je, imechukua hatua gani za kuwadhibiti waletaji wa samaki hao?

(c) Je, Serikali inachukua hatua gani za kuhakikisha walaji hawahatarishi maisha yao?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mbunge wa Viti Maalum, lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara ya kwanza Serikali ilipata taarifa ya kuwa kuna samaki kutoka ndani na nje ya nchi wanaohifadhiwa na dawa ya kuhifadhia maiti *(Formalin)* kupitia taarifa zilizoripotiwa na vyombo vya habari mwezi Juni, 2006.

Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Chakula na Dwa ilifanya uchunguzi wa kimaabara kwa sampuni zote za samaki zilizodaiwa kuhifadhiwa kwa *formalin* matokeo ya uchunguzi huo yalionyesha kuwa hakukuwa na kemikali zozote za *formulin* katika sampuni hizo. Tarehe 17 Julai, 2006 Wizara ilitoa taarifa ya matokeo ya uchunguzi huo kwa Umma kwenye magazeti.

Taarifa nyingine ya kuwepo kwa samaki wanaohifadhiwa kwa *formalin* nchini iliripotiwa na vyombo mbalimbali vya habari m wezi Aprili 2007. Wizara yangu kwa mara nyingine tena ilifanya uchunguzi katika awamu hii Mamlaka ya Chakula na Dawa ilifanya uchunguzi kwa kushirikiana na Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Wizara ya Mali Asili – Kitengo cha Uvuvi na Maafisa Afya wa Mikoa.

Aidha, sampuli zilizochukuliwa katika vituo mbalimbali vya kuuzia samaki na sehemu ambako samaki hugandishwa kabla kusafirishwa. Matokeo ya uchunguzi huu pia, yalionyesha kuwa hakukuwa na kemikali zozote za *formalin* katika samaki hao. Taarifa kwa umma kuhusu matokeo ya uchunguzi huo ilitolewa tarehe 17 Mei, 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge pamoja na Bunge lako Tukufu kuwa si rahisi kwa dawa ya kuhifadhia maiti kutumika kuhifadhia samaki au vyakula vingine. Hii ni kwa sababu dawa hiyo ina harufu kali sana ambayo hata kama ikioshwa haiwezi kwisha. Hata hivyo, kibiashara matumizi ya dawa hii kwa ajili ya kuhifadhia samaki hayana faida kwa kuwa gharama yake ni kubwa sana hali ambayo ingewalazimu wafanya biashara kuwauza kwa bei kubwa sana ili kupata fedha.

**MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA:** Ahsante sana nakushukuru Naibu Spika kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Kwa sababu tatizo la kutangaza vibaya uhifadhi wa samaki uliathiri wavuvi na mapato yao. Je, ni nani atawafidia wavuvi hawa ambao wamepoteza soko kwa muda mrefu kwa sababu ya matangazo ya uzushi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri hata Waziri mwingine wa Biashara au nini kama uzushi ulikuwepo.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa kama alivyodai yeye mwenyewe kwamba imetolewa ya uzushi sisi kama Wizara taarifa tuliletewa katika vyombo vya habari tumetoa ule ukweli na kwamba haikutumika *formalin* katika kuhifadhi hizi samaki. Sasa kama kuna fidia yoyote ambayo ilitaka kulipwa basi nadhani hiyo itakuwa ni wale waliotoa taarifa na wale waliopata athari wawashitaki wale ambao wametoa taarifa za uzushi ili waweze kuchukuliwa hatua. Lakini Serikali haitawajibika kulipa fidia kwa sababu uzushi haukutolewa na Serikali bali uzushi ulitolewa na waliotoa hizo habari. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nimemwita Mheshimiwa Mongella kwa sababu yeye anatoka Visiwani na samaki ndiyo wako huko.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Spika kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Pia nashukuru kwamba Naibu Waziri amejibu vizuri sana masuala mbalimbali yanayohusiana na uhifadhi wa samaki. Sasa kwa kuwa kisayansi uhifadhi nzuri wa samaki unatokana na kipindi wanavyowekwa samaki hawa katika majokofu ama kwa kutumia barafu na sasa hivi mashine za namna hii zipo sehemu nyingi sana nchini na ndiyo zimetuwezesha kusafirisha nje samaki kwa mauzo na kadhalika.

Sasa kutokana na hali hii iliyopo sasa hivi nchini. Je Serikali haioni wakati umefika sasa wa kupiga marufuku uingizaji wa samaki kutoka nchi nyingine yoyote zaidi ya Tanzania kwa sababu uwezo tunao na samaki tunao wengi kwa hivi sasa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mrope basi kwa heshima tu, hili swali liko nje kabisa ya lile *original*. Lakini kwa sababu Naibu Waziri, kwanza ni samaki. Lile la kwanza lilikuwa linazungumzia madawa kwenye samaki. Sasa hili ni kuingiza samaki, kidogo liko nje. Labda Waziri kama anaweza lakini Waziri wa Afya siyo swali lake. Waziri wa Viwanda au nini? Waziri wa Viwanda na Biashara.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli ni kwamba Tanzania tunajitosheleza kabisa kwa samaki kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge na kwamba tunauza samaki nje na samaki wetu wana ubora unaokubalika kimataifa na ndiyo maana tunauza Japan, tunauza Jumuiya ya Ulaya kwa kutumia maabara ambazo tumejenga sisi wenyewe na mwaka huu imezinduliwa maabara ya kimataifa kwa kazi hiyo kule Mwanza.

Kwa hiyo, kama kuna samaki wanaoingia nchini hao lazima wawe wachache sana sina habari nao lakini niko tayari kupata habari za Mheshimiwa Mbunge na kuzichunguza kwa sababu hatuhitaji samaki kutoka nje. Samaki wa kwetu ni wazuri na bora kwa kila hali. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ni kwa sababu ya Muswada wa juzi wa *Anti-Dumping* ndiyo maana nimeruhusu swali hili lijibiwe. Maana yake unaweza kununua samaki waliooza tu, afadhali wanunue samaki wa kwetu.

Na. 37

## Tatizo la Ukeketaji nchini

**MHE. MOHAMED ALI SAID** aliuliza:-

Kwa kuwa ukeketaji ni ukatili mkubwa sana wa kijinsia na kwa kuwa, vitendo hivyo vimeenea nchini kote hususan katika Mikoa ya Manyara 80%, Dodoma 68%, 55%, 46% na Mara 37%:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa sasa ni wakati muafaka wa kutunga sheria itakayotokomeza kabisa ukatili huo?

(b) Kwa kuwa, suala hilo ni nyeti. Je Serikali inaweza kuleta mapema Bungeni Muswada kabla ya mwaka 2009?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Ali Said, Mbunge wa Mgogoni Pemba, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mohamed Ali Said, kwamba ukeketaji ni ukatili mkubwa sana wa kijinsia na kwamba vitendo hivyo vya ukeketaji vimeenea sehemu mbalimbali hapa nchini. Katika kukabiliana na ukatili huo wa kijinsia, Serikali kupitia Bunge lako Tukufu lilitunga na kupitisha Sheria Namba 4 ya Mwaka 1998 ambayo inakataza ukeketaji na kuweka adhabu kali kwa wale wanaobainika kujihusisha na vitendo hivyo.

Sheria hiyo inarekebisha Sheria ya Kanuni ya Adhabu – Sura 16 ya Sheria. Kwa mujibu wa Kifungu 169A cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu kama ilivyorekebishwa na Sheria hiyo Namba 4 ya mwaka 1998 ni kosa la jinai kwa mtu yeyote kukeketa au kusabaisha kukeketwa kwa mtoto aliye na umri ambao ni chini ya miaka 18.

Mtu yeyote akibainika na kutiwa hatiani kwa kosa hilo atahukumiwa kwenda jela kwa muda usiopoungua miaka mitano na usiozidi miaka kumi na tano, au atalipa faini isiyozidi shilingi laki tatu (300,000/=) au atalipa faini pamoja na kwenda jela kwa muda huo. Vile vile mtu huyo atalipa fidia kwa kiasi kitakachopangwa na Mahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, mila hii ya ukeketaji ni kongwe katika jamii yetu kwa kuwa imekuwepo kwa muda mrefu hivyo adhabu kali pekee haiwezi kuwa ndio suluhisho.

Waheshimiwa Wabunge, wengi wenu mtakubaliana nami kwamba pamoja na kuwepo adhabu kali katika Sheria zetu bado ukeketaji unaendelea katika jamii yetu na baadhi ya watu bado hawaogopi kukeketa. Hata wale waathirika wa mila hii potofu wamekuwa mstari wa mbele katika kukwepa kutoa ushahidi wanapohitajika kufanya hivyo. Wamendelea kutafuta njia mbadala za kukeketa na kufikia hatua ya kukeketa hata watoto wachanga ambao hawawezi kusema.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni wakati muafaka kwa sisi Wabunge, Serikali na Taasisi zisizo za kiserikali kuongeza jitihada zetu katika kuwaelimisha wale waumini wa mila hii potofu ili iweze kutokemezwa kabisa katika jamii yetu.

Ni pale tu jamii yetu itakapoelewa upotofu wa mila hii ndipo itakapotoweka. Wakati elimu hii ikiendelea kutolewa, Serikali itaendelea kuimarisha vyombo vyake vya Sheria ili kuendelea kukabiliana kwa nguvu zote na tatizo hili.

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika. Kwa kuwa ukeketaji unapingwa na ni kilio cha watu wengi hapa Tanzania na hata Bara la Afrika na kwa kuwa Serikali haishindwi na jambo lolote pindi inapoamua kulikomesha na kwa kuwa wakeketaji ni wahalifu kama wahalifu wengine, ningependa kujua haswa kikwazo kikubwa ni nini ambacho kinashindwa kuwakomesha watu hawa ikiwa asilimia kubwa ya wananchi hawalipendi na wanaolipenda ni wachache? Ahsante Mheshimiwa Nai9bu Spika.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa katika kutokomeza mila hii ni kwamba ni mila iliyojikita katika jamii yetu kwa muda mrefu sana. Katika jamii zingine kitendo hiki kinaonekana kuwa ni sifa nzuri.

Kwa hiyo, sasa kukiondoa inabidi ichukue muda vile vile. Tunajaribu kujenga, kuelimisha wananchi ili waelewe kwamba mila hii si nzuri. Lakini kama nilivyosema inachukua muda kwa sababu imejitikiza ndani ya jamii na katika sehemu zingine kama nilivyosema ni sehemu nzuri kukeketa ama kukeketwa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu nina watu wengi, basi tunaingia katika Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana. Sasa namwita Mheshimiwa Mahenge kama mnavyofahamu Mheshimiwa Yono amefiwa na watoto wake wawili katika kipindi kifupi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mahenge atauliza swali kwa niaba yake. Baada ya majibu ya Waziri tutarudi swali la 38.

Na. 39

**Mkopo wa Shilingi Bilioni Moja kwa Kila Mkoa**

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE (K.n.y. MHE. YONO S. KEVELA)** aliuliza:-

Kwa kuwa fedha ya mkopo wa shilingi bilioni moja kwa kila mkoa imekwishatolewa kama Mheshimiwa Rais alivyoahidi na wananchi wengi hasa wajasiriamali wameipata:-

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha kimetolewa kwa Wilaya ya Njombe?

(b) Je, ni wananchi wangapi waliopata mikopo hiyo kwenye Jimbo la Njombe Magharibi, yaani tarafa ya Mdandu, imalinyi na Wanging’ombe?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. DR. EMMANUEL J. NCHIMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Yono Stanley Kevela, Mbunge wa Njombe Magharibi, kama ifuatavyo;

Ni kweli kwamba Serikali katika mwaka wa fedha 2006/2007 ilitenga kiasi cha fedha shilingi bilioni 21 wastani wa shilingi bilioni moja kila mkoa.

Nusu ya fedha hizo Shs. 10.5bn/= zilitumika kama dhamana ya mikopo kwa wajasiriamali kupitia Benki za *CRDB* na *NMB* ambazo zilitumia fedha hizo kiasi mara tatu ya fedha za dhamana katika kutoa mikopo kwa wajasiriamali.

Nusu iliyobaki imepangwa kutolewa katika mwaka huu 2007/2008 kupitia Taasisi ndogo ndogo za fedha. Hadi mwezi Septemba, jumla ya shilingi bilioni 29.095,800/= tayari zimekwisha kopeshwa kwa Wajasiriamali 35,398 zilizotolewa na Benki za *CRDB* na *NMB.*

Mheshimiwa Naibu wa Spika, baada ya maelezo hayo sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Yono Stanley Kevela, Mbunge wa Njombe Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Njombe imepata jumla ya mikopo yenye thamani ya shilingi milioni 119,681,500/= iliyotolewa na *NMB* kwa wajasiriamali 82, na Benki ya *CRDB* imetoa kiasi cha mikopo yenye thamani ya shilingi milioni 50,000,000/= kwa *IFANYA SACCOS* iliyoko Njombe, yenye wanachama 28 ambao wote ni Wanawake.

Hivyo Benki hizi mbili zimetoa mikopo kwa Wilaya ya Njombe kwa wajasiriamali 110 yenye thamani ya jumla ya Shilingi milioni 169,681,500/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mpango wa Taifa wa uwezeshaji wananchi kiuchumi inatolewa ki-wilaya na si ki-majimbo inakuwa vigumu kupata takwimu zinazoonesha idadi ya mikopo iliyotolewa katika jimbo la Njombe Magharibi, yaani tarafa za Mdandu, Imalinyi na Wanying’ombe.

Aidha nawashauri Waheshimiwa Wabunge wanaotaka kujua kiasi cha fedha zilizotolewa katika Majimbo yao wawasiliane na Ofisi za Waratibu wa mikopo hii. Kila Halmashauri yupo Afisa anaye fuatilia mikopo hii kwa maana ya kuweka kumbukumbu kwa walengwa walionufaika na mikopo hii na maendeleo ya miradi yao.

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Nashukuru sana kwa majibu aliyoyatoa Naibu Waziri. Naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa, katika mikopo hii ya wajasiriamali, ni wajasiriamali 14 tu katika Wilaya ya Makete walioweza kupata mikopo yenye jumla ya thamani milioni 12 tu, kiwango ambacho ni kidogo na idadi ndogo ya waliopewa hiyo mikopo iliyotokana na Ofisi Kuu kusimamisha kupokea maombi ya wajasiriamali katika wilaya ya Makete. *(Makofi)*

(a) Je, serikali itachukua hatua gani za dharura kuwasaidia wananchi hao wa Makete ili nao waweze kupata maisha bora?

(b) Kwa kuwa katika wilaya ya Makete ni *SACCOS* sita zilizokuwa zimeomba mikopo hii ya wajasiriamali yenye thamani ya milioni 600. lakini hivi ninavyoongea hakuna *SACCOS* hata moja iliyopata mikopo hii kwa sababu tu wakaguzi wa mahesabu walioko Iringa kwa kukosa uzalendo walishindwa kufika Makete na kukagua mahesabu ya *SACCOS* hizi, na hivyo kufanya watu hawa wasipate mikopo na hivyo kushindwa kuondoa umasikini. Je, serikali pia hapa itachukua hatua gani za dharura kuwasaidia wananchi hawa wa Makete? Asante sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. DR. EMMANUEL J. NCHIMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mahenge, yenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo :-

Kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Mahenge kwa utafiti wake wa kuweza kujua kiwango cha watu waliokopeshwa na kiasi gani wamepata. Hii inaonesha alivyo karibu na wananchi wake.

Pili naomba kumhakikishia kwamba si wote ambao hawajapata mikopo maana yake ni kwamba wamekosa. Utaratibu wa Benki unaendelea vizuri katika Benki zote, watu wengine wenye sifa wanaendelea kuratibiwa na mikataba iko tayari wanasubiri tu marejesho ya watu wengine waliomalizika, ikimalizika ndio nao wachukuliwe. Lakini pia utaratibu wa pili ambao tunauandaa ambao ni wa awamu ya pili utazingatia pia waombaji hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kusema wale walioomba katika *SACCOS* sita na ambao ametuambia kwamba hawajapata mikopo kwasababu wakaguzi hawajaenda kuwakagua. Kwa kuwa wakaguzi hawa wanahusika na Serikali nitumie nafasi hii kuwaagiza huko waliko waende mara moja kufanya ukaguzi na hatuwezi kutoa maelekezo kwamba wapewe mikopo bila kukaguliwa. Wakaguliwe mara moja na tupate taarifa kupitia Wizara ya Ushirika na Masoko mapema inavyowezekana.

**MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa fedha hii inaitwa kwa jina la *JK* iliahidiwa pia kufika Zanzibar. Kwa hiyo ni lini zitafika fedha hizo?

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Soud Mbunge wa Jang'ombe kama ifuatavyo:-

Ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba fedha hizi zilikuwa zifike Zanzibar. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba fedha hizi, milioni 600 zimeshafika Zanzibar. Na Rais wa Zanzibar naye ametoa shilingi vile vile milioni 600 kwahiyo kuna shilingi bilioni 1 na milioni 200 na utaratibu wa kuanza kuzikopesha kwa taarifa tulizozipata umekwisha andaliwa, kwahiyo wakati wowote mikopo itaanza kutolewa Zanzibar *(Makofi)*.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Waheshimiwa, kwaajili ya muda tunaendelea na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Nilikuwa imenipa tabu kwasababu Waziri mgonjwa, Naibu Waziri ndio huyo, kwahiyo imenipa shida kidogo.

Mheshimiwa, Mheshimiwa Lucy Sawere Nkya, atauliza swali hili. Mheshimiwa Lucy ndiye anauliza swali.

Na. 38

**Watoto Wanaoishi Kwenye Mazingira Magumu**

**MHE. DR. LUCY S. NKYA** aliuliza:-

Kwa kuwa idadi ya watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu hususan kwenye miji mikubwa ya Tanzania wengi wa watoto hao hawapati malezi bora na elimu:-

(a) Je, Serikali inafahamu idadi ya watoto wanaoishi mitaani katika sehemu za miji mikubwa?

(b) Je, Serikali inayo mipango gani kwa kuzuia wimbi la watoto kuingia mitaani?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA K.n.y. WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Lucy Sawere Nkya, Mbunge Viti Maalumu, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inafahamu kwamba kuna watoto wanaoishi katika mazingira magumu katika sehemu za miji mikubwa. Hadi sasa Serikali haijafanya utafiti ili kupata idadi kamili ya watoto wanaoishi mitaani katika sehemu za miji mikubwa ya nchi yetu na hivyo haina idadi kamili ya watoto hao.

Wizara yangu inayo nia ya dhati kabisa ya kufanya utafiti ili kufahamu idadi na kupata taarifa zaidi kuhusu watoto wanaoishi mitaani, lakini jitihada hizi zinakwamishwa na ufinyu wa Bajeti unaoikabili Wizara yangu. Hata hivyo, Wizara inaendelea na jitihada za kutafuta vyanzo vingine vya fedha kutoka mashirika ya kimataifa kama vile *UNICEF* ili kufanya utafiti wa kina na hatimaye kupata idadi ya watoto wanaoishi mitaani na yatima.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika (b). Serikali inayo mipango ifuatayo ili kuzuia wimbi la watoto kuingia na kuishi mitaani:-

Wizara yangu inaendelea kutoa mafunzo kwa awamu kwa Wataalam wa Maendeleo ya Jamii walioko katika Wilaya zote nchini ili wayafikishe mafunzo hayo kwa wananchi na wazielewe haki za watoto na hatimaye wawe na uelewa wa kutosha wa kudhibiti ongezeko la watoto kukimbilia kwenda kuishi kwenye miji mikuu na midogo.

Aidha, Serikali ina mpango wa kuunda Kamati mbalimbali katika ngazi za vijiji na mitaa ili kuwatambua na kuwahudumia watoto yatima wanaoishi katika mazingira hatarishi wakiwemo watoto wa mitaani kupitia mifuko ya fedha itakayoanzishwa na jamii katika maeneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu pia imebuni mfuko maalum *(OVC)* yaani *Ofans and Vulnerable Children Trust Fund* ambao utakuwa na lengo la kuwasaidia watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi. Mfuko huo bado uko katika hatua za awali za maandalizi. Na utakapoanza utaweza kuboresha huduma za mafunzo na malezi ya watoto walio katika mazingira hatarishi, yatima na wanaoishi mitaani.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la kudhibiti tatizo la watoto wa mitaani si la Serikali peke yake, bali ni jukumu la jamii pia. Watoto hawa wametoka katika familia zetu hivyo tuna wajibu wa kuwalea watoto hawa na kuwapatia haki zao zote za msingi. Tutaendelea kutoa elimu na kuhamasisha jamii ili kutambua wajibu tulionao kwa kuwapatia malezi bora watoto tuliowazaa.

**MHE. DR. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na nina mpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini ningependa kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa, kuna watoto wanotumiwa na watu wazima wenye afya zao kuwazungusha mitaani kuwasaidia katika shughuli za omba omba. Na kwa kuwa hao watoto wana umri wa kwenda shule na hawajapata fursa ya kwenda shule. Je, Serikali ina mikakati gani ya kuhakikisha kwamba inakomesha hii tabia ya watu wazima kutumia watoto kwenye omba omba na kuwanyima fursa ya kwenda shule ili hao watoto waweze kwenda shule?

Kwa kuwa katika wilaya zetu na mikoa tuna Maofisa Maendeleo ya Jamii tuna na Maofisa wa Ustawi wa Jamii. Nafahamu kwamba kati ya majukumu yao jukumu kubwa

ni kufuatilia haki za watoto, kuangalia kwamba watoto wanapata huduma zinazostahili. Sasa basi, hawa wote wako katika wilaya zetu na wanaona watoto wnatembea mitaani na wanaomba na wako maofisini hawachukui hatua yoyote. Je, Serikali inasema nini kuhusu hili?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA K.n.y. WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dokta Nkya kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba wako omba omba ambao wanzunguka na watoto mitaani na kuwatumia kujipatia fedha. Naomba tu nitoe rai kwamba hivi sasa ni wakati wa kuandikishwa wanafunzi kwenda shule kwa ajili ya darasa la kwanza umefika na kwamba Maafisa Maendeleo ya Jamii kwa kushirikiana na Waratibu Elimu Kata, wawaelekeze watoto hao kwenda kuandikishwa shuleni. Na wale ambao watakuwa wameshapita umri wa kuandikishwa, ina maana watakuwa wameingia katika hatua ya *MEMKWA* kwasababu watakuwa wamepita umri wa darasa la kwanza au la pili na la tatu. Lakini Serikali kwa kushirikiana na Wizra ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi inao mpango.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa wito na hasa kwa wale ombaomba ambao wanazunguka na watoto, kwamba ni haki yao ya msingi wale watoto wao ni kusoma na ya kwamba wawarudishe majumbani wakaandikishwe waende shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili kwamba Maafisa Maendeleo ya Jamii na Ustawi wa Jamii wapo katika sehemu tunazoishi na wanawaona hawa watoto. Naomba niseme tu kwamba Maafisa Hawa wana uwezo tu wa kutekeleza majukumu yao pale ambapo watapata ushirikiano. Hivyo naomba sote kwa pamoja tukiwa kama sehemu ya jamii, tushirikiane kuwasaidia hawa watoto wapate elimu. Naomba niseme suala hili litawezekana endapo sote tutashirikiana na wale wazazi wanaotoka kuzunguka kuomba na watoto, wawarudishe.

Na. 40

**Mikopo kwa Wakulima Vijijini ili Kuendeleza Kilimo**

**MHE. JAMES P. MUSALIKA** aliuliza**:-**

Kwa kuwa kilimo bado ndicho uti wa mgongo wa Taifa ambapo asilimia 80 (80%) ya Watanzania hutegemea kilimo kuendesha maisha yao, na kwa kuwa kilimo vijijini bado ni duni ambapo hakuna zana za kisasa, pembejeo na mitaji haba:-

(a) Je, Serikali iko tayari kuzisukuma Taasisi, asasi na Mifuko ya Fedha kutoa mikopo vijijini hususan kwenye maeneo yanayolima mazao ya biashara kama Pamba, Korosho na Kahawa badala ya mikopo hiyo kulenga maeneo ya mijini tu?

(b) Je, Serikali itawasaidia vipi Wajasiriamali wenye miradi ya kilimo cha Pamba, Dengu, Mpunga, Mahindi na bustani wa Kata za Busolwa, Kharumwa na Nyang'hwale ambao Benki ya *NMB* imekataa kuwapa mikopo; na wale wa *SACCOS* ya Kata ya Bukwimba na Mwingiro ambao Benki ya *CRDB* inasita kuwapa mikopo?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. DR. EMMANUEL J. NCHIMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, naomba kujibu swali la Mheshimiwa James Musalika, Mbunge wa Nyang'hwale, kama ifuatavyo:-

Katika kuanzisha mpango wa uwezeshaji wananchi kiuchumi na kukuza ajira, Serikali imeweka kipaumbele katika kuinua hali ya wananchi kupitia miradi ya uzalishaji kama vile kilimo, ufugaji, viwanda vidogo vya usindikaji mazao na kadhalika. Ili kufanikisha mpango huu Serikali iliandaa mkakati wa kufikisha fedha za uwezeshaji kupitia njia ya mikopo nafuu kwa wajasiriamali wadogo walio mijini na vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa mkakati huo, Serikali ilitenga bilioni 21 ambazo zimetolewa awamu mbili. Awamu ya kwanza ya mwaka 2006/2007 ambapo shilingi bilioni 10.5 zilitolewa kama dhamana kwa benki za *CRDB* na *NMB*.

Awamu ya pili ni mwaka huu 2007/2008 ambapo shilingi bilioni 10.5 zitatolewa kwa Asasi ndogo ndogo za fedha ili ziwakopeshe walengwa hasa wale wa vijijini ambao awamu ya kwanza haikuwafikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa James P. Musalika, Mbunge wa Nyang'hwale lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu wa Spika, katika awamu ya pili ya utekelezaji wa mpango wa utoaji mikopo kwa wananchi ua wajasiriamali, Serikali kwa kupitia Benki Kuu ya Tanzania imeandaa utaratibu wa kutumia Asasi ndogo ndogo zenye uwezo na uzoefu wa kutoa mikopo kwa wananchi waishio vijijini ambako Benki za kawaida hazikuweza kuwafikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Asasi zilizoteuliwa na Benki Kuu kushiriki katika utekelezaji wa kutoa mikopo kwa wananchi vijijini na maeneo mengine ambayo hayana huduma za kibenki ni pamoja na hizi zifuatazo:-

Benki ya Posta, *Pride Tanzania, SEDA, Akiba Commercial Bank, Presidential Trust Fund, Mufindi Community Bank, Mwanga Community Bank, Mbinga Community Bank, Kagera Farmers Cooperative Bank, Azania Bank, SCCULT,* na *Dunduliza Cooperative.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Watendaji wa Asasi hizi hivi sasa wanapewa mafunzo na Benki Kuu, na baada ya hapo watawekeana mkataba (*MOU)* ambao utaeleza masharti ya mikopo hii na maeneo ambako kila Asasi itakwenda kutoa huduma. Lengo ni kuhakikisha kila Wilaya na kila Jimbo linafikiwa katika awamu hii ya pili. Hii ni pamoja na maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge ya kata za Busolwa, Kharumwa na Nyang'hwale. Mikopo hii itatolewa kwa kuzingatia kipaumbele kwa *SACCOS* na vikundi vya uzalishaji.

Ni matumaini yetu kwamba mpango huu utaanza wakati wowote kuanzia sasa mara tu Benki Kuu ikikamilisha kuziandaa Asasi hizi.

Napenda kutoa wito kwa Viongozi wa Wilaya na Watendaji katika maeneo ya Tarafa na Kata kutoa ushirikiano kwa Asasi hizi mara zitakapoanza kutoa mikopo huko vijijini. Ni muhimu pia kuwasaidia wajasiriamali wabuni miradi ya uzalishaji hasa kilimo, ufugaji, viwanda vya kusindika mazao na kadhalika. ili kukuza uchumi na kuongeza ajira ambayo ndiyo madhumuni ya mpango huu.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Namshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa, jibu la Mheshimiwa Naibu Waziri anasema sasa hivi hawa ambao, Asasi ambazo zimeteuliwa kutoa mikopo huko vijijini wako kwenye semina inayotolewa na Benki Kuu na baadaye waingie kwenye uandikaji wa *Memorandum*. Lakini kwa kuwa wakati huo huo sasahivi kilimo hiki cha pamba na mahindi kinafuata msimu na msimu ni sasahivi. Sasa hivi wakulima wanahitaji mkopo kununua pembejeo, kulima mashamba, kununua zana za kilimo.

Je, Serikali haioni kwamba itarudia makosa hayo yaliyofanyika mwaka jana, ambapo baadae pesa itakuwa tayari kuanzia mwezi wa pili, wa tatu mwaka kesho. Kwa hiyo, na kuwanyima haki hawa ambao wanataka kukopa?

La pili, kwa kuwa Serikali ina mtindo wa kujali sana wachuuzi wa mjini na kuwasahau wakulima ambao wangeweza kuzalisha na kuongeza pato la nje fedha za kigeni na badala yake kuwajali sana hawa wachuuzi ambao wanatuletea hata vifaa *fake* kama vile nyaya za umeme. Je, Serikali inaweza kuwa, kwa kuanzia pesa hizi za *JK* za awamu hii zote kabisa ziende kwa wakulima wa pamba, wa dengu, wa korosho, ili baadaye ziongeze pato la Taifa kwa fedha za kigeni?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. DR. EMMANUEL J. NCHIMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Musalika kama ifuatavyo:-

La kwanza, Serikali inatambua umuhimu wa kuzingatia misimu katika kuangalia miradi hii ya kukopesha wananchi. Na ndio maana tumezielekeza na kuzishauri benki za *CRDB* na *NMB* kwenda haraka sana katika utekelezaji wa mpango huu. Lakini vile vile *BOT* imeelekezwa kusimamia mafunzo haya kwa haraka ili utaratibu huu uanze mara moja. Nikuhakikishie Mheshimiwa Naibu Spika na Mheshimiwa Mbunge kwamba tutafanya kila jitihada kufuatilia kwa karibu kuona kwamba zoezi hili linakamilika mara moja na utaratibu huu unaanza ili isiwaathiri wakulima.

Swali la pili, Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza niseme Serikali inawajali wananchi wote bila kujali wa mijini na vijijini. Na inajitahidi kila inavyowezekana kuwafikia wote. Kwahiyo na katika mpango huu kama tulivyofanya mwanzo, tumechagua Taasisi ndogo ndogo za fedha awamu hii ya pili ili tuhakikishe wakulima vijijini wanafikiwa.

Naomba niwahakikishie kwamba tunayo dhamira ya dhati ya kuona kwamba wakulima vijijini wanafikiwa bila kuwaathiri wachuuzi wadogo wadogo ambao nao ni wananchi wa Tanzania.

Na. 41

**Televisheni Ya SUA *(SUA TV)***

**MHE. OMAR M. NIBUKA** aliuliza:-

Kwa kuwa, malengo ya kuanzisha Televisheni ya *SUA (SUA TV)* ni kwa ajili ya kusambaza elimu ya kilimo bora cha kisasa kwa mazao mbalimbali na kufanya matokeo ya tafiti mbalimbali za mazao yafike haraka kwa wananchi wa Tanzania hasa wakulima:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuiongezea masafa *SUA TV* ikiwa ni pamoja na vifaa ili kuongezea uwezo?

(b) Je, Serikali iko tayari kuongeza nguvu ya kifedha kwa Taasisi ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, ili kiwafikie Watanzania wote hasa wakulima vijijini?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omar Mzeru Nibuka, Mbunge wa Morogoro Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba madhumuni ya kuanzishwa kwa *SUA-TV* ni kwaajili ya kusambaza elimu ya kilimo bora na cha kisasa ambayo hutokana na matokeo ya utafiti unaofanywa na Wataalam wa chuo hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kutokana na matatizo ya fedha ya kununulia *"Transmitter"* kubwa, masafa ya *SUA-TV* ni mafupi kwani huenda umbali wa

kilometa 30 tu. Wizara yangu ikishirikiana na Chuo chenyewe, pamoja na wadau wengine inachukua hatua za muda mfupi na za muda mrefu ili kuongeza masafa hayo na hivyo kutekeleza azma ya *SUA-TV* ya kusambaza taarifa na matokeo ya utafiti mbalimbali kwa wananchi wengi zaidi nchini.Hatua hizo ni kama ifuatavyo:-

(i) Chuo kimekamilisha mchanganuo wa mahitaji ya *SUA-TV* kuongeza masafa kutoka kilometa thelathini (30) hadi kufikia kilometa tisini (90). Mchanganuo huo utaombewa fedha Serikalini kwenye Bajeti ya mwaka 2008/2009.

(ii) Chuo kinafanya utaratibu wa kushirikiana na *TV* nyingine nchini kama vile *TVT, ITV, Star TV, Channel '10'* na *TVZ* katika kurusha matangazo yake. Katika ushirikiano huu Chuo kitakuwa kinatayarisha *program* za elimu na ushauri katika kilimo ambazo *TV* zingine nilizozitaja zitakuwa zinatangaza nchi nzima. Kwa utaratibu huu tunaamini kuwa taarifa na matokeo ya tafiti za *SUA* zitakuwa zinawafikia wananchi wengi zaidi Tanzania. Hatua ya muda mrefu ni Chuo kuandaa andiko la Mradi ambao utawezesha kupata fedha kutoka Serikalini na kwa wafadhili mbalimbali ili kununua vifaa vya kisasa vya *TV* ili *SUA-TV* iweze kuonekana katika Mikoa yote ya Tanzania. Mradi huu pia utawezesha *SUA-TV* kuajiri watangazaji mahiri na kuwaendeleza waliopo sasa.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu itaendelea kukitengea fedha zaidi Chuo hiki kadiri hali ya kifedha itakapokuwa inaruhusu.

**MHE. OMAR M. NIBUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri. Lakini kwa kuwa uti wa mgongo wan chi yetu ni kilimo, na ili kufikia malengo hayo ya kilimo eeh, yanahitaji kilimo bora cha kisasa na kwa kuwa wananchi waliokuwa wengi au wakulima waliokuwa wengi bado hawajaweza kulima kilimo cha kisasa. Na kama alivyosema katika jibu lake la msingi kwamba masafa ya *SUA-TV* ni mafupi na hata watakapojaribu kuongeza yatafikia kilometa 90 ambazo katika Mkoa wa Morogoro ni sehemu ndogo sana. Na pamoja kwamba anasema baadaye wataunganisha na *TV* nyingine katika Mikoa mingine, lakini wananchi wa Wilaya za Morogoro ambazo ziko ndani zaidi watakuwa pia hawawezi kupata matangazo hayo. Je, sasa haoni kwamba Serikali ingejitahidi iongeze masafa badala ya kuwa 90 yawe mengi zaidi ili wananchi wa Morogoro vijijini na Wilaya zake wote waweze kunufaika ili waweze kulima kilimo cha kisasa, waweze kupata tija?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu ya Juu Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dokta Mzeru kama ifuatavyo:-

Kwa kweli, alichosema Mheshimiwa Mbunge, ndicho na mimi nilichosema. Kwamba jitihada zinafanyika kuwapata wananchi wengi kwa kutumia kwanza hizo *TV* nyingine. Lakini pia tunaongeza masafa na pesa ikipatikana tutaongeza masafa zaidi. Kwa hiyo wote tuko katika lugha moja.

Na. 42

**Kituo cha Polisi cha Bububu**

**MHE. MASOLWA C. MASOLWA** aliuliza:-

Kwa kuwa, kituo cha Polisi cha Bububu ni miongoni kwa vituo vikongwe Zanzibar, ambacho kinahudumia Jimbo la Bububu na baadhi ya Majimbo ya Mfenesini, mtoni na Dole:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kukipelekea kituo hicho gari au pikipiki na vifaa vya mawasiliano (*walk talkies)* ambavyo ni muhimu kwa kuwasiliana panapokuwa na matukio ya uhalifu?

(b) Je, ni lini Jengo la Ofisi ya kituo hicho litafanyiwa matengenezo pamoja na kukamilisha uasambazaji wa umeme kwenye jengo wanaloishi familia mbili za askari?

(c) Ni lini hati miliki ya eneo la kituo itapatikana?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruksa yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia, napenda kumjibu Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mbunge wa Bububu, swali lake lenye sehemu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kituo cha polisi Bububu hakina usafiri wa gari na pikipiki, ikiwa ni pamoja na kuwepo kwa upungufu wa vifaa vya mawasiliano. Hata hivyo Serikali ina mpango wa kulitafutia ufumbuzi wa kudumu suala hilo kupitia mpango wa maboresho wa jeshi la polisi. Lakini kwa hivi sasa lipo gari la *OCD* Magharibi Unguja ambalo linatumika kufuatilia matukio ya uhalifu. Aidha, pikipiki za doria zimekuwa zikitumika mara kwa mara kutoa huduma kituoni hapo. Kuhusu vifaa vya mawasiliano tatizo hilo limepungua kwa hivi sasa baada ya kituo hicho kupewa *Radio* ya *VHF*, *radio* za mikononi pamoja na simu ya kawaida.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kituo cha polisi Bububu kimo katika mpango wa ukarabati wa mwaka wa fedha 2007/2008. Kinachosurubiwa ni upatikanaji wa fedha za fungu la bajeti ili kazi ya ukarabati wa jengo hilo ianze, pamoja na kusambaza umeme katika nyumba za askari wa kituo hicho cha Bububu.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, taratibu za malipo kwa ajili ya michoro ya eneo hilo zimekamilika. Kinachosubiriwa ni kupatikana kwa fedha za kulipia hati za umiliki wa maeneo ya vituo vya polisi Zanzibar, kikiwemo kituo cha polisi cha Bububu

**MHE. MASOLWA C. MASOLWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Namshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ya kuridhisha kwa kweli. Na nina subiri, nafikiri mwakani itakuwa mambo tayari. Pamoja na majibu hayo naomba kuuliza swali dogo tu la

nyongeza. Kwa kuwa, Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba sasahivi wanatumia gari moja tu la *OCD* kwa Wilaya nzima ya Magharibi kwa maana hiyo. Na Wilaya ya Magharibi ni kubwa na ina watu wengi sasahivi kwa kweli na ma, na uhalifu ndio *centre* ya mambo hayo. Je, Serikali haioni haja ya kuongeza magari mengine japo mawili mahsusi kwa kuzidisha, kuiongezea nguvu hiyo gari moja ili waweze kufanya kulipitia hilo eneo kwa uzuri?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA (MHE. MOHAMED ABOUD MOHAMED :** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruksa yako na kwa niaba ya Waziri wa Usalama wa Raia, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cosmas Masolwa, kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa nichukue fursa hii nimshukuru sana Mheshimiwa Mbunge, kwa mashirikiano yake na Jeshi la Polisi hasa katika kusaidia vifaa vya mawasiliano katika kituo cha Bububu, asante sana. Aidha nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba nia ya Serikali ni kutatua matatizo yote ya vitendea kazi kwa Jeshi la Polisi. Lakini kutokana na hali halisi ya uchumi wa nchi yetu ambapo kuna tatizo kubwa la ufinyu wa Bajeti kutekeleza mahitaji yote yaliyotakiwa kwa Jeshi la Polisi hivyo kwa sasa hali hiyo tutaendelea nayo Mpaka pale tutakapopata uwezo wa kutosha ili tuwe na uwezo wa kuwa na magari ya kutosha katika Jeshi la polisi. *(Makofi)*

Na. 43

**Miradi ya Maboresho kwa Wananchi**

**MHE. SHALLY J. RAYMOND** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika awamu ya kwanza, familia za vijiji zikiwemo familia za mkoa wa Kilimanjaro zilinufaika sana na Mradi wa Kopa Ng'ombe lipa ndama katika kuboresha afya za watoto, makazini na kuongeza kipato:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kurejesha upya programu hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Shally Joseph Raymond, Mbunge wa Viti Maalum, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, programu ya kopa ng'ombe lipa ng'ombe imekuwa ikitelekezwa hapa nchini chini ya miradi mbalimbali ikiwemo Mradi wa Mitamba Duniani (*Heifer Project International (HPI*), Mradi wa kuendeleza wafugaji wadogo wadogo katika mikoa ya Tanga na Kagera, Mradi wa kuendeleza Ng'ombe wa maziwa Nyanda za Juu Kusini kwa Mikoa ya Mbeya na Iringa, Mashirika na vikundi mbalimbali. Mingi ya miradi hii imekwishamaliza muda wake lakini baadhi ya vikundi vinaendeleza utaratibu huo. Mradi unaoendelea kutekelezwa hadi sasa ni ule wa Mitamba Duniani (*HPI*) ambao unatekelezwa katika mikoa yote nchini. Katika mwaka 20006/2007 kupitia

mpango huu, jumla ya mitamba 295 imesambazwa hapa nchini kama ifuatavyo:- Kanda ya Kaskazini – 754, Kanda ya Kaskazini Magharibi – 840, Kanda ya Kusini Mashariki - 623 na Kanda ya Kusini Magharibi – 738.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miradi hiyo ilijiwekea mikakati madhubuti ya kuifanya iwe endelevu kwa kuanzisha vikundi, mitandao au ushirika wa wafugaji kwa ajili ya kuendeleza miradi hiyo kwa utaratibu wa mfugaji mmoja kumkopesha mwenzake. Aidha mpango huo ulijihusisha pia katika shughuli za uzalishaji, ukusanyaji, uuzaji na usindikaji wa maziwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa maelezo haya naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mkoa wa Kilimanjaro ni kati ya mikoa maarufu katika ufugaji wa ng'ombe wa maziwa. Takwimu zinaonyesha kuwa mkoa huu una ng'ombe wa maziwa takribani 230,000 kati ya 540,000 waliopo sawa na asilimia 45 hapo nchini. Kati ya miradi iliyochangia katika kuendeleza ufugaji wa ng'ombe wa maziwa mkoani Kilimanjaro ni Mradi wa Uendelezaji wa Ng'ombe wa Maziwa uliofadhiliwa na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa *(FAO)* pamoja na Mradi wa Mitamba Duniani (*HPI*) ambao nimeutaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyokwishasema, mradi huu wa mitamba duniani unaolenga kuinua hali ya maisha ya wananchi wenye kipato kidogo unaendelea kutekelezwa hapa nchini hadi sasa. Kawaida maombi ya mitamba kutoka kwenye mradi huo, wenye makao yake makuu mjini Arusha, huwasilishwa na wafugaji ama vikundi vya wafugaji moja kwa moja kwenye mradi. Mradi huwapatia wafugaji masharti ya namna ya kupokea, kufuga na kusambaza mitamba hiyo. Napenda kuwashauri wananchi wa mkoa wa Kilimanjaro na wananchi wengine wote nchini ambao wangependa kunufaika na mradi huo kuwasilisha maombi yao kwenye mradi. Wizara yangu itakuwa tayari kushirikiana na wafugaji hao ili kufanikisha mpango huo. *(Makofi)*

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuwa lengo la kukopesha wafugaji wadogo ng'ombe wa maziwa ni kuboresha kipato chao. Lakini wafugaji hawa wanakwama kutokana kushindwa kupata madawa ya kutunza ng'ombe hawa, naomba kumwuliza Naibu Waziri. Je, Serikali itafanyaje sasa kutoa kikwazo hicho kwa kuwasaidia kupata madawa? Ili kuboresha afya za ng'ombe hao na kuzidi kupata maziwa kwa wingi.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyowaeleza jana Serikali kuanzia mwaka wa fedha wa 2006/2007 imekuwa ikitoa ruzuku kwa ajili ya madawa ya kuogeshea mifugo ili yaweze kupatikana kwa bei nafuu na tulitangaza kwenye magazeti wazabuni walioshinda kusambaza madawa hayo na pia kuziharifu Halmashauri husika. Hivyo tayari Serikali imekwisha chukua hatua ya kuhakikisha kuwa wafugaji wote wanapata madawa ya kuogeshea mifugo ili kuboresha mifugo hiyo hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Shally Raymond, kwa kuhamasisha ufugaji wa kisasa hususani wa ng'ombe wa maziwa. Nawapongeza pia wananchi mkoa wa Kilimanjaro kwa kuona mapema umuhimu wa ufugaji wa ng'ombe wa maziwa unaoweza kuwanufaisha na kuondoa umaskini, natoa wito mikoa mingine iongeze kasi ya ufugaji wa ng'ombe wa maziwa ili kuongeza uzalishaji wa maziwa nchini ili kuondoa umaskini pamoja na kuboresha afya zetu.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge maswali yamekwisha na muda umezidi, tumezidisha muda kwa sababu katikati hapa mimi nilifanya utambulisho halafu pia hivi vyombo leo vina matatizo. Kwa hiyo, Wabunge wanabidi wahamie chombo kingine na kingine. Kwa hiyo tumetumia muda sio nje ya Katiba tumelipiza muda. SasaWaheshimiwa Wabunge naomba niwaambie kitu kimoja techically mtakumbuka Bunge lililopita ama tulipoanza Bunge ilikuwa ukisimama tu jina lako linatokea kwenye screen, hata Spika hapa linatokea jina lako hata kwa Katibu hapa majina yako yanatokea kutokana na kadi uliyonayo hapo ina jina lako.

Sasa tunapokwambia tumia *microphone* nyingine ni vizuri ukachukua kadi yako ukaweka, usipoweka kadi yako anatokea mtu mwingine na hapa kuna *tv*. Kwa hiyo, wale wanaokuwa waandishi wa habari wa *tv* inaonekana jina la yule mwenye kadi sio wewe unayesema.

Kwa hiyo, tunapokwambia *microphone* nyingine chukua hiyo yako ukaweke katika hiyo *microphone* nyingine. Na hivyo basi Wabunge wanaohamahama nao pia haipendezi kwanza mnahangaisha spika lakini pia ni tatizo linakuwa hilo unakuwa wewe mtu mwingine. Kwa hiyo, kaeni kwenye viti vyetu, mnapoomba utumie *microphone* nyingine tumia kadi yako kuongea pale.

Baada ya kusema hayo naomba nitambulishe wageni tulionao, leo tuna wageni wengi. Kwanza kabisa naanza kama nilivyosema Spika wa Bunge la Afrika Mashariki nilishamtambulisha, napenda kumkaribisha sana hapa Dodoma sisi ndiyo *consitutency* yenu. (*Makofi*)

Pia naomba niwatambulishe Waheshimiwa Mawaziri wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambao wamekuja, kwanza kabisa nimtambulishe Mheshimiwa Waziri Mkuu Mstaafu, Mheshimiwa Fredrick Sumaye, yuko katika *garalley* yetu. (*Makofi*)

Kama mnavyofahamu ukumbi huu hata jiwe la uzinduzi ni la Mheshimiwa Sumaye. Kwa hiyo, kila tunapokaa hapa Mheshimiwa Sumaye anakumbuka kwa hilo. Halafu nina Waheshimiwa Mawaziri wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar nikianza na Mheshimiwa Burhay Sadat Haji Waziri wa Kilimo wa Zanzibar na Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM, mwakilishi wa Jimbo la Kikwajuni tafadhali naomba kama upo usimame. Halafu nina Waziri mwingine Mwinyi Haji Makame, yeye ni Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Rais, Zanzibar. (*Makofi*)

Halafu ninaye Mheshimiwa Waziri yeye mdogo wangu Mheshimiwa na mama yake mdogo na mtu Samier Saluu Hassan Waziri wa Biashara, Utalii na Uwekezaji,

Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM, nafikiri Mawaziri nimemaliza, kuna Naibu Waziri Mheshimiwa Shawana Buheti Hassan Naibu Waziri wa Afya na matibabu Zanzibar, wako na mumewe Yussufu Hamis Katibu mwenezi wa CCM mkoa wa Kaskazini. Samahani kama wengine sikuwataja maana yake sijapata majina. (*Makofi*)

Lakini tuna wageni wengine, mgeni wa Mheshimiwa Dr. Hussein Ally Mwinyi, ana mgeni wake anaitwa Sumay Mary Said ambaye ni Mwenyekiti wa Jumuiya waliyowekeza katika biashara ya utalii Zanzibar, asimame alipo. Mgeni wa Mheshimiwa Suleiman Nh'unga, ambaye ni Ndugu Shawana, ndiye yule nimeshamtaja Naibu Waziri na Mke wake. Mgeni wa Mheshimiwa Hoogan nafikiri ni Waziri walishatajwa. Nina wageni ambao ni maafisa kutoka mikoa ya Shinyanga, Kagera, Mwanza, Mara, Dodoma, Tabora, Kigoma, Arusha, Kilimanjaro, Morogoro, na Manyara. Nadhani wana semina hawa maana yake naona mikoa mengi tu iko hapa. *(Makofi)*

Kuna wageni wa Mheshimiwa Mohamed Rajab, huyu ni Katibu wa Tawi Jang'ombe yupo mshika fedha wa tawi hilo hilo la Jang'ombe, yuko mjumbe wa Kamati ya Siasa tawi hilo hilo nadhani. Halafu yuko Mheshimiwa Mvita Kibendera, mstaafu baraza la wawakilishi.

Wageni wengine ni wa Mheshimiwa Haroub Masoud naomba wote kuna Mheshimiwa Mwenyekiti wa CCM mkoa wa Kusini Unguja, kuna Mheshimiwa Hassan Shaban - Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Kati. Kuna Mheshimiwa Subira Mohamed, Katibu wa CCM Wilaya ya Kati, kuna Ndugu Mussa Ame Silima, kuna Ndugu Ally Ramadhan na kuna Ndugu Juma Abdallah. Kuna Mwantuma Dau, Ndugu Mwinyi Juma na Ndugu Habiba Alawi.

Halafu tuna wageni wengine wa Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis yuko Mheshimwia Mjumbe Msuri, Mwenyekiti wa Wilaya ya Magharibi Zanzibar, kuna Mheshimiwa Mkongela Ali Pira, Katibu wa Wilaya ya Magharibi Zanzibar.

Kuna wanafunzi 65 kutoka *Dakawa High School* na walimu wao. Halafu pia ninapenda kuwatambulisha wageni ambao ni Mheshimiwa Mchungwa ambaye ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Meatu hawa ni wageni wa Salm Khamis. Tuna mgeni Seleman Nassoro na Naibu Spika naye ana wageni wake kuna madiwani wawili kutoka Halmashauri ya Mji wa Njombe kuna Mheshimiwa Mama Haule Diwani wa Viti Maalum, kuna Mheshimiwa Agustini Mbanga, Mwenyekiti wa Halmashauri Mstaafu. Halafu kuna wapiga madebe na wakereketwa wawili wasimame huko. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge na wageni wangu mlioko huko wote ni wageni wa Bunge wengine majina yao hatuna lakini kama kawaida yetu Bunge ni la wananchi kwa hiyo wakati wowote unaposikia kuja kusikiliza Bunge kwa utaratibu kama uliyofuata. Basi wageni hawa wanapenda kuwatambulisha wageni wao lakini wote wanakaribishwa kwa kwa kweli karibuni sana. Tuendelee na shughuli zinazofuata.(*Makofi*)

Sasa matangazo ya kazi kwanza kabisa Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara, Mheshimiwa William Shellukindo anapenda kuwatangazia Wajumbe wa

Kamati yake kwamba leo tarehe 1 Novemba, 2007 kutakuwa na Kikao cha Kamati, kitachofanyika saa 7.00 mchana katika ukumbi Na. 231gorofa ya pili, wajumbe wanaohusika wakumbuke kuhudhuria bila kukosa.

Katibu wa Chama cha Wanawake wa Bunge, Mheshimiwa Switi, anawatangazia wajumbe wa Chama cha Wanawake wa Bunge kuwa wawe na kikao kwa muda mfupi tu kesho tarehe 2 Novemba, 2007. Kwa wanachama wote, kuzungumzia mambo yao wenyewe watakakutana wapi sijui. Nadhani tutatangaza tena kesho kwa hiyo naomba kesho hiyo wakutane kwa muda mfupi lakini *time* hawakusema, kwa sababu ni kesho.

Baada ya kusema hivyo nadhani matangazo yamekwisha sasa tuendelee na shughuli za kawaida, Katibu endelea na *Order Paper*.

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Wataalam wa Mionzi wa mwaka 2007
### (*The Medical Radiology and Imaging Professionals Bill, 2007)*

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada uitwao *The Medical Radiology and Imaging Professionals* wa mwaka 2007 kama ulivyopangwa kwenye shughuli za leo pamoja na marekebisho yake yaliyoambatishwa sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika miaka ya hivi karibuni sekta ya afya imekuwa na mabadiliko mengi kwa lengo la kuboresha utoaji wa huduma za afya hapa nchini. Kutoka na mabadiliko hayo Wizara imeona umuhimu wa kutunga sheria ya kuunda baraza la wataalam wa rediolojia ambayo inapendekezwa iitwe the *Medical Radiology and Imaging Professionals Act*, 2007. Jitihada za Serikali katika kuboresha huduma za Afya zimatoa fursa kwa sekta binafsi pia kutoa huduma za afya kwa wananchi. Hali hii imefungua mianya kwa sekta binafsi kutoa huduma rediolojia ambazo zinaweza kusababisha huduma hii kutolewa kwa viwango visivyokidhi na hivyo kuhatarisha maisha ya wananchi kama hakutakuwepo chombo cha kusimamia na kudhibiti huduma hizi za rediolojia hapa nchini.

Mheshimwia Naibu Spika, sheria iliyopo hadi sasa *the radiation act* ilianzishwa na *Tanzania atomic energy commission* sheria hii inaangalia zaidi usalama wa mazingira yenye mitambo ya ki-*nuclear* zikiwemo idara za *X-Ray* mahospitalini. Lakini haisimami kabisa utendaji wa wataalam wa fani hii katika sekta ya afya, utalaam wa mionzi ni suala nyeti, hivyo watendaji wake wanatakiwa kusimamiwa katika utoaji wa huduma hii ili kuhakikisha kwamba huduma zinazotolewa hazina madhara kwa wananchi. Katika

uzoefu wa kutekeleza sheria iliyopo imeonekana ina upungufu mwingi, upungufu ni kama nitakavyoorodhesha:-

(a) Matumizi mabaya na ya kiholela ya mionzi ya *X-Ray* yatolewayo na watu wasio watalaam.

(b) Ongezeko kubwa la vituo vya watu binafsi ambavyo baadhi viko chini ya viwango.

(c) Ongezeko la wagonjwa wanaohitaji huduma ya mionzi kwa ajili ya uchunguzi au tiba.

(d) Kuwepo kwa matukio ya ukiukwaji wa maadili katika utoaji wa huduma za rediolojia katika baadhi ya hospitali. Ilishindikana kuyatolea uamuzi matukio haya na badala yake yakaamuliwa kwa kutumia taratibu za kawaida za kazi. Vilevile sheria ya *Radiation Act* haikidhi usimamizi wa wataalam wanaotumia vyombo vya mionzi katika kuhudumia wagonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhumuni ya Sheria inayopendekezwa ni kuweka utaratibu wa kisheria wa kusimamia wataalam wa Rediolojia yaani mionzi ni suala nyeti hivyo watendaji wake wanatakiwa kusimamiwa katika utoaji huduma ili kuhakikisha kwamba huduma zinazotolewa kwa wananchi hazina madhara.Wizara iliwasiliana na wadau mbalimbali ili kupata maoni yao na haya maoni yalizingatiwa katika mapendekezo ya sheria hii pamoja na yale yaliyopendekezwa na wajumbe walioshiriki katika ngazi mbalimbali kabla ya kujadili katika waraka wa baraza la Mawaziri.

Matarajio yetu endapo hii sheria itatungwa ni kwamba huduma za afya zitaboreshwa tutahakikisha usalama kwa wagonjwa na pia tutakuwa na nguvu ya sheria ya kuwalinda wataalam wagonjwa na jamii kutokana na utendaji wa mbovu wa matumizi ya mionzi.Muswada huu unakusudia kupendekeza sheria ya baraza la wataalam wa rediolojia litakalosimamia utendaji wa wataalam hao. Muswada umegawanyika katika sehemu kuu sita ambazo zinapendekeza mambo muhimu kama ifuatavyo:-

1. Sehemu ya Kwanza inapendekeza mambo ya Awali ambayo yanajumuisha jina la sheria inayopendekezwa, tarehe ya kuanza kutumika kwa sheria hiyo, matumizi yake na ufafanuzi wa maana ya msamiati kama ilivyotumika katika sheria inavyopendekezwa. Matumizi yake na ufafanuzi wa maana ya msamiati kama ilivyotumika katika sheria inayopendekezwa.
2. Sehemu ya Pili inapendekeza kuundwa kwa Baraza la wataalam wa rediolojia ili kusimamia utendaji wa wataalam hao. Uteuzi wa wajumbe wa Baraza, majukumu na mamlaka ya Baraza ni mambo yanayofafanuliwa katika sehemu hii. Inapendekezwa kwamba Baraza litakuwa ni chombo chenye mamlaka peke yake litakaloshughulikia usajili wa wataalam wa rediolojia katika ngazi mbalimbali. Sehemu hii vilevile inapendekeza pia uteuzi wa msajili wa Baraza Naibu Msajili na watendaji wengine wa Baraza.

3. Sehemu ya Tatu inapendekeza mambo yanayohusu mambo usajili wa wataalam katika ngazi mbalimbali chini ya sheria inayopendekezwa, sifa za usajili utaratibu wa usajili na utoaji wa shahada yaani *Certificates* chini ya sheria hii ni mambo yanayopendekezwa katika sehemu hii. Kwa mujibu ya mapendekezo haya usajili wa wataalam wa rediolojia kabla ya kutekeleza taaluma zao ni jambo la lazima.

4. Sehemu ya Nne inapendekeza masuala ya fedha ya Baraza, masuala haya yanajumuisha vyanzo vya mapato ya Baraza, mahesabu ya fedha na ukaguzi wa mahesabu pamoja na malipo ya wajumbe ya baraza la wafanyakazi wa baraza hilo.
5. Sehemu ya Tano inapendekeza mambo ya ujumla yanayohusu wataalam wa rediolojia, mambo yanayopendekezwa ni pamoja na uchapishaji wa majina ya wataalam waliosajiliwa, utaratibu wa kusitisha au kufuta shahada ya usajili na utovu wa maadili kitaaluma na utaratibu wa rufaa chini ya sheria inayopendekezwa.

6. Sheria ya Sita na mwisho inapendekeza mambo mbalimbali yakiwemo makosa na adhabu kinga ya wajumbe wa baraza wa Kamati na Kamati za baraza na watendaji wengine wa baraza. Mamlaka kutengeneza kanuni na kanuni za maadili chini ya sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho baada ya maelezo hayo kwa heshima naomba kuwasilisha Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Wataalam wa Huduma za Rediolojia nchini yaani *The Medical Radiology and Imaging Professionals Act,* 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. DR. HAJI MWITA HAJI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA HDUMA ZA JAMII):** Mheshimiwa Naibu Spika, Naomba kutoa maoni ya Kamati ya Huduma za Jamii kuhusu Muswada wa Baraza la Wataalam wa Rediolojia yaani Mionzi la *Medical Radiology and Imaging Professionals Act,* 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile Mwenyekiti wangu alishatoa rambi rambi kwa niaba ya Kamati, kwa niaba ya wananchi wa jimbo la Muyuni naomba kutumia nafasi kutoa rambi rambi kwa familia na wananchi wa mkoa wa Kilimanjaro, kwa kifo cha Mheshimiwa Salome Mbatia, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum na Naibu Waziri

wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Mungu ailaze Roho ya Marehemu Mahali Pema Peponi.

Aidha, natoa pole kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliopatwa na ajali mbalimbali za magari akiwemo Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir, Mbunge wa Jimbo la Mchinga na Mheshimiwa Prof. Juma Kapuya Mbunge wa Jimbo la Urambo Mashariki na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, tunawaombea wapone haraka. *(Makofi)*

Kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii Mheshimiwa Omar Shaban Kwaagw', Mbunge wa Babati Mjini nachukua nafasi hii kwa mujibu wa Kanuni za Bunge za Mwaka 2004 Kanuni ya 70(2) naomba kutoa maoni ya Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Huduma za Jamii ambayo uliipa jukumu ya kufikiria Muswada wa Sheria ya Baraza la Usajili la Wataalam wa Rediolojia mionzi, yaani *The Medical Radiology and Imaging Professionals Act* 2007.

Kamati ilikutana na ilipata maelezo ya Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii na pia ilipata maoni ya wadau wa Muswada na hatimaye ilichambua na kupitia vifungu vyote vya Muswada.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaunga mkono hatua ya Serikali ya kuleta Bungeni Muswada wa Sheria ya kuanzisha baraza la usajili wa wataalam wa rediolojia yaani mionzi. Kwa madhumuni ya kuweka utaratibu wenye mtiririko mzuri wa kusimamia utendaji na utekelezaji wa wataalam wa rediolojia yaani mionzi kwa lengo la kujenga mazingira sahihi na maadili ya kuboresha huduma ya afya nchini.Kamati inaelewa fika matatizo na hatari zinazoweza kujitokeza kutokana na matumizi yasiyo na matumizi ya kiholela yasiyozingatia maadili ya taaluma ya rediolojia mionzi. Katika mashine zinatumia mionzi uchunguza malazi au matatizo ya afya ya binadamu kama vile *X-Rays*, *Ultra Sound*, *CT Scan* na kadhalika. Kamati ilielezwa kuwa huduma za rediolojia zimekuwa zikitolewa na watumishi wasio na utalaam kwa fani ya mionzi katika baadhi ya hospitali hapa nchini. Pia baadhi ya wataalam rediolojia hukiuka maadili ya taaluma zao katika baadhi ya hospitali na kuwa sheria iliyopo ya *Radiation Act* ilishindwa kutoa jawabu la kutosheleza kuchukua hatua sahihi kwa waliokiuka maadili ya taaluma na hivyo Serikali kulazimika kutumia busara za kawaida kupata jawabu.

Taaluma ya rediolojia mionzi ni nyeti na hatari, hivyo inatakiwa itolewe na wataalam sahihi katika mazingira ikiwa ni pamoja na kuchukua tahadhari zinazotakiwa ili kuepuka madhara kwa wagonjwa na watalaam. Vilevile kutokana na hatua nzuri ya Serikali kuboresha hospitali za wilaya mikoa hospitali maalum na hospitali za rufaa ikiwa ni pamoja na na kuzipatia mashine zinazotumia mionzi katika uchunguzi kama vile *X-Ray Ultra Sound* na *CT Scan* na kadhalika. Hivyo kutokana na changamoto hizo Kamati inakubaliana na Serikali kuwa kuna umuhimu wa kuwa na sheria ya kusimamia na kudhibiti wataalam rediolojia hapa nchini.

Inaona kuwa na Muswada wa Sheria hii umeletwa kwa kuzingatia Kanuni ya 149(2) ya utumishi wa umma ya mwaka 2003 na sheria ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1982 kifungu 174(a) (2) zilizoelekeza kuanzisha mabaraza ya usajili wa wataalam sera ya

afya ya mwaka 1990 kama ilivyorejea katika mwaka 2007 na pia kwa kuzingatia umuhimu wa kila sekta kusimamia taaluma za wataalam waliopo katika Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia maelezo hayo hapo juu Kamati pia inakubaliana na Serikali kuwa sheria hii ni muhimu katika yafuatayo:-

Kwanza, Serikali itaweza kuwa na utaratibu mzuri wa kusimamia utendaji kazi wa wataalam wa radiolojia yaani mionzi.

Pili, taaluma za radiolojia yaani mionzi ni nyeti hivyo wataalam watasimamiwa kuona kuwa huduma zinatolewa bila kuleta madhara kwa wananchi.

Tatu, huduma ya afya itaboreshwa.

Nne, usalama wa wagonjwa utahakikishwa na pia sheria itawalinda wataalam, wagonjwa na jamii kutokana na utendaji mbovu wa matumizi ya mionzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala yaliyotajwa hapo juu yataweza kusimamiwa na kutekelezwa kwa ufasaha na Baraza la Usajili Watalaamu wa Radiolojia yaani mionzi linalopewa jukumu la usajili na usimamizi wa utendaji wa watalaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kufikiria Muswada huu, Kamati ilipitia sehemu zote saba na vipengele vyake na hivyo kutoa maoni katika vifungu mbalimbali ambavyo Serikali imeshauriwa kuviboresha kama ifuatavyo:-

Sehemu ya pili, inahusu Wajumbe wa Baraza. Kifungu Na.5(1)(f), Kamati inashauri kuwa maneno *Regional, Radiographer* yabadilishwe na kuwa maneno *Radiotherapist*. Kipengele cha G maneno *Private Hospital Association* yabadilishwe na kuwa *The Association of Private Hospital or Private Health Facilities in Tanzania.* Kipengele H kisomeke *A Medical Nuclear Physicist*.

Kifungu Na.6(2)J, Kamati inashauri kipengele hicho kitolewe ufafanuzi kwa sababu jukumu la ukaguzi wa ithibati ya mitaala na vifaa vya kufundishia linatekelezwa na vyombo vilivyoundwa kwa sheria zilizotungwa na Bunge hilihili kwa mfano Tume ya Vyuo Vikuu yaani *Tanzania Commission for University* na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi yaani (*NACTE)* na kuwa kinaweza kuleta tatizo la kuingiliana kati ya vyombo vya Serikali katika kutekeleza majukumu yake. Kamati inashauri kuwa iipengele hiki kifanyiwe marekebisho vinginevyo Kamati inashauri kiondolewe.

Kifungu 11 cha Muswada, Kamati inapendekeza kuwa kipengele Na.3 kisomeke kama ifuatavyo:-

”*There shall be a Deputy Registrar appointed by the Minister from among Medical Radiology and imaging professionals for the purpose of existing the Registrar in his day to day duties”*

Kifungu 17(2) cha Muswada, Kamati inapendekeza kuwa maneno *Health Laboratories Practitioner* yabadilishwe kuwa *Medical Radiology and Imaging professionals* ambayo yanahusu sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni ya jumla. Kamati inashauri kuwa huduma ya kufanya uchunguzi wa maradhi au tiba kwa matumizi ya vifaa na taaluma ya radiolojia ni nyeti na hatari hivyo ni vema na lazima vifaa vya kupima mionzi vivaliwe na watalaam wakati wote wanapotumia vifaa vya mionzi.

Pia, Kamati inashauri kuwa ni lazima watalaamu kuchukua tahadhari zote ikiwa ni pamoja na kutumia kofia maalumu za kuzuia uwezekano wa kupata saratani ya damu au kupata tatizo la vipara vichwani.

Vilevile, mashine zinazotumia utaalamu wa radiolojia zifanyiwe ukaguzi wa mara kwa mara na matengenezo yafanyike ili kudhibiti uwezekano wa kuvuja kwa mionzi. Aidha, mabaki ya vifaa hivyo yahifadhiwe katika maghala maalumu yaliyoandaliwa kwa shughuli hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Kamati inashauri Serikali kupitia Baraza la Usajili wa Watalaam wa Radiolojia yaani mionzi kusimamia kwa makini matumizi ya vifaa vinavyotumia mionzi, kufanya uchunguzi wa wagonjwa na pia tiba inayotumia taaluma hii. Aidha, kutokana na sera ya soko huria na kufunguliwa kwa milango ya biashara inayoelekea kuanzishwa kwa hospitali mbalimbali za watu binafsi na mashirika ya kijamii yakiwemo ya dini na kuwepo kwa uwezekano wa kuagizwa au kuingizwa nchini vifaa mbalimbali vya tiba ya kufanyia uchunguzi wa magonjwa vikiwemo vifaa vinavyotumia taaluma ya radiolojia, ni vema Serikali au Baraza la Usajili kujiridhisha na uwezo au ubora wa vifaa hivyo na pia kuwepo kwa watalaam wenye viwango vya elimu ya kutumia vifaa hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia, naomba kuchukua fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, Mheshimiwa Prof. David Homeli Mwakyusa (Mb.) na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Dr. Aisha O. Kigoda (Mb.) na Wataalamu wa Serikali kwa ushirikiano na ufafanuzi waliutoa wakati Kamati ilipokuwa ikijadili na kuchambua Muswada wa Sheria ya Baraza la Radiolojia yaani mionzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Wajumbe wa Kamati hii kwa mawazo na maelekezo mazuri kwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii na ninapenda pia kuchukua fursa hii kuwashukuru kwa dhati kwa kushiriki kwa umakini wakati Kamati ikifikiria hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji. Waheshimiwa Wabunge, mpaka sasa aliyeomba kuchangia ni mchangiaji mmoja tu kwa hiyo kama kuna mtu alifikiri kuchangia basi nafasi ipo. Sasa nitamwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Omar!

**MHE. OMAR ALI MZEE (K.n.y. MHE. DR. ALI TARAB ALI – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Sheria ya Uanzishwaji wa Baraza la Wataalam wa Mionzi ya mwaka 2007, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Na.43(5)(b)(c), toleo la 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wa Bunge hili Tukufu kutoa pole kwa familia ya Marehemu Salome Mbatia. Pia natoa pole kwa jamii nzima ya wanawake wa Tanzania bila ya kujali itikadi zao kwa kumpoteza kiongozi huyo mwenye mwamko wa kupigania haki za sisi wanawake na kusukuma gurudumu la maendeleo ya nchi yetu. Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema peponi, amen.

Naomba pia kutoa pole kwa Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Kiongozi wa Upinzani Bungeni kwa kufiwa na mama yake mpendwa wakati hili linatokea yeye mwenyewe ni mgonjwa na yuko nje ya nchi kwa matibabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na timu nzima ya wataalam wa Wizara yake kwa kuleta Muswada huu ambao kwa ujumla unatambua umuhimu wa taaluma ya tiba hii ya mionzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhumuni ya Muswada huu ni mazuri kabisa kutokana na hali halisi ya wale wanaojihusisha na taaluma yenyewe na mazingira halisi wanayofanyia kazi wataalam hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, taaluma yoyote ambayo inahusisha vifaa vya sayansi na hasa vyenye kuhitaji uchunguzi wa kitaalam au utafiti wa hali ya juu, mara kwa mara vinakuwa na gharama kubwa katika kupatikana kwake na vile vile gharama za uendeshaji. Magonjwa yanayofanyiwa uchunguzi ili kujulikana kwa kuhusisha taaluma ya mionzi *(investigative radiology*) kama vile *X-ray*, *computed tomography, CT-Scan* na vipimo vingine ambavyo wataalam waliomo katika fani hiyo ndio wanaweza kuvieleza vizuri, mara zote inaendana na gharama kubwa anayotakiwa kulipwa na mgonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukubwa wa gharama hizo unatokana na "*Complications on Radiotherapy* ". Kwa sababu hii na kwa kuangalia hali halisi ya kipato cha Watanzania walio wengi, ni dhahiri kuwa vipimo na tiba inayohusisha taaluma hii ya mionzi bado itawawia vigumu Watanzania wengi. Wakati tunatunga sheria hii muhimu, ni vema pia tukaelezea kuwa sheria hii nzuri, inawezekana sana isiwanufaishe Watanzania walio wengi kwa ajili ya gharama hizo. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali iangalie utaratibu wa haraka na wa makusudi utakaowawezesha Watanzania angalau wa

kipato cha chini kupatiwa vipimo hivi ambavyo mara nyingine ni muhimu sana kwa uhai wao, kwa bei ya chini, yaani '*subsidized*' vinginevyo wananchi walio wengi ambao hawawezi kulipia gharama ya *CT-Scan* na vipimo kama hivyo, hawatapata kabisa huduma hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni jambo linalohitaji hatua ya haraka kwani sisi viongozi tunapougua mara moja siyo tu tunalipiwa gharama ya vipimo na Serikali lakini tunarushwa nchi za nje kama vile Afrika Kusini, India, Uingereza na kwingineko. Katika masuala ya uhai, hakuna ukubwa na kila mmoja anahitaji kupata angalau huduma za msingi. Ni kwa msingi huo basi, hatua ya dharura ya Serikali itaisaidia sana jamii kubwa ya Watanzania katika kupata huduma hizi na wao wakachingia labda kiasi kidogo kwa kadiri ya uwezo wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuundwa kwa Baraza hili la wanataaluma inayohusisha tabibu ya mionzi lizingatie "*ethical responsibilities as radiologist*" kati ya majukumu hayo ni kutoa tafsiri sahihi ya picha ya mgonjwa (*providing excellent image interpretation*), kutoa tathmini ya haraka kuhusu matokeo ya picha za mgonjwa (*assessing the appropriateness of the imaging examination*) na kulinda maslahi/matakwa ya mgonjwa (*protecting patient interests).*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Baraza litakuwa na kazi kubwa ya kuhakikisha wataalam wa fani hii wanaendana na hali halisi ya Watanzania kwa kuweka mbele "*ethical responsibilities"* za taaluma yenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana na sasa tumepata wachangiaji wawili lakini kwanza kabisa nitamwita Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa atafuatiwa na Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga. Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, karibu.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nichangie Muswada uliopo mbele yetu. Kwa kuwa si mara yangu ya kwanza kuongea ndani ya Bunge hili, naomba nisirudie kutoa pole na rambirambi kwa ndugu zetu waliopata misiba na maafa mbalimbali ila tu kwa kuwa Kiongozi wangu Mheshimiwa Hamad Rashid anapata *operation* leo basi nimwombe tu Mwenyezi Mungu ampe nguvu ya kuweza kupokea maumivu yanayotokana na kazi hiyo kubwa iliyopo mbele yake kule India.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda niseme tu kwamba Muswada huu ni Muswada muhimu. Niungane na Mwenyekiti wa Kamati pamoja na Msemaji wa Kambi ya Upinzani katika kukazia yale ambayo yataufanya Muswada huu uweze kufanya kazi yake vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuunga mkono yale yaliyosemwa na wasemaji wetu hawa wawili, nianze tu kwa kutambua kwamba Muswada huu unatumika *Mainland* Tanzania kwa jinsi ulivyoainishwa katika Kifungu cha II cha Muswada wenyewe na hilo niliunganishe na Kifungu Na.19 ambacho ndicho kilichonifanya nisimame.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimegundua jambo hili hapa mwishoni kwa kuwa Muswada huu sikuwa nao mapema lakini sina hakika kama wenzetu waliochambua Muswada waliona athari ya kifungu hiki.

**NAIBU SPIKA:** Kifungu namba ngapi?

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu Na.19 ukurasa wa 13 ambapo kinasomeka kama ifuatavyo:-

"*A foreigner and Tanzania citizens who qualified Mainland Tanzania shall upon payment of prescribed ...*"

Sasa nina tatizo kidogo na Kifungu hiki sina tatizo kwa upande wa *foreigner* yule mgeni asiye Mtanzania lakini inapomuunganisha na *Tanzanian Citizen* yaani Mwananchi Mtanzania anaye-*qualify* halafu inatumia neno zito kabisa *outside Mainland Tanzania* kwa maana ya kwamba hata yule anaye-*qualify* Tanzania Visiwani na yeye ni lazima awe *registered* kana kwamba na yeye ni *foreigner,* hapo ndipo ninapoona tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, inanipa kidogo shida kwa sababu kifungu hiki ukikisoma pamoja na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 13 ambayo inaruhusu Mtanzania yeyote kuzunguka na kutembea na kuishi mahali popote katika Jamhuri na kwa maana hiyo kufanya kazi vilevile bila ubaguzi wa aina yoyote katika Jamhuri ya Muungano, utaona vinapingana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma kifungu hicho pamoja na Kifungu Na.17 vilevile inanipa uzito kabisa kwamba huyu Mtanzania kwa nini aweze kubaguliwa na kutakiwa kuandikishwa wakati amesoma na kupata *qualification* yake mathalani *State University of Zanzibar*. *State University of Zanzibar* iko ndani ya Muungano na inatoa vyeti ambavyo vinapaswa kutambuliwa kama vyeti vilivyotambuliwa katika Jamhuri. Najua Wizara ya Afya si suala la Muungano pia najua *State University* iko chini ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar lakini huyu mwananchi inapofika mahali anabaguliwa kwa mtindo huo, nadhani ingekuwa vizuri masuala makubwa na mazito kama haya basi yakaangaliwa katika sura ya Jamhuri ya Muungano badala ya kuangaliwa kwa sura ambayo inaweza ikaonekana ni suala la kubaguana. Mimi hili linanipa matatizo ingeandikwa tu kwamba "a *foreigner who qualified outside Mainland Tanzania*" sina tatizo lakini inapokuwa "a *Tanzanian Citizen who qualified outside Mainland Tanzania"* nadhani Waziri atusaidie kama hili linaweza kuleta utata baadaye na kuonyesha kwamba linawabagua watu wetu katika sura ya aina hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati ninahitaji nipate ufafanuzi wa hilo na kuona kama linaweza likatuletea ugumu huko mbele hasa tukizingatia kwamba wakati tukitunga sheria huko nyuma tulikuwa tunajua kwamba Elimu ya Juu ni suala la Muungano lakini sasa hivi Elimu ya Juu polepole inaanza kuacha kuwa suala la Muungano. Elimu ya Juu sasa inaweza kutolewa kwa kiwango fulani kama inavyotolewa na *State University of Zanzibar*. Najua imeunganishwa bado ni masuala ya Muungano. Sasa inapofikia suala hili nadhani ni vema tukaangalia na Waziri ananiunga mkono kwamba ni kweli Elimu ya Juu bado ni suala la Muungano kwa hiyo kama ni suala la Muungano kifungu hiki ni lazima kiangaliwe katika sura ya Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwa kifupi suala la pili ambalo naliona ni vema likaangaliwa. Muswada huu tumesema hata kwenye Kamati kwamba ni Muswada muhimu sana kwa sababu kimsingi unagusa eneo nyeti sana. Vipimo ni sawa na dawa na hata wakati mwingine dawa haiwezi kutolewa kama vipimo havijapatikana unakwenda kutoa dawa tu au tiba baada ya kupata vipimo sahihi kutokana na kilichoelekezwa na hawa wataalam wetu ambao ni maalum sana. Kwa msingi huo, ni wataalam ambao ni lazima tuwaheshimu kwelikweli. Sasa kwa sababu ni wataalam ambao ni muhimu kwa ajili ya uhai wetu, mambo ya msingi mawili naomba niyaseme hapa.

La kwanza, ni kwamba tuwe na sheria kwa sababu sheria ndiyo inayolinda *standards*, *quality* na kadhalika. Sheria ni lazima iweke vigezo na vipimo vinavyotakiwa lakini ni muhimu sasa tuangalie je, katika hospitali zetu za Serikali vipimo hivi na vyombo hivi vinavyotoa vipimo tunavyo au vipi? Kama tunavyo, je, vinafanya kazi au havifanyi kazi? Kwa mfano, *X-ray* nyingi zinazokuwepo kwenye hospitali zetu za Wilaya muda mwingi unakuta *X-ray* ipo lakini *film* hakuna au *X-ray* imeharibika.

Kwa mfano, ni juzijuzi tu nilikwenda pale *Ocean Road* nikakuta kipimo cha mionzi kinachopima wagonjwa wetu wa saratani kimeharibika. Niliambiwa kitu ambacho kilinistua sana kwamba kutengeneza ni lazima wataalam wake watoke nje ya nchi. Tunaweka mazingira ya aina gani katika vipimo muhimu vya aina hii? *Ocean Road* kama tunavyojua wote ni taasisi pekee kwa nchi nzima inayoshughulikia wagonjwa hawa wa saratani sasa inapokuwa kwamba mtaalam ni lazima atoke sehemu fulani, sikumbuki niliambiwa nchi gani nadhani niliambiwa anatoka Libya au sijui ni wapi, sasa unapopata wataalaam wanaotoka nchi fulani tu kwa sababu labda ndipo tuliponunua au ndipo tunapopata *spare parts* zetu, ni tatizo na watu wetu wanapata shida.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni lazima tuangalie na katika taratibu zetu, je, tuna *provide* fedha kwa kiwango gani ili vifaa hivi vipatikane kwa urahisi ili watu wetu wasipate shida? Tusiangalie tu upande wa udhibiti bali tuangalie na upande wa pili wa upatikanaji wa hivi vifaa vyenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili, matumizi ya vifaa hivi ni ghali kwelikweli. Katika Hospitali za kwetu ukienda Muhimbili kwa mfano mara nyingi vipimo hivi unakuta havipatikani na wagonjwa wetu wanaaambiwa nendeni mahali fulani au nendeni hospitali fulani. Nina uzoefu nilioupata hivi karibuni ambapo mgonjwa ameambiwa aende kupata kipimo mahali pengine kwa mfano MRI Waziri nadhani ni

Daktari anaielewa. Kipimo cha MRI ukienda kwenye hospitali hizi nyingine kinaanzia Sh.200,000/= sasa Sh.200,000/= ninaweza tu mimi Mbunge, Waziri au labda na Afisa mkubwa wa Serikali lakini mwananchi wa kawaida akiambiwa afuate kipimo hiki ni wazi atarudi nyumbani kumwomba Mwenyezi Mungu wake amsaidie tu afe polepole kwa sababu hataweza kupata hicho kipimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kusema hapa ni kwamba tukitambua hivi vipimo ni sehemu ya tiba na wanaopata tiba hii ni Watanzania wetu ambao hali yao tunaifahamu amekuwa *referred* labda Muhimbili kutoka Rukwa au Karatu au hata Kagera amefika Dar es Salaam anaambiwa kipimo hiki hakiwezi kupatikana. Ninaomba kuwe na utaratibu maalum wa kuweza kuwasaidia angalau Serikali i-*subsdise* hivi vipimo ili viweze kupatikana kwa kila mtu na kwa kwa kila ngazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati nzuri, napenda kutamka *interest* yangu, mimi ni Mwenyekiti wa *CCBRT*, sisi kule *CCBRT* tunajaribu kufanya matibabu yaweze kupatikana kwa kila mtu kwa kila ngazi kwa kuwa-*charge* wakati mwingine wale wenye uwezo zaidi ili yule asiye na uwezo aweze kulipiwa na hela zilizotolewa na yule mwenye uwezo. Sasa tusipoingia kwenye utaratibu wa aina hii nadhani tutawafanya Watanzania wetu wengi washindwe kulipia gharama za vipimo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisemi Serikali ilipie kwa sababu wakati mwingine tatizo ni hela, taasisi yetu ya Muhimbili labda haina hela au labda hata hospitali za Mikoa na Wilaya hazina hela lakini tusipofanya utaratibu wa kuchangia kwa kuangalia mwenye uwezo achangie ili kile anachotoa yule mwenye uwezo kiweze kufidia kwa yule ambaye hana basi tutakuwa tumetengeneza matabaka katika nchi yetu na sidhani kama tutaruhusu matabaka yaweze kujengeka hasa katika maeneo nyeti na mazito kama maeneo ya tiba na matibatu. Maeneo haya ni maeneo ambayo ni uhai wa mwananchi na usipomuangalia mwananchi katika eneo hili huna mahali pengine ambapo utaangalia. Kwa hiyo, ni vema tukaepuka kabisa kujenga matabaka katika maeneo yanayohusu matibabu ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa Mheshimiwa Waziri anisaidie baadaye kueleza namna gani tutafanya haya matibabu yawe *affordable*. Katika enzi ya sasa na katika dunia ya sasa kinachozungumziwa ni *affordability* ya matibabu yaani namna gani tutafanya matibabu yaweze kufikika kwa kila mwananchi bila kujali hali yake ya maisha ikoje na uchumi wake ukoje na vilevile hali yake ya fedha ikoje. Tusipofika katika hatua hiyo, nadhani tutakuwa hatujasaidia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Mheshimiwa Waziri pia atusaidie kutueleza wataalaam hao ni wengi kiasi gani? Malalamiko mengi tuliyonayo ni kwamba wataalam hao pia nao hawapo. Muswada wetu unazungumzia majina mengi sana ya hawa wataalam siyo tu wa *X-ray* wala wa *Radiology* lakini inatumia majina mengi sana, sasa ninataka kufahamu tu na nchi ijue kwamba hali yetu ikoje katika kuwaandaa? Tuna vyuo vingapi vya kuwaandaa hawa wataalam? Je, tuna wataalam sasa na tuna *plan* ya muda mrefu kiasi gani kwamba katika muda fulani ujao tutaweza kujitosheleza kwa kupata wataalam hawa ili hata tunaposema tunaweka vikwazo hawa wanaotoka nje watimize

masharti yetu basi tuwe na uhakika pia kwamba na sisi tuna mpango maalumu ndani ya muda fulani tunaweza kujitosheleza kwa kuwa na watalaamu wetu katika hospitali zetu kwa kadri sheria inavyotaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua wataalam hawa wanatakiwa tu wawepo katika ngazi fulani ya hospitali kutokana na unyeti wenyewe lakini pia ni kutokana na gharama kubwa ya vifaa, kutokana vilevile na jinsi ambavyo huwezi tu kuwapeleka kwenye kila ngazi kwa mfano kwenye Hospitali za Wilaya, siyo kila aina ya ugonjwa ni lazima uweze kupimika tunafahamu tatizo hilo lakini je, tunao wataalam wengi kiasi gani na utaratibu wetu wa kuwapata ili kujitosheleza umeandaliwa kwa kiasi gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa na sasa nitamwita Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga.

**MHE. SIRAJU JUMA KABOYONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Jina langu linawapa taabu sana lakini tutazoea taratibu. Wale walionifahamu zamani kwa jina la Juma wanaweza kutumia tu Juma lakini ni Siraju Juma Kaboyonga.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo, kwa kweli Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa *notes* zake na zangu zinalingana kwa kiasi kikubwa. Kwa hiyo, katika kuchangia hoja hii, nitatumia muda mfupi kuliko nilivyotarajia hapo mwanzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, ni kwamba huu ni Muswada wa kitaalamu kuhusu jambo la taaluma ya hali ya juu kwenye eneo la matibabu. Kwa hiyo, watalaamu wameutazama na mambo yote ya kitalaamu yamezingatiwa. Mimi ninataka nisisitize yafuatayo.

La kwanza, ni kwamba eneo la uchunguzi wa maradhi ni eneo muhimu sana hata kabla ya kupata dawa kwa sababu Daktari hawezi kumtibu mgonjwa ambaye hajui ugonjwa wake. Eneo la mionzi yaani *radiology* kama vile ambavyo baadaye tutakuja kuona katika eneo la *Laboratories* na kwa kweli hoja hizi mbili zinafanana sana na tungeweza hata kuzizungumzia zote kwa pamoja kwani yote ni maeneo ya uchunguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nirudi kwenye eneo la mionzi. Kwa bahati mbaya sana eneo kubwa ambalo tunalifahamu wengi tunapozungumzia mionzi hapa nyumbani Tanzania ni eneo la *X-ray*. lakini zaidi ya *X-ray* kuna *CT-Scan*, *MRI*, *Utra-Sound* haya yote ni maeneo ambayo yanasaidia wenzetu Madaktari kuweza kujua huyu mgonjwa tatizo lake ni kadhaa wa kadhaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati mbaya, haya maeneo ya *CT-Scan, MRI* na kwa kwa kiasi fulani *Utra-Sound* yamekuwa ni maeneo adimu kupatikana kwa maana ya uchunguzi hapa nyumbani. Kwa kweli haya ndiyo maeneo ambayo kwa kiasi kikubwa yanahusika kwa baadhi ya wagonjwa ambao wanakwenda nchi za nje, wanapofika kule

hujikuta sehemu kubwa ya vipimo wanavyopata ni hivyo vya *CT-Scan*, *MRI* na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa suala ambalo ningependa Serikali kupitia *Council* hii tutakayoiunda chini ya Muswada huu waangalie uwezekano wa kutengeneza mazingira kwa sekta binafsi kujihusisha katika kutoa huduma hii muhimu ya vipimo hivi. Kwa kweli katika nchi nyingine hususan zilizoendelea siyo lazima *CT-Scan* na *MRI* iwe palepale hospitali inakuwa nje tu yaani nje ya Muhimbili au nje ya Agha Khan lakini ni mahali ambapo panajulikana kwa kifupi kwa mfano inaweza ikawa tu ni XYZ *Diagnostic Centre* ambapo ukiingia pale hapafanyiki kitu kingine isipokuwa *Diagnostic* tu za mambo mbalimbali kuanzia *Laboratory* na masuala ya CT-*Scan*, *MRI* na vipimo vingine vinavyofanana na hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu vipimo hivi kama alivyosema msemaji aliyetangulia ni vipimo vya ghali sana kwa maana ya mashine, Serikali peke yake haiwezi kubeba mzigo huu. Kwa hiyo, ninachoshauri ni kwamba *Council* hii itengeneze mazingira ya kuwezesha sekta binafsi iweze kuingia na kutoa huduma hii muhimu sana katika sekta ya afya. *Council* itatengeneza namna gani mazingira hayo? Ni pamoja na kuishauri Serikali iweke vivutio mahsusi kwa wale watakaoweza kuwekeza katika maeneo haya muhimu ya uchunguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya vivutio hivyo vinaweza vikawa ni pamoja na kutoa ruzuku kwa sababu sekta binafsi ikiingia hata Serikali yenyewe ikiwa na hivi vifaa *rates* yaani ada ambazo zinatakiwa kutolewa kwa vipimo vya *MRI* au *CT-Scan* zitapungua. Kwa hiyo, ndani ya Muswada huu katika mahali panapohusika Mheshimiwa Waziri anaweza akaona ni wapi aweke namna ya kwamba *Council* hii itasimamia utoaji wa huduma hizi katika sekta binafsi au sekta nyingine yoyote lakini itahakikisha kwamba ada zinazotozwa hazizidi kiasi fulani kwa vipimo fulani fulani. Kama itatokea kwamba ile ada itakayowekwa ni ya chini kuliko gharama za utoaji wa huduma hizo basi hapa itafutwe namna ya jinsi ambavyo Serikali itaweka utaratibu wa kutoa ruzuku kwa sababu ni huduma muhimu lakini vilevile ni huduma ghali sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwenzangu aliyetangulia amezungumza na mimi nataka nisisitize kwa kweli nilikuwa nimeliweka hili katika *notes* zangu. Ni suala la wataalam tunaowazungumzia. Wataalam tunaowazungumzia na mimi najiuliza wako wapi? Kwa sababu ni jambo ambalo ni la kawaida ukienda kwenye eneo lolote la hospitali ambapo huduma za *X-Ray* zinatolewa unaambiwa msoma *X-Ray* hayupo kwa hiyo majibu yako hayajawa tayari. Anayesoma *X-Ray* hayupo. Majibu ya namna hii yapo katika sehemu nyingi au huduma za *X-Ray* zimesimama kwa sababu yule anayeshughulikia *X-Ray* hayupo. Hii ni dhahiri kwamba wataalam wetu katika eneo hilo ni wachache sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo, Muswada wetu vilevile ungeangalia jinsi gani utatoa mamlaka na kwa kweli umetoa mamlaka katika *Council* hii ya kusimamia *training* lakini hapa ndipo tunaporudi kwenye eneo la elimu na tunatilia mkazo juu ya masomo ya Sayansi kwa sababu vijana wetu ambao tutawapeleka

kusomea maeneo ya *Radiology* kwa kweli ni lazima wawe na msingi wa Sayansi angalau wawe wamefaulu *Chemistry*, *Physics* na *Biology* ili waweze kuelewa masomo ya *anatomy* na kadhalika. Kwa kifupi msingi wa vijana tutakaowapeleka kwenye eneo hilo la *Radiology* ni wale waliosoma masomo ya Sayansi katika shule za Sekondari na sasa hawapo. Kwa hiyo, tufanye jitihada za makusudi kuhakikisha kwamba Serikali yetu kwa kupitia Muswada huu ambao tutaupitisha leo utaweka mkazo kwenye suala nzima la kuwafundisha vijana ambao ndiyo watakuwa wanashughulikia au ndiyo watakuwa wanashughulikiwa na sheria hii. Sheria hii itashughulikia mabingwa na wataalam katika masuala ya *Radiology* ambao kwa kiasi kikubwa hawapo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu hatuna huduma hizi za *Radiology* hapa nchini kwa kiasi kikubwa kama nilivyosema hapo awali na jinsi ambavyo huduma za *Radiology* kwa upande wa matibabu ni muhimu sana, ninathubutu kuiomba Serikali itafute uwezekano wa kufungua eneo hili kwa rafiki zetu. Mathalani nafahamu kulikuwa na mazungumzo na hospitali ya Apollo ya India ili hospitali hiyo ambako ndiko tunapopeleka wagonjwa wetu wengi waweze kufungua aina ile ile ya hospitali hapa Tanzania. Hiyo *Apollo Hospital* ni kubwa na ina uwezo mkubwa sana, haya mambo yote tunayoyazungumza ya *Radiology* na mambo mengine yote wao wanayo na ni rafiki zetu. Hebu tuletee mfano wa hospitali ambayo itaweza kutoa huduma zote hapa nchini ikiwa ni pamoja na eneo la *Radiology* ambako tutaweza kupata nafasi ya kuwafundisha vijana wetu *practically* kwa kuwatumia hao wenzetu wa Apollo, tuwaruhusu waje, kuna tatizo gani? Tuwaruhusu waje wafungue hiyo hospitali hapa Tanzania, hayo mambo yote ya *Radiology* watakuja nayo na vijana wetu watapata mahali pa kujifunzia na sisi tutapata mahali pa kutibiwa hapa hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliona hili niliweke hapa ndani kwa maana ya kusisitiza tu kwamba hatuna uwezo lakini uwezo wa kutoka nje upo na wapo tayari kutusaidia tuuchukue kwa masharti ambayo kwa kweli yanakubalika. Tuzungumze nao, wakija hao tutapata mahali pa kufundishia vijana wetu somo zima hili la *Radiology* na sisi wagonjwa, wananchi wa Tanzania tutapata mahali pa kuweza kupata tiba yenye uchunguzi wa uhakika hapa hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa tu kusisitiza tena katika yale maeneo ambayo sisi wenyewe tunayo. *Council* hii itusaidie kuhakikisha kwamba kwenye upande wa *training* hatufundishi tu wapiga picha na wasoma picha, tufundishe vilevile vijana ufundi wa kuweza kuziangalia hizo mashine maana hizo mashine zinafanya kazi muda mrefu na zinachoka haraka kwa hiyo zinahitaji kuangaliwa mara kwa mara ili ziweze kuendelea kutoa huduma hii muhimu ambayo tunaizungumzia katika hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kutoa mchango wangu katika hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwanza kabisa mnasikia kelele inayoudhi humu ndani. Taarifa tulizonazo ni kwamba walikuwa wanaweka bati vizuri huko juu. Hawakuliweka bati hilo vizuri upepo unapita ndiyo unaosababisha kutikisika

namna hiyo. Kwa hiyo, hatua zinachukuliwa, nadhani mnasikia sauti inayoudhi katika kusikiliza.

Lakini la pili, mwezi uliopita tulikuwa kwenye Mkutano wa Wabunge wa Jumuiya za Madola, *Commonwealth Parliamentary Association* kule India. Tuliambiwa kabisa kwamba ile hospitali ya Apollo ilikuwa imeshaleta wazo la kuja kufanya kazi hapa Tanzania badala ya kuwapeleka wagonjwa wengi sana kule. Siku moja nilikwenda pale hospitalini kuwaona wagonjwa nikamkuta na Mheshimiwa Juma Kaboyonga na wengine zaidi ya 20 wakiwa wamelazwa pale. Kwa kweli walisema walishaleta *proposals*. Nadhani Serikali inalifanyia kazi na ni vizuri ikalifanyia kazi upesi kwa sababu kuwapeleka wagonjwa kwa mara moja tu ndege nzima inajaa wagonjwa kwenda Apollo wakati wenyewe wanasema hizo huduma wangeweza kuzifanyia Tanzania, inasikitisha. Hilo ni moja ya jambo tulilolipata tulipokwenda kule kama Wabunge katika *Commonwealth*.

Tunaendelea na msemaji anayefuata, Mheshimiwa Magdalena Sakaya.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia Muswada uliopo mbele yetu. Kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama, naomba nami niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa salamu za pole kwa familia na wananchi wote wa Mkoa wa Kilimanjaro kwa msiba mzito uliotupata wa Mheshimiwa Salome Joseph Mbatia. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi na awasaidie ndugu zake wote na familia yake waweze kuwa na moyo wa ustahimilivu, amen.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nimpongeze Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii pamoja na wataalam wake wote kwa kuandaa Muswada huu na kuweza kuuleta hapa Bungeni ili tuweze kutoa michango yetu. Muswada huu ni muhimu sana tukitambua kwamba uchunguzi katika afya ya binadamu ni tiba ya kwanza kabisa inayomwezesha Daktari kuweza kutoa tiba sahihi baada ya kujua kwa usahihi mgonjwa anaumwa kitu gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kwenda moja kwa moja kwenye Muswada kwa kuangalia kifungu 24 ambacho kinahusu wataalam wanaotakiwa kusajiliwa kuweza kuwa kwenye *Council* ya wataalam wa *Radiology*. Kwenye kifungu chote hiki hapa Mheshimiwa Waziri amesema kwamba *Radiology Officer* anatakiwa awe ni *Diploma holder*. Ningependa kujua ni kwa nini Waziri ameanzia *Diploma holder* kwa sababu ninafahamu kwamba uchunguzi ni kitu ambacho kinahitaji mtu ambaye ana *qualification* ya hali ya juu. Kwa nini tusingeanzie na *Degree holder* kwa sababu ni *Council* muhimu kwa afya za watu? Kwa hiyo, ningeshauri na kupendekeza pamoja na kuwa watu wenye fani hii ya *Radiology* wapo wachache lakini tuanze na watu wenye *degree* halafu hao wengine labda wenye *Diploma holder* wawe ni *Assistant Radiology Officers* ili tuweze kupata wataalam wenye uhakika kwenye fani hii ya *Radiology*.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kuhusiana na hii huduma ya *Radiology*. Huduma hii kwa hapa Tanzania Hospitali nyingi sana haipo labda ni kwenye hospitali kubwa za Mikoa na Wilayani hospitali chache lakini katika hospitali nyingi sana huduma hii haipo na hata pale ilipo inatolewa kwa wagonjwa wachache sana. Mfano, ni hospitali ya Mkoa wa Dodoma, ukienda kwenye *Ultra-Sound* wanasema mashine yao ina uwezo wa kutoa vipimo kwa watu wachache tu kwa siku labda watu watatu, wanne, watano na baadaye wanasema kwamba huduma hii imesitishwa na ni mpaka ujiandikishe tena kwa ajili ya siku inayofuata. Kwa hiyo, ningependa sana sambamba na kuboresha huduma ya afya basi Serikali ijitahidi sana kuweza kuweka vyombo vya kutosha kwa ajili ya huduma hii ya *Radiology*. Kwa kweli hospitali kubwa kama ya Dodoma kuwa na uwezo wa kupima watu watatu au wanne halafu wengine mpaka kesho yake unaweza kuona ni jinsi gani ambavyo wagonjwa wengi wanakosa huduma hii ambayo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kuhusiana na wataalam kwenye fani hii. Kama walivyozungumza wenzangu, wataalam kwenye huduma ya *Radiology* ni wachache sana wakati mwingine inalazimu mgonjwa kutibiwa bila kupewa kipimo. Pia wataalam wanaotumiwa kwa sasa hivi wanakuwa hawana ule ujuzi wa kutosha. Wakati mwingine inalazimu mgonjwa kufanya vipimo katika hospitali mbili au tatu tofauti kwa sababu nyingine vipimo vinavyotolewa kwa kweli vinakuwa siyo vya uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mifano hai na halisi kabisa. Kuna mama mmoja mjamzito ambaye amewahi kupata *High Blood Pressure* kwa sababu amefanya kipimo kwenye hospitali moja akapewa majibu ambayo siyo sahihi, akaambiwa mtoto amegeuza miguu chini akaenda hospitali nyingine akaambiwa mtoto amekaa upande. Baada ya kufanya vipimo katika hospitali mbili tofauti akawa amekuwa *confused* kabisa. Nilimwambia aende hospitali moja ya *private* Dar es Salaam. Alivyofika kule akapewa vipimo ambavyo ni vya uhakika pamoja na kuwa ilikuwa ni hospitali ya *private* yule mama *pressure* yake ikaweza kutulia na akaweza kujifungua mtoto wake salama. Kwa hiyo, hii ni dhahiri kwamba kwa sasa hivi vipimo vyetu kwenye hospitali zetu siyo vya uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri na Wizara wahakikishe kwamba wataalam japo kuwa wapo wachache kwa sasa hivi lakini waweze kutoa majibu ambayo ni sahihi vinginevyo wanaweza kusababisha magonjwa mengine juu ya ugonjwa ambao wanaenda kutafuta utatuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni gharama kuhusiana na hii huduma. Ni wagonjwa wengi sana wanaoshindwa kupata huduma hii kutokana na gharama kubwa. Sasa ningependa Mheshimiwa Waziri ajitahidi pengine gharama zinakuwa kubwa kutokana na kwamba labda huduma zenyewe ni chache au vifaa vyenyewe vipo vichache, mimi sielewi lakini ni watu wachache ambao wanaweza kumudu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama walivyozungumza wenzangu, ningeomba sana Mheshimiwa Waziri ahakikishe huduma hii iweze kuwa *affordable* kwa sababu ni watu wengi sana ambao hawawezi ku-*afford*. Ukienda kwenye *Government Hospitals* mtu

mmoja anaambiwa atoe Sh.20,000/= kwa ajili ya kupata *X-Ray,* ni wagonjwa wangapi wenye uwezo wa kutoa Sh.20,000/= ili waweze kupata hicho kipimo? Ni wachache sana. Kwa hiyo, unakuta kwamba mtu mwingine anashindwa kwenda kupata hicho kipimo *simply* kwa sababu hana uwezo wa kuchangia na matokeo yake ni kwamba hawezi kujua anachoumwa anabakia kuugulia nyumbani na matokeo yake tunapoteza nguvu kazi ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine kutaka kujua sambamba na Muswada ulioletwa, Serikali imeandaa mpango gani wa kuhakikisha kwamba vijana wengi wanasomea fani hii? Kwa sababu wataalam ni wachache, kuna utaratibu gani umeandaliwa kuhakikisha kwamba vijana wengi wanasomea fani hii? Kwanza, waipende na waisomee ili tuweze kuwa na wataalam wa kutosha tukijua kwamba uchunguzi ukitolewa vizuri kwenye vipimo unampa Daktari nafasi nzuri ya kuweza kutoa tiba nzuri na hivyo Watanzania kuweza kupata tiba inayostahili kwenye magonjwa yanayotusumbua na hivyo kuweza kuhakikisha nguvu kazi ya Taifa inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, yangu ni hayo machache, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. DR. OMARI M. NIBUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia hoja hii iliyopo mbele yetu ya Muswada wa *The Medical Radiology and Imaging Professionals.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kuchangia, naomba niungane na wenzangu walionitangulia kutoa salamu zangu za rambirambi kwa familia ya Marehemu Salome Joseph Mbatia kwa kifo kilichotokana na ajali na tunawaomba ndugu zake wawe na subira kwa hili jambo lililotokea na ambalo pia limetugusa na sisi wote kama Wabunge.

Lakini pia napenda nitoe salamu zangu za rambirambi kwa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wenzetu ambao wamefiwa kwa mfano Mheshimiwa Mustafa Mkulo ambaye alifiwa na mama yake mzazi, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed ambaye alifiwa na mama yake mzazi lakini pia ndugu yetu Mheshimiwa Yono Stanley Kevela ambaye alifiwa na watoto wake wawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia naomba nitoe pole kwa wale Waheshimiwa Wabunge wote waliopata ajali kwa namna moja au nyingine kama ndugu yetu Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir, Mheshimiwa Prof. Juma Kapuya na pia Waheshimiwa Wabunge wengine kama dada yetu Zaynab Vulu na wengine ambao walipata ajali. Nawaombea kwa Mwenyezi Mungu wapate afya njema ili warudi tusaidiane katika kuendesha gurudumu hili la Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kwanza nimpongeze Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii pamoja na Naibu Waziri wake lakini na wataalam waliowasaidia katika

kuleta Muswada huu hapa Bungeni. Muswada huu ni muhimu na dhamira ya Muswada huu kikubwa mno ni kuwasimamia wataalam wa *Radiology* katika kutekeleza majukumu yao hasa katika kudhibiti mionzi isilete madhara kwa watumiaji wa huduma hii kwa maana ya wagonjwa. Hili ni jambo la msingi sana kwa sababu hiyo mionzi ikitumiwa ovyo ovyo inaweza ikaleta madhara makubwa katika mwili wa mwanadamu kwa sababu hiyo mionzi ina nguvu na katika kuleta Muswada huu wa kuwasimamia wataalam ni wakati muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tunaposema kuwasimamia wataalam katika kudhibiti hiyo mionzi kama walivyosema wenzangu walionitangulia ni kwamba kwanza wataalam tuliokuwa nao katika fani hii ya *Radiology* ni wachache sana utakuta hata katika hospitali za Mikoa, Idara ya *X-Ray* unaweza kukuta kuna wataalam wawili pengine mmoja na wasaidizi tu wachache. Sasa tunaposema kusimamia maana yake hatokei mtu mwingine kutoka Wizarani au wapi aende akasimamie katika hospitali kwa maana wanaosimamia ni wale wataalam ndani ya zile hospitali na wakijua madhara ya mionzi hii itasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hospitali zetu nyingi nchini hapa kama nilivyosema zina wataalam wachache na baadhi ya hospitali zinatumia wahudumu wazoefu katika Idara hizo kufanya shughuli hii kitu ambacho ni hatari sana. Ni hatari kwao wenyewe wanaotoa huduma hii lakini pia ni hatari kwa wale wanaowapa huduma kama nilivyosema kwamba mionzi ni hatari.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe tu ushauri kwamba Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa wakati huu walioleta Muswada basi iende sambamba pamoja na kuwapatia elimu ya kutosha hao watumishi wanaofanya kazi katika kitengo hiki cha mionzi kwa maana ya *X-Ray*, *CT-Scan* na kadhalika ili waweze kujua lile wanalolifanya lakini pia kutoa huduma bora kwa wagonjwa ili wagonjwa waweze kupata huduma inayofaa na wenyewe pia wakijilinda wakijua kwamba wanapofanya kazi hiyo kwamba kazi hiyo ina madhara kiasi gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ningependa hiyo iende sambamba pamoja na vifaa vinavyotumika katika Idara hiyo ya Mionzi. Zipo hospitali hazina vifaa kabisa na unaweza kukuta pengine nyingine zina *apron* moja tu ya mpira ya kuzuia mionzi ili isiweze kumpata lakini watumishi wanaofanya kazi pale ni wengi pengine watatu, wanne, watano, lakini pengine ule mpira upo moja tu ambao pengine akiuvaa mtu mmoja wengine wanakuwa hawana. Kwa hiyo, kwa kadri siku zinavyoenda wakiendelea kufanya kazi katika Idara ile maana yake wanaendelea kupata athari za mionzi kidogo kidogo na baadaye watapata matatizo makubwa ikiwa ni pamoja na saratani. Ningeomba Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ilichukulie jambo hili kwa uzito unaostahili kuhakikisha kwamba Idara hii ya *X-Ray* au Idara ya Mionzi wanapata vifaa vya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama walivyosema wenzangu walionitangulia kwamba Idara hii ina wafanyakazi wachache. Kwa nini wanakuwa wachache? Nafikiri wataalam wengi wanaokwenda kusomea masomo ya afya hawapendi kuingia katika Idara hii kwa sababu haina motisha. Kwa hiyo, kutokana na uzito wa jambo hili, kwanza mtu

akijua kwamba anaenda kufanya kazi ya hatari na nyeti lakini motisha ni ndogo kwa maana wanapata mshahara mdogo pia hawapati *incentive* kama *risk allowance* ambapo zamani zilikuwa zikitolewa kwa wale wafanyakazi waliokuwa wanafanya kazi katika mazingira magumu yaani mazingira ya hatari. Kwa hiyo, hao watu kusema kweli wanaji-*expose* kwenye hatari siku hadi siku lakini mtu anaona hakuna chochote atakachopata matokeo yake anaona afadhali akasomee kitu ambacho anaweza akapata kidogo manufaa zaidi ya hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninamwomba Waziri kwa vile ananisikia walichukulie jambo hili kwa uzito unaostahili kwamba hao wafanyakazi wa Kitengo cha Mionzi ni wafanyakazi wanaofanya kazi katika mazingira ya hatari. Kwa hiyo, vilevile wangeweza kupata motisha na si motisha tu ya kupata fedha pekee lakini hata aina ya vyakula kwa mfano wangekuwa wanapewa maziwa na vitu vingine ili angalau kujaribu kujikinga na hatari za kushambuliwa na mionzi hiyo ya *X-Ray*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara hii ya Mionzi ni Idara ambayo kama nilivyosema mwanzo inahitajika kuangaliwa kwa makini ikiwa ni pamoja na majengo yake yawe ni ya aina ya fulani kutokana na kuhakikisha kwamba mionzi hiyo haiwafiki watu wengine walio karibu na vyombo hivyo vinavyotumika. Utakuta kuna sehemu nyingine pengine mashine za mionzi wagonjwa wengine ambao hawahusiki na upimaji wa mionzi hii wapo karibu sana kiasi kwamba na wenyewe wanapata hatari bila kujua.

Kwa hiyo, ninashauri pia katika hospitali zetu kabla ya shughuli hizi hazijaanza siku hadi siku iwe inatolewa elimu ya afya kwa hao wagonjwa ambao wanakuwepo katika sehemu hizo za kutolewa huduma za mionzi ili wajue hatari zake. Kwa sababu binadamu huwa anaona tatizo lile ambalo linamgusa kwa wakati ule lakini kwa sababu mionzi hiyo inapo-*affect* mtu hakuna maumivu ya wakati huo, kwa hiyo, mtu hawezi kujua athari zake lakini kumbe siku hadi siku utakuta mtu yule anaathirika bila kujua na baadaye atapata magonjwa mabaya kama magonjwa ya saratani.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hii ni pamoja na wafanyakazi wengine katika Idara ya Afya ambao kwa namna moja au nyingine na wenyewe wanahusika ingawaje siyo moja kwa moja lakini wanahusika kwa namna moja au nyingine na mionzi hiyo. Kwa mfano, Wauguzi ndani ya hospitali wao shughuli zao za siku hadi siku huwachukua wagonjwa kwenye wodi kuwapeleka kwenye Idara ya Mionzi kwa ajili ya kupata vipimo vya *X-Ray*, *Ultra Sound* na *CT-Scan*.

Kwa hiyo na hao Wauguzi wenyewe pia wanapata matatizo siku hadi siku bila wao kujua. Kwa hiyo, nashauri Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ilichukulie jambo hili kwa uzito unaostahili ili wahusika wote waweze kupata elimu ya kutosha kuhakikisha kwamba watu hawapati madhara kutokana na mionzi hiyo ambayo tunaizungumzia hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri kwa kuzingatia jambo hili ni vizuri Wizara husika iongeze Vyuo kwa ajili ya wafanyakazi wa Idara ya Mionzi au kupanua wigo wa Vyuo hivyo ili waweze kupata elimu ya kutosha. Ingawaje sikubaliani na mzungumzaji aliyepita kwamba kutokana na uzito wa jambo hili kwamba wataalam hao wangeanza na

*level* ya *degree*. Nafikiri haitakuwa rahisi kwa sababu katika nchi yetu bado hatujawa kwanza na wataalam wa kutosha kwa ajili ya kuwahudumia Watanzania waliokuwa wengi. Kwa hiyo, kwa *level* hiyo ya *Diploma* ambayo ameiwasilisha Mheshimiwa Waziri nakubaliana nayo isipokuwa tu ni kwamba hatua za makusudi zichukuliwe ili kusudi na wengine waweze kupata nafasi ya kupata elimu kuanzia *Diploma* na kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia katika Muswada huu wa *The Medical Radiology and Imaging Professionals,* nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Ningependa pia kuungana na wenzangu kutoa pole na rambirambi zangu kwa niaba ya wapiga kura wangu wa Mkoa wa Morogoro kwa familia ya marehemu Mheshimiwa Naibu Waziri Salome Joseph Mbatia na kwa Serikali na kwa wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro ambao wamempoteza kiongozi wao shupavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa pia nichukue nafasi hii kuwapa pole Waheshimiwa Wabunge wenzangu ambao wamepata ajali katika kipindi hiki kilichopita. Tunaomba Mwenyezi Mungu awasaidie waweze kupona kwa haraka. Nawapa pole pia ndugu zetu Waheshimiwa Wabunge ambao wamepoteza ndugu zao kwa njia mbalimbali. Lakini ningependa kusema kwamba ninawapa pole na ninawaombea wote waliofariki Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi, Amen.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii kwa kuleta Muswada huu hapa Bungeni. Muswada huu umekuja kwa wakati muafaka ambapo watu wengi wanakuja nchini kuwekeza kwenye sekta ya afya. Wanapokuja kuwekeza wengine wanakuja na wataalamu wao ambao wana viwango na wasiokuwa na viwango. Ninaamini sasa kwamba Serikali imeona Watanzania tunahitaji pia kupata huduma nzuri na sio watu wanakuja kufanya biashara kutokana na matatizo yetu, kwa hilo naunga mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachopenda kuzungumzia hapa ni kidogo tu. Ibara ya 46 kwenye *miscellaneous provision* amezungumzia juu ya *offences and penalties*. Katika hospitali zetu kwenye ngazi ya Wilaya na Mikoa tuna *radiographers* ambao ni *Assistant Radiographers* hawawezi kusoma picha zetu wanaosoma ni Madaktari wa kawaida, hata mimi nasoma, Mheshimiwa Nibuka anasoma na *Physicians* wanasoma na wataalam wengine ambao sio *Radiographers*. Sasa nimepitia Muswada huu sijaona *provision* ambayo inaturuhusu sisi ambao sio *Radiographers* kuweza kusoma na kuweza kupata kinga kutokana na hii hapa kwamba naweza nikasoma mimi kama Daktari ambaye sio *Radiographers* na ndio tuliyo wengi ambao tunasoma picha za wagonjwa *especially* kwenye *accidents*, kina mama wajawazito na kwenye kutoa *diagnosis* ya *tuberculosis*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa imefika hapa kwamba wananchi wanaelewa sana siku hizi wakaona kwamba labda wewe ulivyotoa *diagnosis* yako haikuwa na usahihi sana, lakini sisi tunapotoa *diagnosis* angalau inatupa *guidance* kwamba huyu mgonjwa

tumsaidie kwa namna gani, *we don't go into very minute, you know observations* ile inafanyika na *Radiographer* lakini sasa kwa sababu hatuna njia nyingine ni lazima sisi Madaktari wa kawaida tuendelee kusoma picha za wagonjwa *especially* kwenye *accident* kwa akinamama wajawazito, wagonjwa wa TB hiki kifungu cha sheria hapa kinaanza kutufunga mikono.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri aangalie namna ya kutoa marekebisho ili kuwepo na *profession* ya *Medical Practitioners* ambao ni Madaktari wanaowahudumia wagonjwa waweze kutumia utaalam wao walionao ambao wamesoma kidogo kwenye *Medical Schools* namna ya kusoma picha za *Radiograph* pamoja na picha za *Ultrasound* ili waweze kufanya hiyo kazi bila wasiwasi wa kwamba tumefungwa na kifungu cha sheria ukikosea kidogo hawa wenzetu wa *Medical Radiology Council* watakuja kutukamata na kutufunga au kutupiga faini. Naomba hilo liwe wazi ili Madaktari wetu wasiogope mpaka hapo tutakapoweza kuwa na *Radiographer specialists* kwenye kila Hospitali mpaka kwenye ngazi ya Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina mengi ila napenda kusema tu kwamba Muswada huu ni mzuri kama utatekelezwa na lingine ni kwamba vyeti vya wale wanaokuwa *trained* nje na anaotoka nje na wataalam wanaokuja kwenye *Private Hospitals* pia vihakikiwe kama wanasema wana digrii na *High Education Accreditation Committee* kwa sababu naona *Radiographers* peke yao kwenye hii *Council* hawataweza kupitia na kuona kwamba vile vyeti vina uhalali kweli na kama kweli hivyo Vyuo Vikuu vipo. Mwenye kufahamu Vyuo Vikuu ambavyo ni *real accredited* ulimwenguni itakuwa ni *Higher Education Accreditation Committee* ambayo ipo. Sasa ninapenda kushauri kwamba kama inawezekana basi kuwepo na *representation* kwenye hii *Council* ya mtu wa *High Education Accreditation Committee*. Huu ni ushauri nimetoa kwa nia njema na ninaomba kuunga mkono hoja kwa asilimia kwa mia, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Sina wasemaji wengine. Kwa hiyo, nimwite mtoa hoja aweze kutoa ufafanuzi katika mjadala huu.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii kwa mara ya pili ili niweze kuhitimisha hoja niliyoileta hapo awali.

Napenda nitoe shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamepata nafasi ya kuchangia ama kwa kuzungumza au kwa maandishi. Maoni yao tutayazingatia katika utekelezaji na pale itakapobidi katika kurekebisha sheria. Kama ilivyo ada, naomba nianze kuwatambua waliochangia. Kwanza wale waliopata nafasi ya kuzungumza hapa Bungeni ni Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, ambaye ni Makamu wa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu, Mheshimiwa Omar Ali Mzee aliyezungumza kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Dr. Mzeru Nibuka na Mheshimiwa Dr. Lucy Sawere Nkya, mwanafunzi wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, waliochangia kwa maandishi ni hawa wafuatao. Mheshimiwa Hemed Mohamed Hemed, Mheshimiwa Janet Bina Kahama, Mheshimiwa Lucy Nkya tena na Mheshimiwa Saverina Mwijage. Nawashukuru kwa kuuboresha Muswada wangu na naomba nipitie baadhi ya hoja ambazo zimetolewa na wachangiaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutoka Kamati za Huduma za Jamii, Mheshimiwa Haji Mwita Haji ameonesha vipengele mbalimbali ambavyo vilionekana vinahitaji kuboreshwa na nafurahi kusema kwamba vyote vimeboreshwa na yale yaliyozungumzwa yako katika jedwali la marekebisho. Alitushauri vile vile kwamba tuongeze vifaa katika hospitali na vile vile kuhakikisha ubora na hii imejitokeza tena wenzetu wengi wamezungumza kuhusu uchache wa vifaa na kwamba hospitali nyingi hazina vifaa na vile vile hivyo vifaa vinaharibika mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusema kwamba hivyo vifaa ni gharama na tunakwenda pole pole na sasa hivi kama Serikali tumefikia hatua ya Wilaya. Tumekuwa na mradi wa *ORET* ambao tulishirikiana na Waholanzi uliotuwezesha kupeleka vifaa vya *X-ray* na *Ultra-Sound* katika Hospitali zote za Wilaya na kipaumbele sasa hivi tunakitoa kwa Wilaya mpya ambazo na zenyewe zikiwa na jengo linalokidhi kuwa na mionzi basi na kwenyewe tunapeleka, utaratibu huo bado unaendelea.

Lakini vile vile ili kuhakikisha kwamba hivi vifaa vinadumu, tunao mkataba wa watu wa *Phillips* ambao ndio wataalam, vifaa vyote ni vya *Phillips* ili wafanye *preventive maintenance*. Kila mwaka wanazungukia Hospitali kwa muda maalum. Nina imani kama mara mbili kwa mwaka kwa sababu hatutaki kungojea mpaka mashine inawekwa juu ya mawe ndio tuanze kutafuta mtu. Lakini inapoharibika kabla hawajapita *round* basi hapo ndipo tunawatafuta kwa dharura lakini utaratibu huo wa *preventive maintenance* tumeusimamia si kwa vifaa hivyo tu lakini hata kwa vifaa vingine.

Mheshimiwa Slaa ulizungumzia habari za vifaa vya *Ocean Road*. Ni kweli ni vifaa vya siku nyingi na jinsi tunavyochoka hata binadamu unahitaji *maintenance* ya mara kwa mara. Lakini niseme kwa kushirikiana na *International Atomic Energy Agency* tumepata mashine ya gharama ya Sh.2mil ambayo tunafanya utaratibu wa kuizindua na tutategemea kwamba Mkuu wa Nchi ndio ataizundua mwezi Januari.

Mheshimiwa Omar Mzee alizungumzia habari za gharama …

**NAIBU SPIKA:** Waziri umesema milioni 2 au?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Bilioni 2, samahani.

**NAIBU SPIKA:** Tukaona kazi hii! (*Kicheko)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Omar Ali Mzee wa Kambi ya Upinzani amezungumzia habari za gharama ya matibabu haya na hii imezungumziwa vile vile na Mheshimiwa Dr. Slaa na Mheshimiwa Sakaya. Ulikuwa ushauri tu kwamba gharama ilivyo kwa sasa hivi ni kubwa na Serikali ikashauriwa

kwamba iangalie namna ya kupunguza. Nadhani gharama zilizokuwa zinazungumzwa katika huduma hizi maalum ni za *CT-Scan* au *MRI*.

Mheshimiwa Slaa labda unajua kwamba *MRI* tuliipitisha hapa fedha yake ni Sh.4bil ambapo tumeshainunua bado kui-*fit* tu na ni kweli ni kipimo ghali na wagonjwa wengi wakienda nje wanakwenda kufanyiwa hicho kipimo ndio waendelee ambapo tungekuwa na majibu hapa hapa tungepunguza gharama. Nachukua ushauri wa Mheshimiwa Slaa kwamba *CCBRT* ambapo yeye ndiyo Mwenyekiti wa Bodi wana utaratibu wa kuwatoza zaidi wale wenye uwezo lakini nadhani hata *MOI* wanayo, unatoza kwa pale wanapokaa lakini kwa huduma tungependa iwe sawa mtu asije akafikiri kwamba kwa sababu unalala *grade one* basi na huduma iwe bora zaidi, hiyo tena ndiyo itakayoweka tabaka. Lakini ukisema kwamba kwa sababu unataka kukaa kwenye chumba ambacho kinajitegemea basi utalipa zaidi sawa sawa na hoteli unaweza ukachukua *suite* au ukachukua chumba kidogo. Kwa hiyo, huu utaratibu tumeuanzisha *MOI* karibu asilimia 25 ya *OC* yao inatokana na utaratibu huu. Kama ulivyosema hii fedha tunayopata inasaidia wale ambao hawana uwezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeambiwa kwamba wataalam ni wachache na ukaongeza Mheshimiwa Dr. Slaa na hata wachangiaji wengine kuuliza kwamba wako wangapi na tuna mpango gani? Ma-*radiographer* walioko kazini ni takriban 200 kwa nchi nzima. *Radiologist* wapo 20, Vyuo vya *Radiographers* tunavyo viwili hapa Muhimbili na Bugando na Vyuo vya Ma-*Radiologist* ambavyo ni vya Vyuo Vikuu ni *KCMC* na Muhimbili. Nakubaliana na wote mliozungumza habari za uchache lakini uchache wa wafanyakazi wa sekta ya afya kama nilivyosema jana una *cut across,* ni uchache karibu kila mahali. Ni kweli kuna maeneo mengine ambako uchache ni mkubwa zaidi kuliko mahali pengine lakini kama nilivyosema jana ni katika huu mpango ambao uko mbele yetu huu wa *MAAMU* suala la kuongeza wafanyakazi ni kitu ambacho kimepewa kipaumbele cha kwanza. Mpango huu ni wa miaka 10 kuanzia mwaka huu wa fedha vipindi viwili vya miaka mitano mitano na mambo ambayo mmesikia mara kwa mara ni kwamba vile vile tungependa kuongeza vituo vya kutolea huduma ambavyo pia ni vichache.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka huu hamjatusikia tukienda kunadi hii sera ya kujenga *dispensary* au *health centres*, tumejikita kwanza katika kuongeza wataalamu. Tulichofanya moja ni kuimarisha vyuo ambavyo tunavyo. Kuna vingine tulivifunga, tumevifungua sasa. Mheshimiwa Savelina anajua kule kwao Chuo cha Kagemu kimefunguliwa, kuna kingine kiko Mpanda, lakini tunataka kuimarisha hivi vilivyopo kwanza kabla hatujafungua vingine. Nia ni kuongeza idadi ya vijana ambao tunawasaili na kama nilivyosema jana ni kwamba mwaka huu tumeongeza usaili kwa asilimia 40. Kwa hiyo, tutakuwa tunaongeza hivyo hivyo mpaka hapo tutakapoona tunajitosheleza labda hiyo kasi ndio tutaipunguza kidogo.

Mheshimiwa Kaboyonga na wengine wamezungumzia kwamba uchunguzi ni muhimu na kweli ni muhimu. Kupata *diagnosis* ndio mwanzo wa kupona kwa mgonjwa vinginevyo utakuwa unabahatisha tu. Dawa zinapatikana karibu kila mahali lakini kama

hujafanya utambuzi ni nini kinamsumbua mgonjwa itakuwa ni pata potea tu. Kwa hiyo, hilo na sisi tunalijua na tunaliona.

Alizungumzia pia kukosekana kwa *Ultrasound. Ultrasound* ziko kila Hospitali za Wilaya, *CT-Scan, MRI* kusema kweli ni vichache. Utaratibu tulionao kwa sasa hivi ni kwamba tunapopeleka mgonjwa India kama tumefanya vipimo vya *laboratory* au *X-ray* tunawapelekea hivyo vipimo kwa njia ya *Tele medicine* na wenyewe wanajua huyu mgonjwa anayekuja wategemee nini na wakati mwingine wanatushauri hapo hapo kwamba mfanye kipimo kingine zaidi ili na wenyewe wajitayarishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia alitushauri kwamba tuweke mazingira ili sekta binafsi ije. Mazingira yapo na ukweli ni kwamba Tanzania tunasifika kwa kuwakaribisha na kuwavutia watu kutoka nje. Tunaambiwa kwamba inachukua wiki au wiki mbili kwa mtu kuleta maombi yake kama anataka kuwekeza mpaka anapata jibu. Hili ni suala ambalo tunaendelea kujitahidi. Kwa hiyo kama unamfahamu mtu ambaye ana nia ya kuja kufanya kazi kama hiyo sisi tutafanya kazi naye bega kwa bega ili kufanikisha suala hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia alizungumzia suala la Apollo. Ni kweli hata hapa Bungeni tumewahi kujibu swali linalohusu mahusiano kati ya Serikali na hiyo Hospitali ya Apollo iliyo *New Delhi* ambako tunapeleka wagonjwa wetu wengi. Nia ni kwamba tuweze kuwavutia wajenge kitu kama kile hapa nchini ili ipunguze idadi ya wagonjwa tunaowapeleka kule lakini vile vile tuweze kuwafundisha vijana wetu. Labda ni ripoti tu kama tulivyojibu swali moja hapa na pia kwa kusisitiza kwamba sekta binafsi ni muhimu katika kutoa huduma hapa nchini, huu uhusiano ni kati ya Apollo Hospitali na NSSF. NSSF ikiwa sekta binafsi ndio wameingia nao mkataba na ninavyojua wako katika hatua ya kusaini *Memorandum of understanding.* Kwa hiyo Apollo hatujawatupa, wanatusaidia sana kutibu wagonjwa na labda Mheshimiwa Kaboyonga nawe ulipelekwa huko na mategemeo yetu ni kwamba utaalam walionao tungependa tuupate hapa.

Mheshimiwa Sakaya alisema kwamba huu Muswada ungeanzia juu kidogo yaani kuwatambua ni wepi tuwaingize katika usajili huu na hili lilijitokeza jana vile vile tulivyokuwa tunazungumzia habari za *health professionals.* Kama alivyosema Mheshimiwa Dr. Nibuka ni kwamba Ma-*Radiographer* tulionao ni wachache, Ma-*Radiologist* ni wachache, lakini ukiangalia kazi wanazofanya zinatofautiana tu ule uwezo *Radiologist* anaweza akafanya mambo zaidi kuliko *Radiographer*. Lakini pia pale wanapohitimu wote wanakula kiapo, hapa suala la maadili limesisitizwa sana, wote wanakula kiapo kwamba watafanya hiki hawatafanya kile. Ina maana basi kama tutasema hawa tumeteremka mno basi itabidi tuwe na sheria mbili. Kwa sasa tunadhani muda haujafika tutakuwa na hii sheria moja hapo itakapobidi tukiona mambo ambayo yako *very specific* yanajitokeza kwa wingi katika kundi fulani la hawa wataalam basi tunaweza tuka *amend* sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulisema Hospitali nyingi hazina mashine, nadhani hilo nimelijibu, mashine ni ghali lakini kila Wilaya ina *X-ray*. Suala la gharama pia limejitokeza, ni kweli gharama za *X-ray* ni za kawaida sio kubwa sana, lakini gharama za *CT-Scan* na *MRI* zinakuwa kubwa kwa sababu ya vitu unavyovitumia, *expendables,*

ndiyo maana gharama inakuwa ghali lakini inapokuwa ya Serikali gharama inakuwa nafuu. Ukiangalia *CT-Scan* ya Muhimbili ukilinganisha na ya hospitali nyingine ya Aga Khan bei ni vitu viwili tofauti. Kwa hiyo tunachojaribu ni kwamba hivyo vifaa viwepo wakati wote kwa sababu bei inaweza ikawa nafuu lakini unakuta vifaa fulani havipo basi mgonjwa tena analazimika kwenda huko.

Mheshimiwa Mzeru Nibuka amesisitiza elimu kwa watumishi wanaofanya kazi katika eneo la mionzi ambapo nakubaliana naye kabisa na hilo linafanyika. Pia kuwe na vifaa vya kujikinga kama *aprons*. Haya masuala mawili ya elimu na hii *protective gears* kama *aprons* pia limezungumzwa na Mheshimiwa Kahama, ushauri tu ni kwamba tusisitize kuwepo kwa hivi vifaa na tunachukua huo ushauri.

Alishauri pia anaona kwamba watumishi ni wachache kwa sababu *incentives* hazipo na akataja *risk allowance*. Hizi *risk allowance* zilikuwepo karibu kila fani katika sekta hii sasa ilikuwa ngumu sana kui-*administer* kwa sababu kwa mazingira ya hospitali kila mahali kuna *risk* ya kuambukizwa magonjwa. Tuna watumishi wanaofanya kazi katika wodi za kifua kikuu na wao tulikuwa tunawapa, tunawapa na maziwa lakini utaona kwamba ukianza kumtibu mgonjwa mwenye kifua kikuu inachukua chini ya wiki mbili hawezi akaambukiza mtu tena. Kwa hiyo mtu ambaye yuko *at risk* zaidi ni yule ambaye anamhudumia mgonjwa kabla hajagundulika na hao wanakuwa katika *Medical Ward*. Kwa hiyo kila mmoja ana matatizo fulani katika sehemu yake ya kazi. Watu wanaofanya katika Hospitali ya Wagonjwa wa Akili wao wakati mwingine wanapigwa na wagonjwa.

Sasa ukiangalia watumishi wote wanaofanya kazi katika hospitali wana *risk* za namna fulani kwa hiyo ikaonekana afadhali ku-*standardize* kwa maana hata muuguzi akitoka wodi fulani akapelekwa wodi nyingine kusije kukawa na haja tena ya kuanza ku-*adjust*. Kwa hiyo ndiyo maana inaangaliwa kijumla kwamba tuboreshe maslahi ya hawa wafanyakazi na unajumuisha hiyo *risk allowance*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa *incentives,* ni kweli zinaangaliwa kiujumla. *Incentives* kwa watu mbalimbali wanaokwenda kufanya kazi katika maeneo magumu hili linaangaliwa kama *package* tofauti.

Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, amezungumzia kifungu namba 46 ambacho amesema sahihi kabisa kwamba vijana wetu ambao tunawafundisha katika *Medical School* hata katika shule zetu tunawafundisha kusoma *X-ray*. Kwa hiyo si lazima *X-ray* zote zikasomwa na *Radiologist*. Lakini hiki kifungu kinazungumzia *for the purpose of obtaining registration*, hakisemi kwamba usipokuwa *Radiologist* basi usisome *X-ray* pale mwishoni kinasema kwamba *making propose statement* ina maana kwamba mtu kumbe ni kihiyo asije akaanza kufikiria kwamba anaweza akapata usajili na hii Bodi, hiyo ndiyo ilikuwa mantiki ya hiki kifungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Janet Kahama ameshauri kwamba ingekuwa vizuri suala hili na lenyewe lizingatiwe Visiwani Zanzibar. Kama mnavyojua kuna sheria zinazotungwa na Bunge hili na kuna sheria zinazotungwa na Baraza la Wawakilishi. Lakini tuna mikutano ya mara kwa mara na Wizara inayohusika kule na

tunabadilishana mawazo na kazi tuliyonao sasa hivi ni kujaribu kuwashauri wenzetu ili tuwe tunazungumza lugha moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, amezungumzia habari za kinga, kwanza elimu na pia vifaa kama *aprons* viwepo na viwe vinavaliwa na vile vile ulizungumza juu ya vifaa visiharibike hii ni kwa mtu binafsi anavyoviangalia lakini pia tuwe na *preventive maintanance* ambayo nimeshaizungumzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, alizungumzia suala la nchi yetu kuanza ku-*discourage* vijana na watoto hasa wasitumie sana simu za mkononi na kwamba zinaharibu ubongo. Ni kweli yametokea maandishi mengi katika magazeti na katika vyombo mbalimbali ambapo hatujapata uhakika vinapingana. Mpaka sasa sisi kama Serikali hatujafika mahali ambapo tunaweza tukatoa *statements*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Dr. Lucy Nkya ameshauri kwamba wale waliosomea nje vyeti vyao vihakikiwe na Tanzania *Higher Education Accreditation Committee*. Nakubaliana naye kabisa na katika usajili wa hawa watu ambapo inatazama ubora na *curriculum* ni kazi ya hii *Tanzania Commission for Universities (TCU)* au *NACTE*. *NACTE* inaangalia *Diploma* na *Advance Diploma* lakini vyeti vya Shahada tunapeleka *Tanzania Higher Accreditation Committee* na ndiyo hali ilivyo.

Mheshimiwa Savelina Mwijage ametoa mfano wa kipimo mgonjwa anaambiwa alipie Sh.5,000/= cheti akishatoa fedha anakwenda kwa Daktari anaambiwa dawa hakuna ukanunue hospitali ya nje na fedha aliyokuwa nayo ni hiyo hiyo. Sasa anapenda kujua ninazungumzia nini kuhusu suala hilo? Mimi naona hilo ni *specific* kwa sababu sera yetu iko wazi lakini kama hilo limetokea nadhani inakuwa ni utendaji mbovu wa mtu binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye masuala mawili yaliyozungumziwa na Mheshimiwa Dr. Slaa. Moja lilikuwa linahusu Kifungu Na.19, habari ya Mtanzania anaye-*qualify* nje ya Tanzania. Kwanza, niseme kwamba hii sheria ni ya huku Bara. Kama nilivyosema tuna mikutano ya mara kwa mara na wenzetu wa kutoka Unguja na tunazungumza nao na sheria zingine zinaanzia kule na sisi tukiona nzuri tunaleta huku. Lakini hapa dhamana yetu ni Tanzania Bara ndiyo maana tunazungumzia hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini upo utaratibu wa *exemptions* hata baadhi yetu tuliosoma Vyuo vya Uingereza au Marekani tunahitajika kufanya mitihani lakini wakiona kwamba kinakidhi *standards* za kwao utakuta kwamba maadam una cheti cha kutoka sehemu fulani basi inakuwa ruhusa. Kama hawa watu watakuwa wamehitimu katika Vyuo Vikuu ambavyo viko chini ya Serikali ya Muungano hiyo sioni kama itakuwa na matatizo yoyote. Kwa hiyo, ninachosema hapa ni kwamba hapa tunazungumzia Tanzania *Mainland* kwa sababu hatuwezi tukazungumzia Tanzania nzima pamoja na Zanzibar kwa sababu hii sheria imefungwa mikono haivuki bahari.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nishukuru tena kwa kunipa nafasi hii na nawashukuru tena Wabunge wenzangu ambao wameweza kuuboresha Muswada wangu, ahsante sana na naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja imetolewa. Naomba niwatangazieni kwamba si mnaona hapa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Lowassa hayupo lakini badala yake Mheshimiwa Mohamed Seif Khatib, Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo ndiye sasa anayekaimu nafasi ya Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni. Mheshimiwa Chiligati naye anakaimu nafasi ya Waziri wa Nchi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hoja hii imeungwa mkono sasa tunaingia hatua nyingine, Katibu!

## KAMATI YA BUNGE ZIMA

### Muswada wa Sheria ya Wataalam wa Mionzi wa Mwaka *2007*
### *(The Medical Radiology and Imaging Professionals Bill, 2007)*

Ibara ya 1
Ibara ya 2

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila madadiliko yoyote)*

Ibara ya 3

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 4

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 5

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 6

**MHE. DR. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisimama tangu Ibara ya 5 hukuniona.

**MWENYEKITI:** Ni kweli sikukuona. Sasa naomba turudi Ibara ya 5 kwa sababu tunatunga sheria hatuwezi kuruka.

Ibara ya 5

**MHE. DR. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka kwenye kuchangia kwa mdomo nilitoa ushauri kwamba kwenye *composition* kwa sababu tunaangalia *academic qualifications*, tupate mwakilishi kutoka aidha *High Education Accreditation Committee* ama *TCU*. Sasa Mheshimiwa Waziri amezungumza vizuri lakini hakutoa maamuzi kwenye hilo. Napenda kusema kwamba kama kweli tunataka kuwa *serious* tunaangalia *academic qualifications and standards* labda hapa kwenye Ibara hii ya 5(1)(g)(k) hawa watu pamoja na kwamba mmoja ni *Radiologist* na mwingine *Radiographer* lakini *we could do* na *Radiologist* halafu tukamleta mtu kutoka kwenye *Academic Regulation* ambaye atatoa *fair judgement* na ushauri mzuri kwa *Council*. Ningependa Mheshimiwa Waziri aliangalie hilo na atoe msimamo wake yeye analionaje hilo? Ahsante.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli alichangia kuhusu suala hilo lakini vilevile alishauri kwamba vyeti vya hawa wahusika vipelekwe *Higher Education Accreditation Council* ambayo ni *TCU (Tanzania Commission for Universities)* na hilo nimesema ndivyo inavyokuwa. Sasa hapa anasema pengine atoke mtu kuja kukaa kwenye hii *Council*. Sasa tunaona nia hakuna kwa sababu hapa ni *registration* ya hawa watu na kabla hawajawa *registered* vyeti vyao vinahakikiwa na *Higher Education Accreditation Council*. Sasa kusema hii kazi anafanya kule halafu anakuwepo hapa hatuoni sababu. Lakini tunakubaliana naye kwamba hivi vyeti vihakikiwe na *Higher Education Accreditation Council* ambayo inafanya hiyo kazi kwa vyeti vyote vya watu wenye *degree* waliosoma nje ya Tanzania.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 6
Ibara ya 7
Ibara ya 8

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 9

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge*

*Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 10
Ibara ya 11
Ibara ya 12
Ibara ya 13

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 14

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 15
Ibara ya 16

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 17
Ibara ya 18

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 19

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ibara ya 19, niliuliza na Waziri alijibu vizuri sana. Lakini pamoja na maelezo ya Mheshimiwa Waziri nadhani mimi naona suala hili bado linautata. Sasa mimi ninadhani katika Ibara hii kuna dhana mbili. Dhana aliyoeleza Waziri ni dhana sahihi kabisa kwamba sheria hii inahusu Bara kwa sababu mambo ya afya ni mambo ya Bara na Zanzibar wana Wizara yao ya Afya.

**MWENYEKITI:** Yaani si Wizara ya Muungano?

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Ndiyo kwa maana ya Wizara. Lakini kwa maana ya elimu ambayo hapa ndiyo dhana inayozungumziwa inasema kabisa kwamba "*Tanzania Citizen who qualified outside Mainland Tanzania* " sasa elimu ni suala la Katiba na ni la Jamhuri. Kwa hiyo dhana iliyoko hapa ni suala la elimu si suala la *registration*. Inapofika *Registration procedure* iliyoelezwa katika hii kila mmoja ataifuata lakini inapofika suala la elimu mimi nadhani Katiba inakataza na tusingependa sisi kama

Bunge tutunge sheria ambayo baadaye inaweza kuonekana kwamba inapingana na Katiba.

Ibara ya 13 ya Katiba inaeleza kabisa ni marufuku kwa sheria yoyote iliyotungwa na mamlaka yoyote katika Jamhuri ya Muungano kuweka sharti lolote ambalo ni la ubaguzi ama wa dhahiri au kwa taathira yake. Sasa ukishatamka kwamba "*who qualified outside Mainland Tanzania*", unazungumzia "*outside Mainland Tanzania"!*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa kutumia Kanuni ya 47(2), nipendekeze kwamba utumie mamlaka yako kwa kawaida tunapobadilisha neno tunahitaji kuleta mapendekezo mapema, kwa kuwa hatukuleta na niliomba radhi tumeiona na tumechelewa, uturuhusu kulegeza Kanuni hiyo ili tuondoe neno *Mainland*. Mimi sione athari ya kuondoa neno *Mainland* katika kifungu hiki ili ibaki tu kwamba "*who qualified outside Tanzania"*. Kwa sababu tunachojadili hapa ni mtu aliyesoma nje ya Tanzania ndiyo tunataka kudhibiti elimu yake lakini aliyesoma Tanzania, akisoma Zanzibar, akisoma Dar es Salaam au Bukoba, mimi sioni ni kwanini tunamwekea mipaka ya namna hiyo?

**MWENYEKITI:** Tunajadili hapa *Attorney General* unaweza ukasaidia.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Mheshimiwa Waziri ameshalieza kwa ukamilifu kabisa. Kwa sababu sheria yenyewe hii ukisoma fungu ambalo tumeshalipitisha fungu la pili linasema "*this Act shall apply to Medical Radiology and Magic Professional in Mainland Tanzania"*. Kwa hiyo, linahusu *professionals* wa *Mainland Tanzania*. Sasa nina uhakika walipokuwa wanafikiria juu ya suala hili watakuwa wameona ni kwa sababu gani wanafikiri kwamba *professionals qualifications* ambazo zimefanyika nje ya *Mainland Tanzania* hazitakubaliwa humu ndani na ukweli ni kwamba Bunge hili lina mamlaka ya kutunga sheria kama hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 1 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inasema kwamba Jamhuri ya Muungano ni nchi moja. Ibara ya 2 ya Katiba hiyo hiyo inasema juu ya maeneo mawili ya Jamhuri ya Muungano na Ibara ya 4(3) ya Katiba inasema kabisa kwamba kwa ajili ya utekelezaji bora wa shughuli za umma katika Jamhuri ya Muungano na kwa ajili ya mgawanyo wa madaraka juu ya shughuli hizo baina ya vyombo vilivyotajwa katika Ibara hiyo kutakuwa na mambo ya Muungano kama yalivyoorodheshwa katika nyongeza ya kwanza iliyoko mwishoni mwa Katiba hii na pia kutakuwa na mambo yasiyo ya Muungano ambayo ni mambo yote mengine yasiyo ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kwenye hili suala la hawa wataalam wa *Radiology and Imaging Professionals* si suala la Muungano ndiyo sababu hii Ibara ya 19 imezungumzia juu ya kwamba mtu yoyote ambaye atapata *qualification* nje ya *Mainland Tanzania* itabidi afuate masharti ya kwenye Ibara hiyo. Ibara hiyo, kwa maoni yangu haijabagua mtu yeyote ni kwamba anatakiwa afuate tu masharti yaliyoko chini ya Ibara hiyo ya 19.

**MWENYEKITI:** *Actually* hii *paragraph*, uondoe maneno yale *foreigner* utakuta haina matatizo na ukisema "*Tanzania citizen who qualified outside Mainland Tanzania shall upon payment of prescribed fees be registered"*, ukifunga yale maneno *foreigner* pale ukasoma, unakuta kwamba inakwenda na ile *schedule* ya mambo gani ni ya *Mainland* na mambo gani yasiyo *Mainland*, haimbagui mtu ukiisoma vizuri, tuendelee kuzungumza.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani sijui kama nimeeleweka vizuri. Nilisema inapofika suala la sheria hii kuwahusu *Radiologist* kwa maana ya *registration* ya *Radiologist* ni suala la Bara yaani *Tanzania Mainland*. *Procedure* ya mtu kuomba apate *registration* imeshaelezwa katika Ibara zilizotangulia lakini unapozungumzia suala la "*Tanzania citizen who qualified"* bado tunazungumzia "*who qualified"* ni suala la Elimu ya Juu ambalo ni suala la muungano na Waziri wa Elimu hapa alikuwa ananikonyeza hapa kwamba ni kweli Elimu ya Juu bado ni suala la muungano na iko kwenye nyongeza ya Katiba, kifungu kidogo 14 cha *schedule* ya mambo ya muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama ukishakubali kwamba ni mambo ya muungano na kama tukishakubaliana kwamba aliyesoma Zanzibar au Dar es Salaam au aliyesoma Chuo Kiuu kama kitakuwepo cha Rukwa wote hawa ni watu waliosoma ndani ya muungano, kwa hiyo inapofikia suala la *Radiology* wao waende tu kwa taratibu zile zilizoelezwa za kuomba *registration* lakini hawawezi kufananishwa na *foreigner*. Tanzania ni nchi moja na lazima tujenge dhana kwamba hii ni nchi moja na kama ni nchi moja yale mambo yote yanayotuunganisha katika umoja wetu basi tuyafuate katika umoja. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaondoa dhana ya kubagua mtu aliyesoma Zanzibar ni lazima aonekane ni sawa na mtu aliyesoma Urusi au aliyesoma America. Mimi niko kwenye dhana lakini *registration* sina tatizo, aombe *registration* kama anavyoomba aliyesoma Dar es Salaam kwa sababu hata aliyesoma Dar es Salaam hapati *registration automatically* vyeti vyake lazima avipeleke, ajaze fomu kama inavyoelezwa katika sheria hii. Lakini dhana ya huyu aliyesoma Zanzibar kwa sababu tu hii sheria tunayotunga ni ya Bara na yeye lazima aombe, tuna dhana mbili ya Sheria ya Bara na sheria ambayo inatuunganisha wote ambayo ni Sheria ya Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbuke huko nyuma tulikuwa na ugomvi kama je, *State University of Zanzibar* ni sehemu ya Muungano au sio? Naomba Serikali ikumbuke jibu ililotoa hapa ndani, mimi huwa nafuatilia vitu vyangu kwa mtiririko, tutaweza kuja kuingia kwenye mgongano tusipoangalia kwa umakini. Haturuhusiwi kutunga sheria ambayo itakuwa inakwenda kinyume na Katiba. Kama Serikali itasisitiza mimi sitasisitiza kubishia lakini napenda tu Serikali iangalie dhana hiyo.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ulivyoshauri, tukiondoa hili neno *foreigner* sioni kama tunabagua mtu yeyote hapa. Kwa sababu hili linazungumzia juu ya *registration,* mtu kuwa na *qualification* za kuwa *registered* kwenye daftari hili la Ma-*Radiologist* wa Tanzania *Mainland*. Sasa sioni kama tunambagua mtu yeyote kutoka Zanzibar kwenye hii Ibara ya 19. Kwa sababu hili suala ni la Bara, *registration* ni ya wataalam wa watu wa Bara. Tukitoa *any foreigner* sioni kama tunabagua mtu yeyote hapa.

**MWENYEKITI**: Waheshimiwa Wabunge, ukiangalia zile *side notes*, hapa inaitwa *registration of foreigner*. Sasa hapa huyu Mtanzania ameingiaje hapa? Waheshimiwa mnaruhusiwa ku-*discuss* sio kupiga makofi. (*Makofi*)

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nielezee juu ya yale aliyozungumza Mheshimiwa Slaa. Napenda kusisitiza kwamba hapa tunachozungumzia ni juu ya *registration* ya hawa wataalam kwenye daftari *Mainland Tanzania* na qualification ndiyo zimetajwa pale kwamba mtu ambaye anafaa kuwa *registered* kama *Radiologist* na watalaam waliotajwa pale lazima akidhi mahitaji ya hii Ibara ya 19.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nia hapa si kubagua mtu yeyote ambaye ame-*qualify* kule Zanzibar nia ni kwamba lazima akidhi yale mahitaji ya kuandikishwa kwenye daftari la hawa wanataaluma wa *Medical Radiologist and Imaging Professional*. Kwa hiyo, sisi bado tunafikiria kwamba Ibara ya 19 iachwe kama ilivyo. Kama kuna hoja nyingine itakayotolewa, tutaifanyia kazi na tutaliangalia jinsi inavyokuwa na tutajadiliana na wenzetu wa Zanzibar ili kuona kitu gani cha kufanya kwenye kuleta *amendment* kwenye Ibara hii ya 19.

**MWENYEKITI:** *Just assuming* uondoe "*and Tanzania citizen*" itakuwa na ubaya gani? Ondoa "*and Tanzania citizen"* halafu iwe "*a foreigner who qualified outside Mainland Tanzania shall upon payment of prescribed fees"* itaharibu nini, ama itaongeza nini tukiacha? (*Makofi*)

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda hilo ni la kisera labda Mheshimiwa Waziri anaweza kulizungumzia.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti kwanza nikiri kwamba hizi *marginal notes,* nilikuwa natizama kwenye *schedule of amendment* haipo. Lakini tunalozungumzia hapa ni kwamba mtu yeyote anayetaka *registration* ambaye amesoma nje ya *Mainland Tanzania* anahitajika kufanya hiki na hiki. Ndiyo maana pale awali ilikuwa ni *registration of foreigners* lakini wakati tunazungumza na Kamati ikaonekana si *foreigners* tu bali ni mtu yeyote hata Mtanzania ambaye amesoma nje ya mipaka yetu naye lazima tuhakiki vyeti na anapotaka kuwa-*registered* anatakiwa afuate hayo mambo yaliyoorodheshwa hapo. Sasa nadhani sijui kama huu ni wakati ambao tunaruhusiwa kubadilisha hivi vitu.

**MWENYEKITI:** Ndiyo Unaruhusiwa.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Lakini ikisomeka kwamba "any" sijui Kiingereza itakuaje lakini mtu yeyote *who qualified outside Mainland Tanzania shall upon payment of prescribed fees* blaa blaa blaaa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dr. Slaa wewe unaionaje tukisema hivyo. Tuseme "*any person who qualified outside Mainland Tanzania and so on,* itakuwaje?

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani wewe ndiye uliyeipata dhana yangu sielewi kwanini Mwanasheria Mkuu wa Serikali hakutaka kuelewa. Kilichotupotosha hapa ni neno "*registration of foreigner"* kwenye *marginal note*. Dhana iliyojengwa hapa ni kwamba na *Tanzania citizen* aliyepo nje ya *Mainland* kwa maana hiyo aliyeko Zanzibar ni *foreigner*. Sasa ukisharuhusu hiyo umejenga dhana mbaya sana katika nchi ambayo kila siku tunasema sisi ni nchi moja. Sasa kwa maana hiyo basi tukishakubaliana kama unavyopendekeza "*a foreigner who qualified outside Mainland Tanzania"* sina tatizo.

**MWENYEKITI:** Sio *foreigner* tu tunasema "*any person who qualified outside Mainland Tanzania shall…"*.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Nakubaliana, sawa.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, tunaondoa na hizi *foot notes, marginal notes* zinafutwa tunabakia na "*any person who qualified outside Mainland Tanzania…"*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 20
Ibara ya 21

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 22
Ibara ya 23
Ibara ya 24
Ibara ya 25
Ibara ya 26
Ibara ya 27
Ibara ya 28
Ibara ya 29
Ibara ya 30
Ibara ya 31
Ibara ya 32

Ibara ya 33
Ibara ya 34
Ibara ya 35

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 36

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 37
Ibara ya 38
Ibara ya 39
Ibara ya 40
Ibara ya 41
Ibara ya 42

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 43

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 44
Ibara ya 45
Ibara ya 46
Ibara ya 47

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 48

*((Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 49

*((Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Jedwali la Muswada.

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabaliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Wataalam wa Mionzi wa Mwaka 2007**
***(The Medical Radiology and Imaging Professionals Bill, 2007*)**

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imepitia Muswada wa Sheria uitwao *The Medical Radiology and Imaging Professionals Bill, 2007* pamoja na mabadiliko yake Ibara hadi Ibara na kuukubali. Hivyo basi, naomba basi kutoa hoja kwamba Muswada wa *The Medical Radiology and Imaging Professionals Bill, 2007* sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**NAIBU SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge, nina tangazo kutoka kwa Mheshimiwa Hassan Khatib, Katibu Msaidizi wa *Part Caucus* CCM, anaomba kuwaarifu Waheshimiwa Wabunge wa CCM baada ya Kikao wafike ghorofa ya kwanza chumba namba 106 ili wakapate maelezo ya Mkutano Mkuu wa CCM Taifa. Taarifa nyingine, napenda kutoa taarifa kwa wageni wetu, hatupokei matangazo kutoka kwa mtu yeyote katika nchi hii na kutangaza humu ndani. Kama una tangazo lako kuna vyombo vinavyohusika. Kwa mfano sasa hivi kuna taarab sijui itafanyika wapi lakini mtu tu huko amesema umtangazie, haiwezekani wala Redio Uhuru haiwezekani. Tumieni Mawaziri walioko hapa, ama Kamati zilizopo hapa, ama watu wenye nyadhifa waliomo humu ndani, ama Ofisi ya Bunge, mkipeleka kule tutajua ni nani aliyeleta tangazo hilo. Sasa

mtu yeyote atakayeleta tangazo lake tunamtangazia itakuwa Kiti kimeyumba kidogo. Kwa hiyo, naomba tangazo rasmi liende kwa wanaohusika. *(Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, naahirisha kikao mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 07.00 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Wataalam wa Maabara za Afya wa Mwaka 2007
### *(The Health Laboratory Practitioners Bill, 2007)*

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba muswada wa sheria uitwao, *The Health Laboratory Practitioners Act* kama ulivyopangwa kwenye shughuli za leo pamoja marekebisho yake yaliyoambatanishwa, sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, miongoni mwa majukumu katika kutekeleza Sera ya Afya ni kutambua mapema magonjwa na kuyatibu pamoja na kuwaelimisha wananchi jinsi ya kuzuia, kugundua na kutoa tiba sahihi kwa magonjwa. Katika kufanikisha huduma za uchunguzi wa magonjwa, wanahitajika watumishi wa taaluma na ujuzi katika fani mbalimbali za afya wakiwemo wataalamu wa maabara za afya. Pamoja na hayo, kuna haja ya kuwepo mfumo bora wa utoaji wa huduma hizo na sheria zenye kusimamia na kudhibiti mfumo mzima wa utoaji wa huduma za Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika juhudi za kuboresha utoaji wa huduma za afya, kumekuwa na mabadiliko mengi hivi karibuni katika maeneo mengi ya sekta ya afya ikiwemo huduma za maabara. Sheria iliyopo hivi sasa inayosimamia huduma za maabara ni ile ya Usajili wa Mafundisanifu Maabara za Afya (*The Health Laboratory Technologists (Registration) Act No. 11, 2007*).

Sheria hii imeonekana ina upungufu mkubwa na upungufu huo hauendani na mabadiliko katika mfumo wa utoaji wa huduma za afya nchini *(Health Sector Reform).* Upungufu huo umebainishwa kama ifuatavyo:-

(i)Sheria haitaji wahusika wa Sheria *(Application)* ambao ni muhimu sana kutajwa katika sehemu hii ya mwanzo wa sheria.

(ii)Katika sehemu ya pili inayohusu uundwaji wa Baraza, sheria haikuweka bayana majukumu na mamlaka ya Baraza.

(iii)Usajili wa vyuo vya kufundishia wataalamu wa Maabara za Afya haukutajwa.

(iv)Hakuna Sekretarieti ya watendaji wa Baraza.

(v)Sheria haina maelekezo ya haki na wajibu wa Fundisanifu, Maabara za Afya.

(vi) Kanuni za utendaji kazi wa Mafundisanifu Maabara, hazikuonyeshwa katika sheria hii.

(vii)Sheria haikuorodhesha kanuni na maadili ya utendaji kazi *(Professional Code of Conduct and Ethics)* ambazo ni muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhumuni ya sheria hii inayopendekezwa, ni kuweka utaratibu wa kisheria wa kusimamia Mafundisanifu Maabara hapa nchini, kuweka vipengele ambavyo vitasaidia katika kusimamia na kutekeleza utoaji wa huduma bora kwa wananchi. Sheria mpya ikipitishwa, itafuta sheria ya sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hatua za mwanzo za kuandaa mapendekezo ya muswada, Wizara iliwasiliana na wadau mbalimbali kupata maoni yao ili yaweze kuzingatiwa katika sheria mpya, pamoja na yale yaliyopendekezwa na wajumbe walioshiriki katika ngazi mbalimbali za kujadili mapendekezo haya muhimu. Napenda kutambua maoni ya Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Huduma za Jamii ambao walitoa maoni mengi na mazuri ambayo yamezingatiwa katika utayarishaji wa Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, matarajio na matokeo ya kutungwa sheria hii mpya ni kama ifuatavyo:-

(i)Kuboresha utoaji wa huduma za afya kwa jumla kwa kuzingatia mabadiliko yanayoendelea katika mfumo wa utoaji wa huduma za afya.

(ii)Kuhakikisha kuwa vyuo vinavyotoa taaluma za wataalamu wa maabara ni vile tu vinavyotambuliwa na Baraza la Wataalamu wa Maabara za Afya *(Health Laboratory Practitioners' Council).*

(iii) Kuimarisha utekelezaji wa sheria yenyewe n.k.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wadau na wajumbe wote waliochangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na umuhimu wa mambo yaliyozingatiwa katika Muswada, Muswada huu umegawanyika katika sehemu kuu nane. Sehemu ya Kwanza inapendekeza masharti ya awali kama: jina la sheria, tafsiri ya misamiati mbalimbali na tarehe ya kuanza kutumika Sheria. Sehemu ya Pili inapendekeza uanzishwaji wa Baraza la Wataalamu wa Maabara za Afya, majukumu na madaraka ya Baraza hilo, uteuzi wa Msajili na Naibu Msajili wa Baraza na Majukumu yao. Aidha, sehemu hii inatoa uteuzi na majukumu ya wasimamizi.

Sehemu ya Tatu inapendekeza utaratibu na vigezo vinavyohitajika kwa ajili ya usajili wa wataalamu wa maabara ya afya, madurufu ya ada zinazolipwa na wataalamu hao, taratibu za kumfuta mtaalamu wa maabara za afya kwenye kitabu na orodha ya watu waliopatiwa leseni. Sehemu ya Nne ya Muswada inahusu wajibu wa wataalamu wa maabara za afya na watu waliopatiwa leseni. Sehemu ya Tano inahusu masuala ya uchunguzi wa awali (tafiti) dhidi ya mtu yeyote atakayekataa kufika mbele ya Baraza, haki ya kukata rufaa.

Sehemu ya Sita inahusu masuala ya fedha. Sehemu hii inapendekeza vyanzo vya fedha na mwaka wa fedha wa Baraza, maslahi, makadirio, ukaguzi wa mahesabu na uwasilishwaji wa taarifa za hesabu Bungeni. Sehemu ya Saba ya Muswada inaainisha makosa na adhabu mbalimbali zinazoweza kutolewa dhidi ya mtu atakayekiuka sheria inayopendekezwa. Sehemu ya Nane na ya mwisho, inahusu masharti ya jumla kama vile mamlaka aliyopatiwa Waziri kutengeneza kanuni mbalimbali, kufanya marekebisho na mabadiliko katika Jedwali na inapendekeza pia kufuta Sheria ya Usajili wa Mafundisanifu wa Maabara, 1997.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuhitimisha, baada ya kutoa maelezo hayo, naomba kuchukua fursa hii tena kuishukuru Kamati ya Huduma za Jamii kwa kupitia muswada huu chini ya Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti kwa michango yao waliyoitoa wakati wa kujadili muswada huu.

Mwisho, namalizia kwa kuwaomba Waheshimiwa Wabunge waweze kujadili mapendekezo yaliyomo katika muswada huu pamoja na marekebisho yaliyopendekezwa na Kamati ya Huduma za Jamii na hatimaye kuupitisha na kuwa Sheria ya Kusimamia Wataalamu wa Maabara za Afya, *(The Health Laboratory Practitioners Act, 2007).*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA (K.N.Y. MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii alikwishatoa rambirambi kwa niaba ya Kamati ya Huduma za Jamii, nachukua nafasi hii kwa niaba ya wananchi wangu, wapiga kura wa Jimbo la Rufiji, kutoa rambi rambi za dhati kwa familia na wananchi wote wa Mkoa wa Kilimanjaro kwa kifo cha Mheshimiwa Salome Joseph Mbatia aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalumu na Naibu Waziri wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi.

Vile vile natoa pole kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliopatwa na ajali mbaya za magari akiwemo Mheshimiwa Mudhihir Mohamed Mudhihir, Mbunge wa Jimbo la Mchinga na Mheshimiwa Prof. Juma Athuman Kapuya, Mbunge wa Jimbo la Urambo

Magharibi na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. *Inshallah*, Mwenyezi Mungu atawaponyesha haraka ili tuweze kuwa nao katika Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii, naomba kutoa maoni ya Kamati ya Huduma za Jamii kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 70(2), Toleo la Mwaka 2004 iliyotupa sisi uwezo wa kuufikiria Muswada huu wa Sheria ya Wataalamu wa Maabara za Afya wa mwaka 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilikutana na ilipata maelezo ya kina kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii akisaidiwa na Naibu wake na ilipata muda wa kutosha kujadili na kuhoji vifungu na vipengele vya Muswada huu. Kamati ilipata maelezo sahihi kabisa kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii na Naibu wake na pia kutoka kwa Wataalamu. Kamati iliweza kupitia vifungu vyote kwa makini na kuuelewa Muswada mzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaunga mkono hatua ya Serikali ya kuuleta Muswada huu ikiwa ni hatua madhubuti ya kutekeleza kwa vitendo maelezo ya Sera ya Afya ya 2007 ambayo pamoja na masuala mengine, inasisitiza umuhimu wa kutambua magonjwa mapema, kuyatibu na kuwaelimisha wananchi jinsi ya kujikinga. Katika kufanikisha utekelezaji wa Sera ya Afya, huduma za uchunguzi wa magonjwa, kunahitajika wataalamu wenye ujuzi mbalimbali wakiwemo wataalamu wa maabara. Aidha, kutokana na mabadiliko mengi ya kiuchumi na kisiasa, Serikali iliwahi kuleta katika Bunge hili Muswada wa Sheria ya Usajili wa Mafundisanifu wa Maabara *(The Health Laboratory Technologists (Registration) Act, 1997),* sheria ambayo kwa wakati huu inaonekana kuwa na upungufu mkubwa na hivyo kutokidhi mahitaji na matakwa ya sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilizingatia upungufu uliobainishwa katika kutekeleza sheria hiyo ambayo ni pamoja na kutobainisha wazi walengwa na wahusika, vilevile kushindwa kuainisha vigezo vya kuanzishwa kwa vyuo vya taaluma za maabara za afya. Hali kadhalika kutokuwepo kwa Sekretarieti ya Baraza katika kurahisisha utendaji wa *Council* hiyo, kutokuwepo kamati za kusaidia utendaji na kutotajwa kwa wataalamu wa sayansi ya fani ya maabara.

Vilevile Kamati inaona kuwa Muswada wa sheria hii umeletwa kwa kuzingatia Kanuni ya 149(2) ya Utumishi wa Umma na Sheria ya Serikali ya Mitaa ya 1982, kifungu cha 174(2), zilizoelekeza kuwa Mabaraza ya Usajili wa wataalamu na Sera ya Afya imeelekeza kuwepo na Mabaraza ya Usajili wa wataalamu na sera ya afya ambapo kulikuwa na sera ya afya mwaka 1990 iliyorejeshwa mwaka 2007. Pia kwa kuzingatia umuhimu wa kila sekta kusimamia taaluma za wataalamu walio katika Serikali. Hivyo, kutokana na changamoto hizo zikichangiwa na maendeleo ya mabadiliko katika nyanja za taaluma, sayansi na teknolojia katika Ulimwengu wa Utandawazi, Kamati inakubaliana na Serikali kuwa kuna umuhimu wa kuwa na sheria ya kusimamia ubora, maadili, taaluma na kuwadhibiti wataalamu wa maabara ya afya hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati hii pia inakubaliana na Serikali kuwa sheria hii ni muhimu na italeta mafanikio yafuatayo:-

(i) Kuboresha utoaji wa huduma za afya kwa ujumla kwa kuzingatia mabadiliko yanayoendelea katika mfumo mzima wa huduma za afya.

(ii)Kuhakikisha kuwa vyuo vinavyotambuliwa na Baraza *(The Health Laboratory Practitioners Council)* ndivyo vinavyohusika kutoa taaluma ya wataalamu wa maabara.

(iii)Kuimarisha utekelezaji wa sheria yenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kufikiria Muswada huu, Kamati ilipitia sehemu zote 8 na vipengele vyake vyote na kisha ikatoa maoni kama ifuatavyo:-

(i)Kamati imeona kuwa Muswada wa Sheria unatambua kuwepo kwa madaraja mbali mbali ya wataalamu wa maabara za afya yanayotokana na viwango vya elimu yao ambayo yanalenga kuwatambua, kuwasajili wataalamu wa maabara za afya katika madaraja yanayozingatia taaluma walizonazo.

(ii)Baraza litahusika kusimamia maadili ya utendaji kazi ikiwa ni pamoja na kutoa adhabu kali za aina mbalimbali pale inapotakiwa.

(iii) Kamati inashauri kuwa Baraza liwe na mazingira yatakayowawezesha wataalamu wa ngazi za chini kujiendeleza kitaaluma na kufikia ngazi za juu ikiwa ni pamoja na kuwepo mipango ya mafunzo kazini inayotambuliwa na Baraza.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni ya jumla:-

(i)Kamati inashauri kuwa Serikali ifanye juhudi za makusudi kuimarisha na kuongeza idadi ya wanataaluma wa maabara za afya ambao kwa sasa ni wachache sana. Inasemekana kuwa wataalamu wa maabara za afya waliopo sasa hivi ni aslimia 32 tu ya mahitaji ya ikama katika hospitali mbalimbali za Serikali.

(ii)Wataalamu wa maabara za afya waimarishwe katika kuzingatia maadili yao ya kazi kutokana na wao kuhusika katika kuchunguza maradhi mbalimbali ya wagonjwa. Hapa maana yake ni *confidentiality* au nasema kama mchunguzi kaona ugonjwa, basi anatakiwa amwambie yule mgonjwa tu, asimwambie mtu mwingine yeyote, hata ikibidi mume, anaumwa, basi mkewe akija asipewe habari za mumewe na mke akiumwa, mumewe akija, asipewe habari za mkewe, huyu mume hana haki hiyo. Lazima yule aliyepimwa ndiye apewe majibu ya matokeo ya vipimo. Hii ndiyo maana ya *confidentiality of medical information.* Hiyo itabidi ifanyiwe mkazo katika dunia yetu ya sasa.

(iii)Kamati inaishauri Serikali kuimarisha na kuboresha vitendea kazi vya maabara za afya katika hospitali zake ambako ni kimbilio la wananchi wengi ikiwa ni pamoja na kupata vifaa vya teknolojia ya kisasa vinavyoweza kurahisisha uchunguzi wa magonjwa mbali mbali kwa usahihi zaidi na kwa muda mfupi zaidi.

(iv.)Kamati inasisitiza kuwa ni lazima wagonjwa wapimwe kabla ya kupewa matibabu ili kuepeuka matatizo, mathalan, kuepuka matumizi ya dawa yasiyo sahihi. Pili, mgonjwa anaweza akapewa dawa akatumia kwa muda mrefu bila kupona kwa sababu hatukupata *diagnosis*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua fursa hii kuwapongeza Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, Mheshimiwa Prof. David Mwakyusa na Naibu wake, Mheshimiwa Aisha O. Kigoda na wataalamu wa Serikali kwa ushirikiano na ufafanuzi waliotoa wakati Kamati ilipokuwa ikiujadili Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii, nawapongeza wajumbe wote wa Kamati hii kwa mawazo na maelekezo mazuri waliyompa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii. Napenda pia kuchukua fursa hii kuwashukuru kwa dhati kwa kushiriki kikamilifu wakati wa majadiliano ya Kamati hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kamati ya Huduma za Jamii, naomba kuunga mkono hoja na vile vile naomba kuwasilisha. Asante sana. *(Makofi)*

**MHE. NURU A. BAFADHILI (K.N.Y MSEMAJI WA UPINZANI - WIZARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, napenda kutoa maoni yetu, kuhusu muswada wa Sheria ya Uanzishaji wa Baraza la Wataalamu wa Maabara za Afya wa Mwaka 2007 *(The Health Laboratory Practitioners Bill, 2007),* kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 43(5) (b) (c), Toleo la 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba na mimi niungane na Waheshimiwa Wabunge kutoa pole kwa familia, Mheshimiwa Rais, ndugu na marafiki kwa msiba mkubwa uliotupata wa kuondokewa na mpendwa wetu, hayati Salome Joseph Mbatia, aliyetutoka hivi karibuni katika ajali ya gari. Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. *Amin!*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha napenda kutumia nafasi hii kutoa pole za dhati kwa Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed, Kiongozi wa Upinzani ambaye alifiwa na mama yake hivi karibuni wakati yeye akiwa India kwa matibabu. Kwa vile leo ndio siku anayofanyiwa upasuaji katika Hospitali ya Apolo, India, tunamwombea Mwenyezi Mungu aweze kumpa nguvu kushindana na maumivu, amjalie afya njema ili arudi mapema kuwahudumia Watanzania kama alivyokuwa anafanya siku zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli kuwa sekta ya afya hapa nchini imepitia mabadiliko mengi sana na ambayo yanazidi kutokea siku hadi siku. Hata hivyo, licha ya maboresho hayo sekta ya maabara bado inasuasua sana katika mwenendo wa mabadiliko hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kusuasua huko kwa sekta ya maabara kunasababishwa na mambo mengi zaidi ya yale majukumu ya kiusimamizi *(management)*. Tumeshuhudia mara nyingi hospitali kubwa ya Rufaa kama Muhimbili ikikosa huduma za uhakika za

maabara na kuwalazimu wagonjwa kwenda katika hospitali ya binafsi ya Tumaini, Aga Khan au nyingine binafsi kupata vipimo vinavyotakiwa. Hii ni katika ngazi ya juu ya Taifa, sasa jambo la kujiuliza: je, katika ngazi za Wilaya, Kata na Vijiji hali ya huduma za maabara iko vipi?

Taarifa tuliyo nayo ni kuwa ni zahanati chache sana zina vipimo muhimu kama vya malaria. Hii ni hali ya hatari sana kwa maisha ya wananchi wetu. Zahanati, na vituo vya afya vinaweza kuwepo kwenye eneo lakini kama havina vipimo husika na vya uhakika, ni vigumu sana kwa tabibu kutoa matibabu sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kweli kabisa wakati mwingine tunatoa shutuma nyingi kwa madaktari na wauguzi kwa kuwapa wagonjwa dawa ambazo haziendani na ugonjwa wa mtu. Mtu wa kwanza anayemwezesha daktari kufanya kazi yake kwa ufanisi ni mtu wa maabara, pindi anapotoa matokeo ambayo si sahihi kulingana na ugonjwa wa mtu, maana yake ni kuwa Daktari itamlazimu kutoa dawa ambazo hazitakuwa sahihi kwa matatizo ya mgonjwa. Imetulazimu kulisema hili kutokana na malalamiko kuwa wako wananchi wamepata vilema vya kudumu na wengi wamepoteza maisha yao kutokana na watendaji wa maabara kutoa majibu tofauti na kupelekea madaktari kutoa dawa ambazo haziendani kabisa na ugonjwa wenyewe.

Ni jana tu, tumeshuhudia katika luninga katika hospitali ya Mwananyamala watu wamedhurika kwa kupewa madawa ambayo yamewasababishia madhara ya ngozi. Huu ni uzembe wa aina yake. Lakini pia inawezekana ni kutokana na uhafifu au kutokuwepo kwa vifaa maalumu vyenye kutoa majibu ya uhakika kwa vipimo vinavyochukuliwa. Vyovyote vile hali hii si ya kutazamwa tu, kwa vile inahusu uhai wa binadamu. Ni lazima hatua za haraka zichukuliwe kurekebisha dosari kama hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuweka Baraza la Kudhibiti utendaji kazi katika fani hii bila ya kuwepo na maabara zenyewe ni kama mchezo wa kuigiza. Wataalamu watafanyia wapi kazi zao? Hali hii ya kutokuwa na vifaa na nyenzo za kufanyia kazi ndiyo kwa kiwango kikubwa, inayosababisha wataalamu wetu kukata tamaa, kuondoka nchini na kwenda kufanya kazi nje ya nchi kama vile Botswana, Swaziland, Lesotho, Namibia na kadhalika, ambapo mazingira ya kazi yanatambua na kuthamini utaalamu wao kwa Serikali kuwapatia vifaa na nyenzo za kazi. Hata sisi tukiweka vipaumbele vyetu vizuri hili nalo linawezekana.

Kambi ya Upinzani haina tatizo na muswada huu. Lakini inadhani vyema kwanza Serikali ikatengeneza mazingira mazuri ya kiutendaji kwa wanataaluma hao kwa kuimarisha maabara kivifaa na nyenzo husika *(consumables)* jambo ambalo litaimarisha huduma na kujenga morali ya watumishi.

Sheria peke yake haiwezi kufanya kazi iwapo mazingira mazima ya kazi hayajawezeshwa na kuboreshwa. Kambi ya Upinzani inaamini kuwa kuimarisha huduma za maabara ni hatua nzuri na muhimu katika kuimarisha huduma za utabibu katika ngazi

zote, kuanzia Taifa, Mkoa, Wilaya hadi ngazi ya zahanati, kila ngazi kwa uzito na utaalamu unaohitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuimarishwa kwa huduma za maabara katika ngazi za chini, kutapunguza msongamano wa wagonjwa kuja katika hospitali za mikoa na taifa kwa ajili ya kufuata vipimo. Vituo vyetu vya afya vya Serikali navyo vitapata tena heshima iliyopotea kwa kulinganisha na zahanati za watu binafsi ambazo mara nyingi ndizo zinazokuwa na vifaa na nyenzo hizo za maabara. Wananchi nao watajenga tena imani na taasisi zao, kwani hizo zinaendeshwa kwa kodi na jasho lao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani kwa ujumla inaitaka Serikali kupitia kwa Mheshimiwa Waziri kutoa tamko kuwahakikishia Watanzania kuhusu mkakati wa makusudi wa kuimarisha utendaji kwa sekta ya maabara hasa katika hospitali na zahanati za Serikali katika ngazi zote, na ni lini mpango huo utaanza kutekelezwa rasmi na utakamiliki lini? Sanjari na hilo itakuwa bora Mheshimiwa Waziri akilieleza Bunge hili kuwa ni kiasi gani na kwa namna gani hasa Serikali inakusudia kuwekeza kwenye utafiti na uchunguzi katika maabara?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya vyama vya Ushindani inaamini kuwa hii ndio njia pekee ya kutengeneza Tanzania salama na imara. *MEWATA* wameonyesha njia. Iwapo kundi dogo la madaktari wameweza kuleta tofauti katika jamii, Serikali inayotumia kodi ya wananchi wote imeshindwa nini? Tunapenda kuwapongeza sana madaktari wanawake kwa kazi nzuri wanayofanya hasa katika masuala ya saratani ya matiti. Tunawaomba moyo huu udumishwe na tunawashukuru na kuwapongeza wananchi wote waliowaunga mkono katika harakati zao za kuokoa maisha ya mama Mtanzania. Ni vema basi Serikali nayo ikaunga mkono jitihada zao hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bafadhili, asante kwa kuwasilisha vizuri maelezo yako. Waheshimiwa Wabunge, naona Muswada wa asubuhi na huu, unafanana kidogo. Kuna mchangiaji mmoja tu, Mheshimiwa Lubeleje.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia Muswada huu muhimu. Kwanza kabisa, nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kuleta Muswada huu.

Kwa kuwa nilishatoa salamu za rambi rambi wakati nawasilisha Maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, sitarudia tena, niendelee moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema naunga mkono hoja hii kwa sababu maabara ni eneo nyeti sana katika kuboresha huduma za afya, hospitali za wilaya, mikoa, zahanati na vituo vya afya. Kama walivyosema Waheshimiwa wabunge wenzangu,

nasema miswada hii kwa kweli inafanana. Huu uliopita sasa hivi na huu tunaoujadili inafanana, kwa hiyo, matatizo mengi yanafanana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tiba sahihi ni pamoja na kupata majibu au matokeo ya uchunguzi katika maabara. Tuna matatizo makubwa ya vifaa hasa katika zahanati, vituo vya afya ambako wananchi wengi wapo na kuna wagonjwa wengi. Huwezi kumtibu mgonjwa kwa kumwangalia tu kwamba huyu mtu ana homa ukasema ana malaria kwa sababu homa ni dalili ya ugonjwa siyo kwamba lazima awe na malaria.

Ni lazima achunguzwe kwenye maabara kuona kama ana malaria au kama ana *typhoid* au magonjwa mengine. Kwa hiyo, nashauri kwamba ni vizuri kuwe na maabara katika zahanati, vituo vya afya ili wagonjwa wasitibiwe bila kuchunguzwa matatizo yanayowakabili.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika hospitali zetu za Wilaya, mikoa, tuwe na vifaa vya kisasa ambavyo vitawafanya wagonjwa wanapokwenda kuchunguzwa afya zao wasichukue muda mrefu kungoja majibu. Kwa mfano, mgonjwa anapimwa damu anaweza kukaa saa mbili au tatu kusubiri majibu. Tuwe na vifaa vya kisasa ambavyo majibu yatatoka haraka, iwe ni dakika tano ama kumi na tano mtu anapata majibu kwa sababu ukiwa na vifaa bora ama vya kisasa itasaidia vilevile kuboresha huduma za maabara katika vituo na hospitali zetu za Wilaya.

Wataalamu ni wachache. Kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge wenzangu asilimia 32 tu, lakini kuna upungufu wa wataalamu wa maabara kama asilimia zaidi ya 60. Wataalamu hawa ni muhimu sana, huwezi kuboresha sekta ya afya bila ya kuwa na wataalamu wa maabara na ni eneo nyeti sana. Nashauri tuongeze Vyuo kwa ajili ya kusomesha wataalamu wa maabara ambao watapelekwa mpaka huko vijijini.

Mhehimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kipengele hiki katika kuunda hili Baraza. Kuna Kamati itakayoundwa kwa ajili ya kuangalia maadili, *code of ethics* na *code of conduct.* Kila kazi ina maadili yake, kuna *medical ethics* lazima wasitoe siri za wagonjwa na hii ni miiko ya utaalamu wa afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema mwanzo miswada hii kwa kweli inafanana, uchache wa wataalamu, upungufu wa vifaa vinafanana, kwa hiyo, naunga mkono hoja hii na namtakia kila la heri muswada upitishwe ili uweze kufanya kazi. Ahsante sana!

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, sasa nitamwita Mheshiwa John Cheyo.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika. Nimesimama na mimi kuweza kuchangia muswada huu, lakini kabla sijafanya hivyo kwa niaba ya *UDP* kama Mwenyekiti nataka kutumia nafasi hii kumpa pole Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi, kwa kifo cha kada ambaye tumemzika juzi, Mheshimiwa Salome Mbatia. Mimi nilikuwepo, najua umeondokewa na kada ambaye alikuwa anategemewa sana labda kuchaguliwa katika mkutano huu mkubwa wa Chama Cha Mapinduzi. Kwa

hiyo, ni haki tuwape wana-CCM wote pole kwa kuondokewa na kada ambaye alikuwa na nguvu sana katika CCM.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, napenda kutumia nafasi hii kuwatakia kila la heri wana-CCM ambao wanagombea nafasi mbalimbali. Mungu awashushie neema na baraka na wagawiwe wote wanaostahili. Na jambo hili nataka kusisitiza, kusema kweli pamoja na kwamba si tu niko katika Kambi ya Upinzani lakini tunaomba wana-CCM mjihadhari kwamba dumuzi la rushwa likiwamaliza ninyi sisi ndiyo litatumaliza kabisa. Nakuombea kura na wewe Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo unipe nafasi. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba sasa nijikite kwenye muswada na jambo la kwanza ambalo nataka kusisitiza zaidi kwa Waziri wa Afya. Ni kwamba kweli hii kada ya *technicians* au wataalamu wa maabara ni kada ya maana sana katika taaluma ya afya. Sisi ambao tunatembea vijijini kusema kweli tunapona tu kwa sababu Mwenyezi Mungu anatupenda lakini utaalamu kwenye *dispensary* zaidi wa maabara umepotea kabisa. Kwa hiyo, nilikuwa natumia nafasi hii kusisitiza katika bajeti yenu, hebu rudini nyuma sasa mwongeze umaana kwanza wa kada hii na wa *dispensary*. Watu wetu wengi sasa wanakwenda kwenye dawa mbalimbali za kienyeji na wengine wanatibiwa ovyo ovyo tu bila kupima.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii itatufanya tumalize watu na wengi wanakufa kwa sababu vipimo havijawa sawasawa. Kwa hiyo, naona ni muhimu kabisa kama huu muswada utaweza kutusaidia kufika mahali ambako kwanza ile fani yenyewe inatambuliwa kimakusudi kabisa kwa njia zote, sio tu kwa kuwekewa *code of conduct* ambayo ni ya maana lakini pia kwa kuwekewa maslahi ambayo kweli wajione bila daktari ni sawasawa na mkulima anayekwenda kulima bila jembe, tukifikia hatua hiyo itatusaidia sana katika hospitali.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengi wetu tumekwishaingia katika hospitali na wengi wetu tumeshauguliwa na si lazima kila mmoja hapa ataje magonjwa au ataje ndugu zake, lakini si ajabu mtu kutumia siku mbili au tatu daktari hajajua kitu kinachomsumbua mgonjwa. Hii ni kwa sababu ya ukosefu wa maabara. Kwa hiyo, hiyo *council* ambayo itatengenezwa hapa, katika kazi zake nimeona katika Ibara ya 6 ni kutengeneza *ethics* na pia kuweza kumshauri Waziri. Basi ifanye hiyo kazi imshauri Waziri vizuri kabisa kwamba wale watu ambao wako katika kada hii wawekewe maadili ambayo yatatusaidia kuweza kupata majibu halisi, vifaa viwepo lakini pia wawekewe adhabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuja kugundua kwamba tunazungumzia tu juu ya mtu ambaye ni *kihiyo* lakini anajiwekea vyeti. Kwa hiyo, anaweza akapata adhabu ya kifungo na mambo kama hayo, lakini vipi yule ambaye hafanyi kazi yake vizuri? Wewe unakwenda kucheki malaria, anakuambia una ugonjwa wa *typhoid* na kumbe huna *typhoid*! Unakwenda kuwekewa *metakelfin*. Mimi nimekwishaona ndugu yangu mmoja ame-*paralyze* kwa sababu ya kupata *overdose* ya *metakelfin* na yeye kumbe alikuwa haumwi ule ugonjwa. Hii inaonesha jinsi gani hawa watu ni wa maana, sasa mtu anapofanya vitu kama hivyo *sanction* zake ni nini, kufukuzwa kazi tu!

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tumeweza kutambua kwamba *ukihiyo* unaweza kwenda jela kama unaandika ripoti za uwongo kwa nini usiende jela? Kwa hiyo, mimi naona itambuliwe kimaslahi, kama ni pesa wapewe pesa za kutosha ili wafanye kazi zao vizuri. Lakini pia wajue wana wajibu, iwe kwamba kama wasipofanya kazi zao vizuri sio tu watafukuzwa kazi lakini pia wanaweza hata kufungwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nataka kusisitiza jambo jingine. Sehemu hii ya utaalamu wa afya ndiyo mahali pazuri ambapo watu binafsi wanaweza wakawekeza fedha zao nyingi na ikasaidia. Tunajua *Clinics*, au *diagnostic centres* ambazo ziko *South Africa* na watu wanazikimbilia; tunajua *Harry street in London* ambapo wewe unaweza kwenda pale ukachunguzwa halafu ndiyo ukaenda kwa daktari. Mimi naona pia umefikia wakati sasa Tanzania kujikuta tuna *Harry streets* mbalimbali hata vijijini ambako watu watajua kwamba katika mji fulani au katika barabara fulani, ukiwa unaumwa si lazima uende kwanza kwa daktari lakini kimbilia kwanza vipimo wakucheki ni kitu gani ndipo uende ukamwone daktari

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naona baadhi ya misururu ambayo tunaiweka kule ndani ya hospitali zetu kumwona daktari na vitu kama hivyo, ingeweza kupunguzwa kama tungeweza kuwa na *Harry Streets* au maabara ndogondogo sehemu mabalimbali na kwa miji mikubwa kama Dar es Salaam pawe na D*iagnostic Centres* ambapo watu watakwenda kuchekiwa na *laboratory* zile zinatangazwa kuwa ni nzuri na zitatoa majibu sahihi na kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naangalia huu muswada, kitu ambacho labda Mheshimiwa Waziri ningependa anieleze ni kwamba najua tumejikita zaidi kwa mtu, je, kule tunakokwenda pakiwepo na mtu *as a company* au *as a person* ambaye anataka kuanzisha *practice* ya maabara ataweza kudhibitiwa na Baraza gani? Nafikiri Baraza kama hili lingeweza pia kuwadhibiti watu kama hawa, kwa sababu nafikiria kule tunakokwenda haitawezekana watu wote kuweza kuingia hospitali bila kuweza kwenda mahali ambapo wanaweza kwenda kuangaliwa afya zao. Kwa hiyo, naona hili ni jambo la maana. Nataka kuchukua nafasi hii kusema kwamba kazi itakayofanywa na watu hawa itakuwa nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa ni daktari. Kwa mfano kule Muhimbili daktari kuwa na *practice* zao nina hakika mtu hawezi akafanya kazi saa nane vizuri na kwa *pressure* zilivyo kama Muhimbili halafu akaenda kufanya kazi ya kwake kwenye maabara yake ama kwenye kliniki yake. Naona jambo hili liangaliwe na Wizara, kama tatizo ni pesa au kama kinachowahangaisha madaktari hawa wasipate nafasi ya kuangalia *results* kutoka kwenye maabara hizi wasiweze ku-*concentrate* kwenye *X-Rays* ambazo zinapelekwa kwao; wasiweze kuangalia wagonjwa vizuri, kama tatizo ni pesa sioni ni kwa nini tusitoe pesa za kutosha kwa wataalamu wetu ili wakae kama ni Muhimbili *eight hours of work*, bila ya kuwa na tamaa ya kwenda kwenye kliniki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu wagonjwa na madaktari wengine wanatumia Muhimbili tu kama vile ni *address* wanakutana Muhimbili lakini matibabu hufanyika

kwenye kliniki ya daktari na ukienda kule matibabu ni ghali sana. Mimi naona utaratibu huu kama njia mojawapo ya kudhibiti hali hii. Watu ambao tunawawekea *council* sasa tuone kwamba kazi yao kweli iwasaidie Watanzania, tuliangalie hili pia turudi kwenye *profession* ambapo mtu anafanya *professional work* yake bila ya kuwa na mawazo ya kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuchangia kidogo niliyonayo. Awali ya yote niipongeze Wizara pamoja na Mheshimiwa Waziri kwa kuleta muswada ambao unatukumbusha kuibua baadhi ya mambo ambayo yanajitokeza kwenye jamii yetu na yanahitaji kusaidiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijachangia naomba pia niutakie heri Mkutano Mkuu wa CCM unaokuja, pamoja na kwamba sijaenda kiundani kwenye muswada huu kutokana na hali inayonikabili ya kuuguliwa na mzazi wangu ambaye namshukuru sana Mwenyezi Mungu amemponyesha kwa kiasi lakini nimeona angalau nipitie katika maeneo ambayo yana utata kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maabara nyingi zinazozungumzwa ziko katika vituo maalumu, yaani zahanati zetu, lakini kuna wananchi ambao wanaishi katika maeneo ya mbali sana na wanahitaji kupata huduma kama hizi lakini kwao inakuwa ni vigumu kuzipata kutokana na hali halisi ya kiuchumi. Swali langu au nililokuwa naliona ni kwamba je, mpango wa kuongeza hizi *mobile labs* kama zipo ambazo zinaweza kutumika kwa ajili ya kuwafuata watu kama hawa ukoje? Kwa sababu, kwa mfano, sasa hivi tunazungumzia sana suala la magonjwa kama haya ya Ukimwi, watu wana nia ya kupenda kwenda wakapimwe, wanahitaji watibiwe kwa wakati, lakini unakuta hata kufuata ile dozi yake inakuwa ni vigumu kwa sababu hawezi tu kujimezea dawa bila kuchekiwa. Nashauri kwamba hizo *mobile labs* ziongezeke ili ziweze kuwasaidia wananchi ambao wapo kwenye maeneo ya mbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hawa mabingwa wa maabara kuweza ku-*practice* baada ya shughuli za ajira maalumu, hapo natofautiana kidogo na msemaji aliyepita kwa sababu mimi nimejionea yaliyonikuta safari hii. Ni kwamba kuna wakati hata ukienda kwenye hospitali hizi kubwa ile nafasi ya kuweza kumwona daktari kutokana na mlundikano uliopo inakuwa ni vigumu. Lakini kama kungekuwa na vituo maalumu hata hawa watu wakakopeshwa, wale wanaokuwa wamemaliza saa zao za kazi wakaenda kufanya pale kazi zao kwa sababu mwingine anakuwa ni bingwa kufuatana na *talents* zake ambazo Mwenyezi Mungu amempa. Kwa hiyo, hata ukimzuia useme kwamba wewe ufanye hapo tu mwisho na usiende sehemu nyingine, yawezekana tukawa tunazuia zile *talents* zisiweze kuwasaidia watu wengi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi mtazamo wangu na nikiungana katika yale yaliyozungumzwa na msemaji aliyepita kwamba kuwe angalau na uwezeshaji wa

kujenga vituo kama hivyo. Hata kama ni kwa mikopo, kwa sababu wagonjwa ni wengi, watu wana pesa wanahitaji kutibiwa lakini wakati mwingine mtu anakuta anashindwa kuenda kutibiwa kwa sababu ya wakati au ratiba maalumu zilizowekwa na pengine kushindwa kupata matibabu kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali iangalie kwa kushirikiana na wawezeshaji mbalimbali kuwawezesha watu hawa ambao wana *talents* waweze ku-*practice* hata sehemu za vijijini, wasaidiwe hata kujenga hizo maabara ndogo. Mtu kama amemaliza, ana ujuzi wake, badala ya kusubiri ajira ya Serikali akiwezeshwa pale anaweza hata akawasaidia wale ambao wapo katika maeneo ya mbali au pia kupunguza mlundikano unaoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa siku ya leo niliona niseme hilo tu angalau liweze kuchangia, Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA**: Ahsante, pole sana kwa kuuguza mgonjwa Baba yako na tunamwombea afya njema. Waheshimiwa kama nilivyosema sina wachangiaji wengine kwa hiyo nitamwita mtoa hoja aweze kutoa ufafanuzi au majibu katika maswali mbalimbali yaliyoulizwa.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu wa Spika, naomba nikushukuru kwa mara nyingine tena kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuhitimisha hoja niliyoitoa hivi punde. Naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa waliopata nafasi ya kuchangia, kwa kuzungumza hapa Bungeni na wale walioleta kwa maandishi, naomba niwatambue kama ifuatavyo:-

Waliochangia kwa kuzungumza ni pamoja na Mheshimiwa Prof. Iddris A. Mtullya, Mheshimiwa Nuru A. Bafadhili, aliyezungumza kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mheshimiwa John M. Cheyo, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, aliyechangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya.

Mheshimiwa Naibu wa Spika, naomba nikushukuru tena na nigusie baadhi ya mambo yaliyojitokeza katika michango hii. Natambua kuwa wote wameunga mkono hoja. Nakushukuru pia Mheshimiwa Bafadhili kwa kuunga hoja mkono.

Mheshimiwa Mtullya, aliyezungumza kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Huduma za Jamii, amekubaliana na muswada huu. Kwa ujumla na niseme tu kwamba mambo yote yaliyojitokeza yaliyotoka kwenye Kamati wakati wa mazungumzo, marekebisho yote yamewekwa kwenye muswada huu mpya. Mheshimiwa Mtullya alisisitiza tu mambo kadhaa. Alizungumzia maadili yasimamiwe kikamilifu na hasa akazungumzia habari za usiri. Vilevile alishauri kuwa kuwe na utaratibu wa kuwaendeleza hawa watumishi suala ambalo tunalipokea, lipo na tutalisimamia kwa karibu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika pia alizungumzia idadi ya watumishi kuwa wachache na hili limejitokeza kwa wazungumzaji wengine. Kama nilivyozungumza jana katika muswada unaoshabihiana na hili, na leo asubuhi, ni kwamba ni kweli idadi ya watumishi katika sekta ya afya ni ndogo na tuna mkakati maalumu ambao umeainishwa katika mpango wetu maalumu wa MAMM kuongeza hao watumishi, na umeanza mwaka huu kwa kupanua Vyuo vyetu. Pia alieleza kuhusu vitendea kazi na teknolojia kwamba iongezwe na alimalizia kwa kuzungumza kwamba wagonjwa wapimwe kabla ya kutibiwa. Nadhani yeye akiwa daktari aliyebobea tuseme pale inapowezekana kuna wakati mwingine inabidi umtibu mgonjwa bila kungojea vipimo lakini tutajitahidi kwa kadri tunavyoweza kuwa na vipimo sahihi vya teknolojia ya juu.

Mheshimiwa Nuru Bafadhili, anasema kwamba utendaji mzima katika suala zima ni kusuasua kwa usimamizi kwamba sio mzuri, zahanati hazina vipimo na kwamba hili Baraza tunalounda wakati hakuna vifaa tunaliunda la nini! Kusema hakuna vifaa labda ni kali kidogo, tuseme vifaa havitoshi, vifaa vipo na labda huduma inapokuwa mbovu ni kwa sababu tunakuwa hatuna kitu kama Baraza hili.

Vifaa vinaweza vikawa vipo vichache, lakini kazi lazima iendelee, hivyo vichache tulivyonavyo viweze kutumika kikamilifu. Watu wenye maadili nikubaliane na wewe kwamba labda usimamizi ni mbovu na nia ya kuunda chombo hiki ni kwamba usimamizi uwe madhubuti, kwa hiyo, akashauri kwamba tuimarishe vifaa pamoja na *consumables* na maabara zenyewe kuanzia ngazi za chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda hapa nieleze tu kwamba kwa kupitia shirika letu la Bima ya Afya, kuanzia mwaka huu kuna pesa zimetengwa zaidi ya shilingi bilioni ambazo Halmashauri zinaweza kukopa kwa ajili ya kuimarisha vifaa vya maabara katika zahanati. Hili tulilisema katika hotuba yetu na hizo pesa zipo, kinachohitajika ni halmshauri kujua namna ya kuzipata hizo pesa. Ni mikopo nafuu, nia ni kwamba Serikali haiwezi kuhimili misukosuko yote ya bajeti na kwa chombo kama hiki kujitolea namna hii ni kitu cha kuwapa pongezi.

Ukazungumzia na kuwapa pongezi MEWATA na sisi tunaendelea kuwapa pongezi na kwamba kama MEWATA wameweza kufanya kazi kubwa kama ile kwa nini Serikali ishindwe. Serikali haijashindwa na labda niseme tu kwamba katika yote yanayofanyika na MEWATA, Serikali ina mchango mkubwa sana, hawa MEWATA wanaoshughulika wote ni wafanyakazi wa Serikali. Kwa hiyo, unaposikia wapo Mwanza wameacha vituo vyao vya kazi sisi tunawasafirisha na kuwapeleka kule, lakini hata vifaa wanavyotumia na maeneo yenyewe kama hospitali, kama *theatre* ni za Serikali, hivyo sisi tunashauri tu kwamba watu waendelee kujitolea kuwasaidia na hata vikundi vingine vya namna hii vyenye nia nzuri kama hii vikijitokeza tuweze kuwasaidia.

Mheshimiwa George Malima Lubeleje, amesisitiza kwamba tiba sahihi hutegemea uchunguzi sahihi. Suala hili tunakubaliana nalo kabisa na kwamba kuwe na maabara katika vituo vya afya vyenye vifaa vya kisasa na pia tuangalie suala la upungufu wa wataalamu na kuongeza vyuo. Nadhani hili wajumbe mtakuwa mmechoka, nimelizungumzia mara nyingi na amefurahishwa na suala la miiko. Kuhusu maabara

katika vituo vya afya hili lina sura mbili: moja, ni la wafanyakazi ambalo tunaliangalia kwa kuongeza idadi lakini vilevile kwa upande wa vifaa nimezungumzia huu utaratibu ulioanzishwa na Shirika la Bima ya Afya kwamba Halmashauri zinao uwezo wa kukopa hela kwa ajili ya kuimarisha hii sekta ya vifaa.

Mheshimiwa John M. Cheyo amesema utaalamu wa maabara katika zahanati umepotea, fani hii itambuliwe. Tunaomba tuchukue hilo lakini utakuta miswada mitatu hii inayoshabihiana toka jana yote tumezungumzia kwamba ni fani ambayo tujaribu kuangalia upya tuone kwamba ni namna gani ya kuwavutia vijana wetu waingie kwenye fani hii na wabaki katika fani hiyo. Vilevile umeshauri kwamba Baraza lisimamie kwa makini maadili na tumekubaliana kabisa na ukauliza kwamba huyu anayetoa ripoti ambazo sio sahihi halafu zinampa matatizo mgonjwa yeye atashughulikiwa namna gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, makosa yanaweza yakatokea katika shughuli nzima za kutibu wagonjwa; yanaweza kuwa ama mtu hajui au ni mzembe, lakini uzembe ambao tunaona kwamba ni *negligence* mtu anaweza hata akapoteza kazi halafu akashitakiwa katika Mahakama, hiyo ipo.

Halafu ukashauri kwamba kwa nini tusiwe na *diagnostic centers* na nadhani umewahi kufika *Harry street,* maana yake umetoa huo mfano na hata Afrika Kusini. Sasa kama mnavyofahamu Serikali sasa hivi haijiingizi kwenye biashara, inaweka mazingira ambayo itawawezesha watu wengine kuwekeza nchini na watu wa kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo hospitali Dar es Salaam, ipo karibu na Mzizima ambapo ukienda pale unaweza ukapimwa, wana *executive examination,* unaweza ukaenda na fedha zako ukalipa. Wanapima kila kitu ambacho wanaweza kufanya hivyo. Kwa hiyo, tukiwa na utaratibu huo na hasa kwa sisi Waheshimiwa Wabunge inaweza ikatusaidia tukabaini matatizo mapema kabisa. Vitu kama *cancer a prostate* ni kitu ambacho kinakwenda taratibu sana mpaka unapokuja kuigundua itakuwa imekwishafika mbali. Kwa hiyo, ni ushauri tu ambao ningefikiria kwamba wanafanya kazi nzuri na tujaribu kupita pale, na madaktari wanapenda kusikia na kumwambia mgonjwa ni mzima sio kila wakati umwambie unaumwa kitu fulani.

Mheshimiwa Cheyo pia ulikuwa umeshauri tukiwa na vitu kama hivyo, mgonjwa akiugua akimbilie kwenye kituo kama hicho badala ya kwenda kwa daktari, aende tu na vipimo. Katika taalauma ya kidaktari tunafikiri tungeanza *the other way round* kwamba uende kwa daktari, yeye ndiye anajua ni vipimo gani vingehitajika ili kumsaidia kubaini ni ugonjwa gani.

Pia aliuliza kwamba hawa wanaoanzisha maabara wanasimamiwa na nani, wanasimamiwa na sheria hii, hapa tunazungumzia usajili kwa wafanyakazi, teknolojia. Lakini maabara na ubora wake viko katika sheria tofauti, tuna chombo kinaitwa *Private Health Laboratories* ambacho kina muundo wake wa usimamizi. Vilevile Mheshimiwa Cheyo, ametukumbusha kwa nini anaitwa bwana mapesa, akasema kwamba hawa

madaktari badala ya kwenda kwenye kliniki nje wanakuwa wamechoka wanaweza kufanya kazi vizuri, bora tuwajaze mapesa mfukoni wasishawishike kwenda huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda utakuwa na taarifa kwamba ni kweli madaktari wanakwenda kwenye hospitali hasa za kwao au za watu binafsi. Waliruhusiwa kuondoka baada ya saa kazi, lakini wengine wanatumia mwanya huo kwenda hata nyakati za kazi.

Tunachokifanyia kazi sasa hivi ni kwamba kama daktari aliyeajiriwa Muhimbili anahitajika kwenda Aga Khan kwa sababu ya taaluma yake basi isiwe kwenda kwa kutoroka. Tuwe na *memorandum*, tunajua kwamba Dr. Slaa yuko *CCBRT* Jumatano mchana. Kwa hiyo, usije Muhimbili kumtafuta kwa sababu yuko kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaingia mkataba na hawa wanaomtumia mtu wetu, tunalipana na kiasi kilichopo ndiyo tunapewa. Mheshimiwa Dr. Slaa ndiyo tunalifanyia kazi ili watu wasiwe wanatoroka. Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya amezungumzia habari za maabara kuwa zipo katika maeneo maalumu tu ya vituo vya kutolea afya.

Lakini kuna wananchi wengi ambao hawana uwezo wako vijijini, kwa nini tusiwe na *mobile laboratories.*Kwa kawaida *laboratory* inamsaidia mganga kufikia uamuzi ni nini atibu. Sasa *mobile clinics* tunazoweza kuzipeleka katika vijiji ni zile za Programu kama ya kupima Ukimwi, kwa sababu wote unataka uwapime Ukimwi. Lakini kwa magonjwa machache ambayo unaweza ukaenda ukapima watu wote halafu uanze kuja kurudi tena kusema fulani tulikupima siku ile tumekuta kuna matatizo kama haya, hii itakuwa ngumu na itakuwa gharama isiyo na maana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa programu ni kweli kuna kliniki za namna hii ambapo tunawafuata wagonjwa na tunawapima. Kwa hiyo, nichukue ushauri wake kwamba nadhani anachozungumzia ni kwamba tuongeze hizo, tuimarishe na tuongeze ziweze kuwafikia watu wengi mara nyingi zaidi kuliko ilivyo sasa. Suala hili alilozungumza Mheshimiwa Stella Manyanya ndilo alilozungumza kwenye mchango wake wa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ningependa nikushukuru tena kwa nafasi uliyonipa. Naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa kwa Mara ya Pili)*

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Wataalamu wa Maabara za Afya wa Mwaka 2007 *(The Health Labaratory Practitioners Bill, 2007)***

Ibara ya 1

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya2
Ibara ya 3

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 4

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 5
Ibara ya 6

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya7
Ibara ya 8
Ibara ya 9

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 10
Ibara ya 11

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 12
Ibara ya 13

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 14

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 15
Ibara ya 16
Ibara ya 17
Ibara ya 18
Ibara ya 19

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 20
Ibara ya 21
Ibara ya 22

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 23
Ibara ya 24
Ibara ya 25
Ibara ya 26
Ibara ya 27
Ibara ya 28
Ibara ya 29
Ibara ya 30
Ibara ya 31
Ibara ya 32
Ibara ya 33
Ibara ya 34
Ibara ya 35
Ibara ya 36
Ibara ya 37

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 38

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 39
Ibara ya 40

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 41

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa masahihisho. Ibara ya 41 haina masahihisho. Iliyo na marekebisho ni Ibara ya 43.

**NAIBU SPIKA:** Kwa hiyo, Ibara ya 41 pamoja na marekebisho inaafikiwa?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nasema Ibara ya 41 haina marekebisho.

**NAIBU SPIKA:** Ibara ya 41 ndiyo yenye marekebisho?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Yenye marekebisho ni Ibara ya 45.

**NAIBU SPIKA:** Kwa hiyo, Ibara ya 41 haina marekebisho?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa natoa masahihisho kwamba Ibara ambayo inapaswa kufanyiwa marekebisho ni 45 na siyo 41.

**NAIBU SPIKA:** Kwa hiyo, Ibara ya 41 ilivyo?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Haina marekebisho yoyote.

**NAIBU SPIKA:** Hata yaliyowasilishwa?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Ndiyo sababu nasema nafanya masahihisho kwenye kile kilichowasilishwa kwenye *schedule of amendments.*

**NAIBU SPIKA:** Kwa hiyo, Ibara ya 41 haina marekebisho.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 42

Ibara ya 43
Ibara ya 44

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 45

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 46

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 47
Ibara ya 48
Ibara ya 49

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 50

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 51

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 52
Ibara ya 53

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Jedwali

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Watalaamu wa Maabara za Afya wa Mwaka 2007 *(The Health Laboratory Practitioners Bill, 2007)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria uitwao, *The Health Laboratory Practitioners Bill, 2007* pamoja na mabadiliko yake, kifungu hadi kifungu na kuukubali. Hivyo basi naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa huo sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria wa Serikali Ulisomwa kwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumemaliza shughuli za Miswada ya leo. Nafikiri kesho pia tutakuwa na miswada inayofuata. Ninalo tangazo kwamba Chama cha Wanawake wa Bunge, kupitia Katibu wake Mheshimiwa Switi, anawatangazia Wabunge wanawake kwamba kesho tarehe 2/11/2007 kutakuwa na kikao kifupi sana katika Ukumbi wa Msekwa baada ya kipindi cha maswali.

Lakini nawashukuru sana kwa kazi tulizofanya. Pia nazishukuru Kamati zote mbili, Kamati ya Huduma za Jamii, kwa kazi nzuri waliyofanya kupitia Miswada hii kwa makini sana na ndiyo maana kulikuwa na marekebisho mengi kwenye Muswada wa asili. Kwa hiyo, ni dalili kwamba Kamati imefanyakazi yake vizuri. Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge, kwa kazi ya siku ya leo. Kwa hiyo, sasa naahirisha kikao mpaka kesho saa 3.00 asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 12.18 Jioni Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Ijumaa tarehe 2 Novemba, 2007 Saa 3.00 Asubuhi)*